Hakikat Kitabevi Toleo Namba 1

# Iman na Uislam

Tafsiri ya ITIQAD-NAMA

NA

**MAWLANA DHIYA’ AD-DIN**
**KHALID AL-BAGHDADI**

Toleo la Kituruki lilitolewa na

**Hüseyn Hilmi Işık**

**TOLEO LA SITA**

**Hakikat Kitabevi**
Darüşşefeka Cad. 53/A P.K.: 35
**34083** Fatih-ISTANBUL/TURKEY
Tel: 90.212.523 4556–532 5843 Fax: 90.212.523 3693
http://www.hakikatkitabevi.com
e-mail: info@hakikatkitabevi.com
2022

# KUMBUKA

Mwandishi wa kitabu Itiqad-nama, Mawlana Dhiya'ad-din Khalid al-Baghdadi al-Uthman (alizaliwa mwaka 1192 hijri sawa na 1778 miladi katika mji wa Shahrazur kaskazini mwa Baghdad, na alifariki dunia mwaka 1242 hijri sawa na 1826 katika mji wa Damascus (syria) quddisa sirruh), Aliitwa Uthman kwa sababu anatokana na ukoo wa Uthman Dhu'nurain "radiyallahu anhu" ambaye ni khalifa wa tatu. Alipokuwa anamfundisha ndugu yake Hadhrat Mawlana Mahmud Sahib hadithi ambayo ni maarufu sana kama **Hadithi al-Jibril**, na ndio ya pili ndani ya kitabu **Al-ahadith al-arbaun** zilizotolewa na mwanazuoni maarufu **an-Nawawi**, Hadhrat Sahib alimuomba kaka yake mkubwa kuifafanua zaidi hadithi hiyo. Mawlana Khalid, ili kuuridhisha moyo wa mdogo wake na kulitimiza ombi lake alikubali kuifafanua hadithi as-sharifu hiyo na akatunga kitabu kwa lugha ya kifursi kwa jina la **Itiqad-nama**. Tafsiri yake kwa lugha ya kituruki kinaitwa **"Herkese Lazim Olan Iman".** Kitabu hiki kilitafsiriwa kwa lugha ya kingereza na kuitwa Belief and Islam, Kifaransa **(Foi et Islam)** na Kijerumani **(Glaube und Islam)** mwaka 1969, na baadae kikatafsiriwa katika lugha mbali mbali kama: Kitamil, Kiyoruba, Kihausa, Kimalayalam na Kidanish. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Awabariki vijana wetu wasio na hatia kwa kusoma na kujifunza itiqad sahihi (iman) kama ilivyofikishwa na wanazuoni wa Ahl as-Sunna.

---

**Kumbusho la mchapishaji:**

Yeyote anayetamani kukichapisha kitabu hiki kwa nakala yake asili au kukitafsiri kwa lugha nyengine anaruhusiwa kufanya hivyo. Pia na watu wanaofanikisha manufaa ya tendo kubwa hili wanapewa vibali kupata baraka ambazo baadae tunaziendeleza mbele ya Mwenyezi Mungu kwa majina yao, Pia tunawashukuru sana. Hata hivyo, ruhusa inategemea na hali ya karatasi zinazotumika wakati wa kuchapisha kwani ni lazima ziwe nzuri na ubunifu wake uwe mzuri na maandishi yawe yamewekwa vizuri bila makosa yeyote.

**Tahadhari:** wamisionari wanafanya juhudi kubwa kutangaza Ukristo. Wayahudi nao wanafanya bidii kusambaza Talmudi. Hakikat Kitabevi (hifadhi ya vitabu) Istanbul wanapambana kutangaza Uislamu na freemason wanafanya jitihada za kuiangamiza dini. Mtu mwenye busara, elimu na upambanuzi atafahamu na atafuata moja ya hizo njia, ile iliyo ya ukweli; na atasaidia kusambaza uwokovu huo kwa binadamu wote. Hakuna njia bora zaidi na ya thamani ya kuwahudumia binadamu kuliko kufanya hivyo.

**"Subhana-Allahi wa bi-hamdihi subhan-Allahil-adhim."** Dhikiri hii inayoitwa Kalima-i-tenzih, ikitajwa na mtu kila asubuhi mara mia moja (100) na jioni pia kwa idadi hiyo hiyo, inamfanya mtu kusamehewa madhambi yake na inamfanya pia kulindwa dhidi ya kurejea kutenda maovu tena. Dhikiri hii pia imenukuliwa kutoka kwenye barua ya mia tatu na saba (307) na mia tatu na nane (308) katika juzuu ya kwanza kwenye kitabu kinachoitwa **Maktubat** kilichoandikwa na walii pia mwanazuoni mkubwa Imam Rabbani quddisa sirruh vile vile kwenye toleo la kituruki.

Ya Rahman, Ya Rahim, Ya Afuwwun, Ya Karim.

Lengo la **Hakikat Kitabevi** (hifadhi la vitabu tukufu linalopatikana Fatih, Istanbul) ni kuielimisha imani yetu, Uislamu na kuifanya nchi yetu iliobarikiwa ipendwe na watu ulimwenguni. Tunamuomba Allahu Taala awe radhi na watu wanaotusaidia, Amin.

Mpenzi msomaji, Assalamu alaikum warahmatullahi wabaraqaatuh.

Maandishi yote ndani ya kitabu hiki yamenukuliwa kutoka kwenye vitabu vilivyoandikwa na wanazuoni Waislamu. Hatujaongeza kitu chochote kwenye nakala hizi. Tumefanya kazi hii ambayo ni muhimu sana kwa madhumuni maradufu, kutumikia watu na pia kutambulishwa kutoka kwenye watu wanao fanya kazi kwa lengo la kufanya watu wafurahie maisha yao na wale wanaopigania au wanaolinda haki za binadamu. Unaposoma maandishi ya hawa wanazuoni wakubwa ulimwenguni kote kwa uangalifu na kuyatilia maanani, utapata elimu yenye manufaa In shaa Allahu taala. Tunaeneza Salamu zetu na upendo wetu kwenu.

Tunamuomba Allahu taala akubarikini afya njema na maisha marefu yenye mafanikio, Amin.

Wa salla-Allahu alaa Sayyidina Muhammadin wa alaa Ali Muhammadi wa barik alaa Sayyidina Muhammadin wa alaa Ali Muhammadi. Allahumma Rabbanaa atinaa fi-d-dunia hasanatan wafil-akhirat-i-hasanatan wa qina adhab-an-nar bi-rahmatika ya Arhamar-Rahimiin. Amiin.

**Hakikat Kitabevi**

# DIBAJI

**Tunaanza kitabu na Basmala: jina lake Allah ndio lenye ulinzi bora. Zawadi zake hazina kipimo. Ni mwingi wa rehma na anapenda sana kuwaondolea waja madhambi na kuwasamehe.**

Allahu taala anawafungulia milango ya kutafuta kile watakacho watu wote waliopo ardhini. Ameumba vitu venye faida na kuvituma au kuwiteremsha kwa kila mtu, na anawaongoza njia ya kupata furaha ya kudumu. Na vile vile anawaongoza awatakao kwenye njia sahihi miongoni mwa wale watu ambao waliiacha njia hijo (siratwal-mustakim) wakakufuru kwa sababu ya kudanganywa na nafsi zao potofu au makundi mabaya au vitabu vyenye madhara makubwa au vyombo vya habari baadae wakatubu. Na anawaokoa kutoka kwenye kuangamia kwa milele. Hawateremshii neema zake wale wenye jeuri ya kupindukia anawaacha kuendelea kuishi ndani ya upotofu walioupenda na kuuridhia. Siku ya mwisho (kiama) atawasamehe wale atakaopenda miongoni mwa waumini waliostahiki kuingia motoni (jahannam) na atawaingiza peponi (janna). Yeye pekee ndie muumbaji wakila kitu ambacho kina uhai, Allah ndiye anayelinda kila kitu kwa muda wote dhidi ya hofu na vitisho. Kwa kujiamini sisi wenyewe kubitia jina la Allahu taala na kutegemea msaada kutoka Kwake tunaanza kuandika kitabu hiki.

Sifa njema ni zake Allahu taala. Amani na baraka ziwe juu ya kipenzi chake Mtume Muhammad "alaihis-salaam". Na sala bora ziwaendee watu wa nyumba yake (Ahl al-Bayt) na juu ya wale wote

ambao wameipigania dini hii ili isonge mbele (maswahaba zake/ as Sahabat al-kiram).

Maelfu ya vitabu vyenye thamani vimeandikwa kuhusu mafundisho ya imani, yanayoamrishwa na yanayokatazwa na Uislamu, na vingi miongoni mwa vitabu hivi vimetafsiriwa kwenye lugha tofauti tofauti za kigeni na kusambazwa kila nchi. Kwa upande mwingine, watu wabaya (zindiki) ambao hawaoni mbali na majasusi waingereza mara kwa mara wanashambulia faida za Uislamu, ukarimu na mwanga wake yaani yale yalioamrishwa na yale yaliokatazwa kwamba eti yanakiuka haki za binadamu hivjo hujaribu kuyafanyia mabadiliko pamoja na kuwadanganya Waislamu.

Hata hivyo, tunashukuru kwamba sasa hivi kila sehemu (nchi) wanazuoni wakiislamu wanafanya juhudi kubwa kuueneza na kuulinda Uislamu. Wanazuoni Waislamu walioandika vitabu kwa kusikia kutoka kwa masahaba Watukufu wa mtume "swallallahu alaihi wa sallam" wanaitwa **Wanazuoni wa Ahl as-Sunna**. Hotuba zisizofaa na makala kwa upande mwingine yameshuhudiwa ambayo yanatajwa kuwa yametolewa kwa kutumia Quran tukufu na hadithi za mtume na kikundi cha watu ambao hawana ufahamu sahihi wa Quran na Hadithi na hawajapitia na kusoma vitabu vilivyoandikwa na wanazuoni wa **Ahl as-Sunna**. Hotuba hizi na makala haya yamethibitishwa kuwa ni yenye ufanisi usiofaa kwa ndugu zetu Waislamu, ila yanawaonyesha tu ujinga wa mawakala wake.

Mtu yeyote anayedai kuwa Muislam au akaonekana anasali jamaa basi huyu mtu anafaa kutambulika kama Muislam. Baadae akionekana kwenye mazungumzo yake kwa mfano, maandishi yake au katika mwenendo wake ikitokea kitu ambacho kina hitilafu na mafunzo ya imani kama yalivyoelezewa na wanazuoni wa **Ahl as-Sunna**, basi ataambiwa kwamba anayoyafanya ni kinyume na Uislamu na asipoacha yatamfanya kuwa mpotofu au murtadi (mtu ambaye ametoka kwenye Uislamu baada yakua Muislamu). Na atatakiwa kuyaacha kabisa na kutubu. Na kama kwakutumia akili yake duni akapuuza anayoambiwa na kusema kwamba hataacha anayoyafanya basi huyu anafahamika kuwa ni mpotofu au murtadi. Hata akiendelea kusali sala (namaz) tano kila siku, akaenda Makka

na akafanya hijja na akaendelea kufanya ibada tofauti na kutenda mema hatoepuka janga hili na hatokuwa Muislamu hadi pale atakapoacha kufanya mambo hayo yanayomfanya mtu awe kafiri na akafanya toba[1]. Kwa kujifunza vizuri vitu ambavyo vinamfanya mtu awe kafiri.

Ni jukumu la kila Muislamu kujikinga mwenyewe dhidi ya mambo yanayomtoa ndani ya Uislamu na kumsababisha kuwa murtadi, na pia anapaswa kuwatambua vyema makafiri na waongo ambao wanajifanya kuwa Waislamu, hasa majasusi wa uingereza na kukaa mbali na madhara yao.

Rasulullah "swallallahu alaihi wa sallam" alielezea katika hadithi sharif kwamba habari za uongo na zenye makosa zitatolewa ndani ya Quran tukufu na hadithi sharif nakusababisha makundi sabini na mbili (72) potofu kujitokeza. Hadithi sharif hii inafafanuliwa kwenye vitabu **al-Beriqa na al-Hadiqa**, ambavyo vilinukuu hadithi sharif hii kutoka kwenye vitabu viwili (2) maarufu **Bukhari na Muslim**. Hatupaswi kuamini vitabu na mihadhara ya kikundi hiki cha watu ambao wanajitokeza kwa majina kama wanazuoni wa kiislamu au maprofesa wa dini. Na vilevile tunapaswa kuwa waangalifu ili tusianguke kwenye mitego ya wezi wa dini na imani hewa. Zaidi ya hayo Waislamu wasio na elimu au wenye elimu ndogo, makoministi, mafreemason pamoja na mamisionari wakikristo kwa upande mwingine mawahabi ambao wamepokea mafunzo kutoka kwa waingereza na Mayahudi, wanafanya jitihada kupoteza watoto wa Waislamu kwa kufufua na kutumia mbinu mpya. Wafanya wawezalo ili kuteketeza au Kuangamiza Imani na Uislamu kwa kutumia makala zenye uongo, filamu, kumbi za michezo, redio na matangazo ya runinga pia mitandao ya kijamii kama facebook, twitter, whatsApp, google, yahoo nakadhalika. Wanatumia mamilioni ya fedha kufanikisha lengo hili. Wanazuoni wa kiislamu "rahmatullahi alaihim" wamefanya jitihada kwa kuwajibu watu hao na wameendelea kuonesha njia ya Allahu taala ambayo ni yenye

[1] Kufanya toba ya madhambi maana yake ni kujuta kwakufanya dhambi, kisha ukamuomba Allahu taala msamaha, kwa mfano kwakusema dua hii “Astaghfirullah al-adhim al-ladhi lailaha illa Anta Huwal hayy-ul-qayyum wa atubu ilaih” na kumuahidi Allah kutorejea kufanya madhambi tena.

furaha na uokovu. Miongoni mwa hao, tumechagua kitabu kinachoitwa **Itiqad-nama** kilichoandikwa na mwanazuoni maarufu Mawlana Dhiya'ad-din Khalid al-Baghdadi al-Uthmani quddisa sirruh ambaye ni. **Itiqad-nama** ni kitabu kilichotafsiriwa kwa lugha ya kituruki na marehemu Haji Fayzullah Efendi mkaazi wa Kemah, Erzincan, nakupewa jina **Faraid al-fawaid** na kuchapishwa mwaka 1312 A.H Egypt. Tafsiri hii imerahisishwa kwa jina Iman na Uislamu. Toleo lake la kwanza ni mwaka 1966. Maelezo yetu yamewekwa kwenye mabano. Tunamshukuru Allahu taala kwa kutujaalia kuweza kuchapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa mara ya kwanza. Asili ya kitabu hiki Itiqad-nama, ni lugha ya kifursi na bado ipo kwenye maktaba ya chuo cha Istanbul (Idara ya Ibnul Emin Mahmud Kemal, nambari F. 2639). Tafsiri yake ya Kituruki ilichapishwa na **Hakikat Kitabevi** kwa jina la `**Iman ve Islam**`.

Katika kitabu **(Durr ul-Muhtar)** kilichoandikwa na mwanazuoni mkubwa Alauddin-i Haskefi "rahmatullahi alaih", mwisho wa mlango wa ndoa ya kafiri anaelezea kwamba, " binti wa kiislamu aliyeolewa au kuposwa halafu akabaleghe au kutimiza miaka ya utu uzima na akawa hajui nguzo za iman na hajitambui kama ni Muislamu basi ndoa yake inakuwa batili (anakuwa murtadi). Anapaswa kufundishwa majina ya Allahu taala na anafaa kuyarudia na kusema ninaamini haya. Kufafanuwa haya, mwanazuoni Ibn Abidin "rahmatullahi alaih" alisema mtoto wa kike anapokuwa mdogo hufuata itiqadi ya wazazi wake, na anakuwa Muislamu. Lakini anapokuwa (kubaleghe) hafati tena itiqadi ya wazazi wake kwa sababu anajiamulia mwenyewe. Anapotimiza umri wa utu uzima (kubaleghe) na akawa hana elimu kuhusu Uislamu na hajitambui kuwa Muislamu basi anakuwa murtadi. Akijifunza nguzo sita za Imani bila kuamini na asipojua umuhimu wa Uislamu, basi hata akitamka kalimatu tawhid (akitoa shahada) yani La ilaha illallah Muhammad rasulullah hawezi kuendelea kama Muislamu. Anafaa kufahamu mambo sita ndani ya (Amantu billah...) pia amri zake Allahu taala kuzikubali na aliyoyakataza kuyaacha. Ibn Abidin katika uchambuzi huu anaonesha kwamba mtu kafiri akisema kalimatu tawhid na akaamini maana yake basi mda huo anakuwa Muislamu. Lakini kama Waislamu wengine akipata nafasi anafaa kukariri maneno yafuatayo pamoja na maana yake: **"Amantu bi'llahi wa Mala'ikatihi wa Kutubihi wa Rusulihi wal-yawm-il-akhiri wa bil-**

**qadari khairihi wa sharrihi minallahi taala walba'thu ba'dal maut haqqun ash-hadu an la ilaha illallah wa ash-hadu anna Muhammadan abduhu wa Rasuluhu."** Pia mtoto wa kiume (kijana) ambaye ni Muislamu asipojifunza nguzo sita hizi na akasema kwamba anaziamini anakuwa murtadi anapofikisha umri wa utu uzima (kubaleghe). Baada ya kujifunza nguzo hizi sita na kuziamini basi anakuwa amepata Imani, baada ya hapo anawajibika kutafuta mafundisho ya kiislamu yote na kujielimisha, kwa mfano kujua amri za Uislamu zinazoitwa **farz** na yaliokatazwa yanayoitwa **haramu**, jinsi ya kutia udhu, kuoga, sala inasaliwa vipi, mtu anasitiri vipi (awrat) utupu wake/sehemu za siri. Anapouliza mtu kuhusu mafunzo haya basi ni lazima kwa yule alieulizwa kumfundisha au kumuelekeza kitabu sahihi kitakachomsaidia kupata maelezo hayo. Akikosa kupata kitabu au mwalimu basi ni lazima atafute mmoja au kitabu. Binti wa kike Muislamu naye anawajibika kama anavyowajibika mtoto wa kiume. Basi pale anaposhindwa kutafuta mwalimu au kitabu kuhusu dini yake ya Uislamu anakuwa kafiri. Atapata udhuru kwakutojua endapo ataendelea kutafuta mwalimu au kitabu sahihi cha kiislamu. Asipotafuta basi anakuwa kafiri moja kwa moja. Muislamu ambaye hatimizi farz (yale yalioamrishwa na Uislamu) kwa wakati wake au akatenda maovu (haramu) basi ataingizwa kwenye moto wa jahannam. Kitabu hiki cha Imani na Uislamu kinaelezea kwa kina mafunzo kuhusu nguzo sita za Imani. Basi kila Muislamu anapaswa kusoma kitabu hiki vizuri na afanye awezalo ili watoto wake na wale anaowajua wapate kukisoma. Sehemu za awrat (utupu) zimefafanuliwa zaidi katika kitabu Endless Bliss juzuu ya nne. Katika maandishi ya kitabu hiki maana ya ayet-i kerima imeitwa ma'al inayomaanisha 'maana' kama yalivyotolewa na wanazuoni wa Tasfiri kwani ayet-i karima au Quran tukufu maana yake aliifahamu mtume "swallallahu alaihi wa sallam" peke yake, na halafu aliwafundisha masahaba zake. Wanazuoni wa tafsiri (ufafanuzi wa Quran tukufu) walitofautisha na kuchuja hadithi zilizoletwa na wanafiki na mazindiki ambao walipata mafunzo ya dini kutoka kwa Waingereza kama watu wasiofuata madhehebu ili waweze kuiharibu dini, na kuhusu zile hadithi sharif wasizofahamu wanazitafsiri kulingana na maoni yao. Kinachofahamika na watu hao ambao hawajasoma dini ya Uislamu na wanasema kiarabu bila elimu ya Tafsiri, basi ufafanuzi wao haujulikani kama tafsiri ya

Quran tukufu. Ndio sababu hadithi sharif inasema kwamba: **'Mtu anayetafsiri Quran karim (tukufu) kulingana na ufahamu wake basi anakuwa kafiri.** Kamusi ya kiarabu na maneno mengine yasiokuwa ya kingereza na ni mageni kwa msomaji wa kiingereza yanaongezwa.

Tunamuomba Allahu taala Atuongoze kwenye njia sahihi ambayo ilioneshwa na maulamaa wa Ahl as-Sunna: Tunamuomba pia atulinde dhidi ya kuamini uongo, udanganyifu na kuendelea kukubali uongo wa maadui wa Uislamu wanaojiita La-madhhabi yani wasiokuwa na madhehebu rasmi wanaotumia majina kama maulamaa wakuu wa Uislamu.

Vitabu vyote vinavyochapishwa kwenye lugha nyingi tofauti vinasambazwa ulimwenguni kote kwa kutumia mtandao wa internet.

**KUMBUSHO:** Wakristu wanajitahidi kuutangaza ukristu, Wayahudi nao wanajaribu kueneza Talmud, Hakikat Kitabevi wanafanya wawezalo kutangaza Uislamu na wa freemasons wanapigania kuangamiza dini. Mtu mwenye akili, mwenye elimu na mwenye hoja atatumia mantiki yake na kufanya chaguo sahihi. Kwakutoa msaada kwa uenezaji wa njia sahihi, itakuwa sababu ya binadamu kupata furaha katika dunia hii na baadae (Akhera).

Ulimwengu wa Uislamu hivi sasa umegawanyika kwenye makundi makuu matatu. Kundi la kwanza ni Waislamu wa ukweli ambao wanafuata nyayo za masahaba wa mtume "swallallahu alaihi wa sallam". Na hao wanaitwa **Ahl as-Sunna au Sunni Muslims au Firqa-i-naajiya**, inayomaanisha kundi ambalo limejiokoa kwenye moto. Kundi la pili ni maadui wa masahaba, na hao wanaitwa **Shia** (mashia) au **Firqa-i-dalla** (kundi lililopotea). Kundi la tatu linaitwa **Wahhabi** au **Najid**, mahali pa kuzaliwa kwao ni Najid Uarabuni. Na vilevile wanajulikana kama **Firqa-i-mal'uuna** (kundi lililolaaniwa). Na katika kitabu chetu kinachoitwa **Endless Bliss** (Neema zisizo na mwisho) na **The Rising and the Hereafter** (Kufufuka na Kiama) inaelezewa kwamba watu hawa wanaita Waislamu 'makafiri'. Na mtume wetu "swallallahu allaihi wa sallam" alilaani watu wanoita Waislamu vile. Uislamu kugawanyika kwenye makundi matatu haya ni natija/matokeo ya hila za Wayahudi na Waingereza.

Kila Muislamu anapaswa kusema **“La ilaha illallah”** mda wote ili kuitukuza nafsi yake, mfano kuitukuza nafsi yake kutokana na ujinga na maovu ambayo yanaathiriwa na maumbile. Na daima anafaa kuirudia dua hii **“Astaghfirullah,”** ili autakase moyo wake, mfano kuuokoa moyo wake kutokana na ukafiri na maovu ambayo yameufunika moyo wake kwa sababu ya nafsi yake kujiingiza kwenye kundi la shetani na maovu, na katika kusoma vitabu hatari. Dua za watu wenye kuufuata Uislamu na kufanya toba kwa makosa yao waliofanya zitakubaliwa na Allahu taala. Mtu asiposali namazi (sala) tano kila siku, na akawatizama wanawake ambao hawajajifunika vizuri na wengine wanaonesha awrat (utupu) wao, na akala akanywa yale yalio haramu, basi itahitimishwa kwamba mtu huyu hafuati Uislamu. Na dua zake hazitokubalika.

| **Miladi** | **Hijri Shamsi** | **Hijri Kamari** |
|---|---|---|
| **2001** | **1380** | **1422** |

## UTANGULIZI

Kwa mwanzo mwenye baraka na mzuri, Mawlana Khalidi Baghdadi ‘quddisa sirruh’ anaanza kitabu chake kwa kunukuu barua ya 17 ambayo imo katika juzuu ya tatu (3) kwenye kitabu **Maktubat** kilichoandikwa na al-Imam ar-Rabbani Ahmad al-Faruqi as-Serhendi[1] "rahmatullahi alaih". Imamu Rabbani ‘quddisa sirruh’ ndani ya barua hiyo anaeleza kama ifuatavyo;

Naanza barua yangu na Basmala. Utukufu usio na kikomo na shukrani ni za Allahu taala ambaye ameteremsha neema za kila aina juu yetu na neema kubwa zaidi ni ya kutujaalia kuwa Waislamu na akatuthamini kwa kutuweka ndani ya umma wa mtume Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam" na ndio neema ya juu zaidi.

Hatunabudi kutafakari na kutambua kwamba Allahu taala pekee ndie anayebariki kila mtu na neema zote, Yeye pekee ndie anayeumba kila kitu ulimwenguni, Yeye pekee ndie anayelinda kila

[1] Imamu Rabbani alifariki mwaka 1034 sawa na 1624 miladi.

kilichopo hai kuishi, Nguvu na sifa njema za binadamu ni baraka na neema zake. Uhai wetu, maarifa, nguvu, hisia za kusikia na kuongea vyote ni kutoka kwake. Mara kwa mara ndie pekee anaeteremsha baraka na neema zisizokua na mwisho. Ndie pekee anayeokoa binaadamu kutoka kwenye tabu na dhiki, ndie anayekubali dua za binaadamu na kuwaondolea dhiki na huzuni. Yeye ndie anatengeneza riziki na kufanya zitufikie sisi. Baraka zake ni nyingi mno na kwa sababu hiyo hawakatii riziki zao wale ambao wanafanya maovu. Ufichaji siri wake ni mkubwa mno na ndio maana hawa jiaibishi wala hawafanyi kudharauliwa na wengine wala hawavui vyeo vyao wale wasiotii amri zake na kujiepusha na yale alioyakataza. Ni mwenye kupenda sana kusamehe, na ni mwenye rehma nyingi na haharakishi kuwaadhibu wale ambao wanastahiki kuadhibiwa. Anasambaza baraka na neema zake kwa wote wale anaowapenda (wanaomtii) na maadui zake (wasiomtii). Hamkatalii kitu mtu yoyote na kwa ihsani yake yenye thamani kubwa anatuonesha njia sahihi kuelekea furaha na uokovu. Anatuonya tusipotee njia ili tuweze kwenda peponi. Na pia anatuamrisha kumfata kipenzi chake mtume "swallallahu alaihi wa sallam" ili tuweze kupata baraka zote bila kikomo na furaha isiyoisha, pamoja na ridhaa yake na mapenzi yake ndani peponi.

Kwa hiyo neema za Allahu taala ni dhahiri kama jua. Fadhila zinazotoka kwa wengine, kwa hakika zinatoka kwake. Na ndie anayefanya wengine kuwa wapatanishi. Na anatoa matamanio, nguvu na uwezo wa kusaidia. Kwa sababu hii, daima ndie pekee anayetuma neema zote kupitia kwa watu wote na sehemu zote. Kutegemea neema na baraka kutoka kwa mtu yeyote isipokuwa yeye ni kama kuomba kitu kutoka kwa mtu aliepewa akiweke amana to au kumuomba maskini sadaka. Jahili pia ni kama wenye elimu na wapumbavu ni kama wenye akili kwa kujua hayo tunayoyasema kuwa ya ukweli na yenye msimamo. Hata hakuna umuhimu wa kuyafikiria. Yule anaefanya wema anafaa kupewa shukrani na heshima. Kwa hivyo ni jukumu la kila binaadamu kumshukuru Allahu taala ambaye ametuneemesha na neema hizi. Jukumu linalo amrishwa na akili basi ni deni. Lakini si rahisi kutekeleza shukrani hizi kwake, binaadamu asili yake kwa kuwa kaumbwa hali ya kuwa hakuwepo kabisa, ni dhaifu, masikini, wanamahitaji na wana kasoro. Lakini kwa yeye Allah daima milele

yupo. Amejiweka mbali na kasoro yani yeye si kama binaadamu. Aina ya ukubwa wowote unamilikiwa na yeye tu. Binaadamu kwa njia yoyote ile hana ukaribu wowote au kufanana na Allahu taala. Kweli binaadamu ambaye ni duni sana, kumshukuru Allahu taala ambaye yuko juu ya kila kitu kwa njia ya kutakasa heshima yake. Kuna vitu vingi ambavyo binaadamu huona kama vizuri na vyenye thamani, lakini Allahu taala mwenyewe anajua kwamba ni vibaya na havitaki. Vitu vingi ambavyo tunaona kama vina umuhimu sana lakini vinaweza vikawa havitakiwi hata kidogo. Kwa sababu hii, binadamu na akili zao zenye kasoro na zisizoona mbali, haziwezi kubainisha vitu vinavyoonesha heshima na shukrani za Allahu taala. Isipokuwa jinsi ya kumshukuru na kumheshimu Allahu taala imeonyeshwa na Yeye Allahu taala, vitendo vinavyochukuliwa kama ni vya kumsifu vinaweza vikawa kashifa tena.

Kwa hivyo, heshima ya kuonyeshwa na majukumu ya binadamu kufanya kwa Allahu taala kwa moyo, ulimi na mwili yote yalielezwa na Allahu taala kupitia kipenzi chake mtume "swallallahu alaihi wa sallam"! Majukumu ya binadamu yaliyooneshwa na kuamrishwa na Allahu taala yanaitwa Islam (Uislamu). Mtu anamshukuru Allahu taala kwa kufuata mafunzo ya mtume wake aliofundisha. Allahu taala hakubali wala hataki kitu chochote kinachohusiana na ibada kinapotoka nje ya mafunzo haya ya mtume "swallallahu alaihi wa sallam", kwa sababu kuna mambo mengi ambayo binadamu huona kama ni mazuri hali ya kuwa Uislamu unayaona kinyume chake na hauyakubali na unayatambulisha kuwa mabaya.

Kwa hivyo, kwa kumshukuru Allahu taala, watu wenye akili wanapaswa kumfata mtume Muhammad "alaihis-salaam". Njia hii inaitwa **Uislamu**. Mtu ambaye anamfata mtume ´Muhammad "alaihis-salaam" huitwa **Muislamu**. Kumshukuru Allahu taala (Mwenyezi Mungu), inamaanisha kumfata Muhammad "alaihis-salaam", na kitendo hiki kinaitwa **ibada** (kuabudu). Mafunzo ya kiislamu ni ya aina mbili; ya kidini na ya kisayansi.

1) Mafunzo ambayo yanahitaji kuhifadhiwa na moyo yanaitwa **Usul-i-din** au mafunzo ya **Imani**. Kwa ufupi, **Imani** ni kuamini nguzo sita zilizofundishwa na Muhammad "alaihis-salaam" na kuukubali Uislamu na kujiepusha kusema na kutumia ishara za

kikafiri. Kila Muislamu anawajibika kujifunza ishara za kikafiri na pia kujiweka mbali nazo. Mtu mwenye Imani anaitwa **Muislamu**.

2) Mafunzo ya kuabudu ambayo yanafaa kutekelezwa na mwili na moyo yanaitwa farz (lazima) na yale ambayo yanayostahiki kuyaepuka yanaitwa **haramu**. Basi mafundisho haya yanaitwa **Furu-i-din** au **Ahkam-i-islamiyya** au **Mafundisho ya kiislamu**.

Kwa kusema **Kalima-i-tawhid (neno la tawhid)**, na kuamini maana na ukweli uliomo, ni jambo la kwanza kwa mtu yeyote kufanya. Kalima-i-tawhid (neno la tawhid) ni **“La ilaha illallah Muhammadun Rasulullah,”** na maana yake ni: “Mungu yupo na ni mmoja. Muhammad "alaihis-salaam" ni mtume Wake.” Kuamini ukweli huu inamaana “kupata au kuwa na Imani,” na “kuwa Muislamu.” Mtu mwenye Imani huitwa **Mu’min** (muumini) na **‘Muislamu.’** Imani ni lazima iwe ya kuendelea. Kwa hivyo, ni lazima kuepukana na vitendo ambavyo vinasababisha ukafiri na kutumia vitu ambavyo vinaashiria ukafiri.

Quran al-karim (tukufu) ni neno la Allah (Mungu). Allahu taala (Mwenyezi Mungu) aliliteremsha neno lake kwa Muhammad "alaihis-salaam" kama ujumbe kupitia kwa malaika Jibril (Gabriel) "alaihis-salaam". Maneno yaliyotumika ndani ya Quran tukufu yako katika lugha ya Kiarabu. Lakini yaliandaliwa na kupangwa aya moja baada ya nyengine na Allahu taala. Maneno yanayopatikana ndani ya Quran al-karim (tukufu) yalishushwa kwa aya, kwa mfano herufi na maneno yalipangwa upande kwa upande yani utaratibu na uratibu wa Quran wote ulipangwa na Allahu taala. Maana inayobebwa na herufi hizi na maneno yanachukua Kalam-i-ilahi (maneno ya Allahu taala). Herufi na maneno haya yanaitwa **Quran al-karim** (Quran tukufu). Maana inayoonesha kalam-i-ilahi (maneno ya Allah) ni Quran. Maneno ya Mungu Quran sio kiumbe. Kama ilivyokuwa kwa sifa zake Allahu taala Quran nayo haina mwanzo na itadumu milele. Kila mwaka Jibril "alaihis-salaam" alikuwa anamtembelea mtume "swallallahu alaihi wa sallam", na kusoma zile aya ambazo tayari zilikuwa zimeteremshwa kwa wakati huo kwa mpangilio kama zilivyopangwa kwenye Lawh-i-mahfudh, na mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam" alikuwa anarudia baada ya malaika mkuu. Kiumbe bora (mtume "swallallahu alaihi wa sallam") alipokuwa anakaribia kuondoka duniani kuelekea

akhera malaika mwenye thamani kubwa Jibril "alaihis-salaam" alimtembelea mara mbili, na kuipitia Quran tukufu yote. Mpendwa wetu mtume "salllahu alaihi wa sallam" na masahaba wengi wao walikuwa wameshaihifadhi Quran tukufu yote. Kwenye mwaka ambao kipenzi chake Allahu taala aliaga dunia, Abu Bakr as-Siddiq ambaye ni halifa wa kwanza wa mtume "swallallahu alaihi wa sallam" aliwakusanya pamoja masahaba wote waliokuwa wameisoma Quran na kuihifadhi kwenye vifua vyao na vipande vilivyokuwa vishaandikwa, na aliandaa kamati na kuikusanya Quran pamoja na kuiandika. Hivyo, kitabu kiitwacho **Mashaf**, kilitokea (nusha ya Quran tukufu ilioandikwa). Masahaba Elfu thelathini na tatu (33,000) walikusanyika pamoja wakakubaliana na kuhakikisha kwamba kila herufi imekaa pahali pake asili.

Matamko au maneno ya mtume Muhammad "alaihis-salaam" yanaitwa **hadithi as-sharifu** (hadithi tukufu). Miongoni mwa hadithi tukufu, zile ambazo maana yake ni kutoka kwa Allahu taala na kutamkwa na mtume Muhammad alaihis-salaam zinaitwa **hadithi-i-qudsi**. Kuna vitabu vingi vya hadithi lakini **Bukhari** na **Muslim** ndivyo vinavyojulikana zaidi.

Katika maamrisho ya Allahu taala (Mwenyezi mungu), mafundisho yanayoamrisha kuamini huitwa Iman, yanayopaswa kutekelezwa huitwa **Farz** (fardha) na yale yanayopaswa kuepukwa huitwa **Haram**. Farz na haram huitwa **Ahkam-i-Islamiyya** (hukumu za kiislamu). Mtu anaekanusha hata moja katika mafundisho ya kiislamu anaitwa **kafir (kafiri)**.

Kitu cha pili ambacho ni lazima mtu afanye ni kutukasa moyo wake. Na tunaposema “moyo”, vitu viwili vitafahamika. Kipande cha nyama kinachopatikana vifuani mwetu kinaitwa ‘moyo’ na kila mtu. Kwa maana hiyo moyo hupatikana hata kwenye wanyama. Moyo wa pili ni ule usioonekana na unakaa ndani ya moyo unaojulikana na kila mtu. Moyo huu wa pili pia huitwa nafsi. Ndio moyo huu ambao umeandikwa kwenye vitabu vya dini. Ndio moyo huu unaozingatia mafundisho ya Uislamu. Na ndio moyo huu tena unaoweza kuamini au kukanusha na kukataa mafundisho ya kiislamu. Moyo unaoamini ni safi na moyo unaokataa na kukanusha ni mchafu, umekufa. Ni jukumu letu la kwanza kusafisha moyo kwa kufanya jitihada sana. Kuabudu, hasa kutekeleza namaz (sala) na

kuomba dua maalumu (istighfar), inaiosafisha moyo. Kutenda yale yaliokatazwa na Mungu (haramu) huchafua moyo. Mtume wetu aliebarikiwa alisema: **“Sema istighfar sana! Muislamu akisema dua inayoitwa istighfar kwa wingi, Allahu taala anamlinda dhidi ya magonjwa yote na balaa zote. Anawateremshia riziq (vyakula) kutoka kwenye maeneo ambayo hawakutarajia hata kidogo”.** Istighfar ni kusema: **“Astaghfirullah”.** Dua kukubaliwa inategemea na muombaji kuwa ni Muislamu, kufanya tawba kwa makosa aliyoyafanya na kuomba dua kwa kujua maana yake na imani. Dua inayoombwa na moyo wenye giza basi dua hiyo haikubaliwi na Allahu taala. Moyo wa mtu anayeomba dua mara tatu kila siku na kutekeleza namazi (sala) mara tano basi mojo wake hutakasika nao ukaanza kutamka. Dua inayoombwa kwa mdomo tu bila ya moyo nao kutamka basi dua hiyo haitakuwa na faida.

Mafundisho ya kidini yaliyofundishwa na dini ya kiislamu ni yale ambayo yaliandikwa kwenye vitabu vya maulamaa wa **Ahl as-Sunna**. Miomgoni mwa mafundisho yaliyofundishwa na maulamaa wa Ahl as-Sunna kuhusu Iman na Uislamu, zipo ayatul karim (aya za Quran tukufu) na hadithi as-sharifu (hadithi tukufu) ambazo maana yake yanafahamika moja kwa moja na yako wazi, na huitwa **nass**, basi yule asieziamini hizo anakuwa **Kafiri.** Pindi akificha kutoamini kwake mafundisho hayo basi anaitwa **Munafik**. Na yule anayeficha kutoamini kwake na akajifanya kuwa Muislamu ili kuwapoteza Waislamu, huyu anaitwa **Zindiq**. Hata hivyo katika (nass) aya ambazo maana zake sio za moja kwa moja mtu wakati wa kuzichambuwa na kutafakari akifahamu vibaya na kuamini vivyo basi huyu hawi Kafir. Lakini kupotoka kwenye njia sahihi ya Ahl as-Sunna itamsababisha kwenda moto wa jahannam. Lakini kwa-kuwa aliamini zile nass ambazo maana yake iko wazi na inafahamika moja kwa moja hatokaa ndani ya jahannam milele, ataokolewa kutoka kwenye moto na kupelekwa kwenye Janna. Watu wa aina hii huitwa **watu wenye bid’at au firkat dalalat** (makundi yaliopotea). Kuna makundi sabini na mbili (72) yaliyopotea. Hawa na makafiri, murtadi wote Ibada zao, wema na msaada wao kwa watu havitokubaliwa na Allahu taala na havitowasaidia siku ya kiama. Waislamu wenye Iman wanaitwa **Ahl as-Sunna wal-jamaat au Waislamu wenye itiqadi ya ki-sunni**. Waislamu wa ki-sunni jinsi ya kutekeleza ibada yao wamegawanyika katika makundi

(madhehebu) manne (4).[1] Watu hawa wanajulikana kuwa Waislamu wa Ahl as-Sunna, wanasalimiana, wanapendana na wanasaidiana. Mtu ambaye hayumo katika makundi manne haya hawezi kuwa Muislamu mwenye itikadi ya ki-sunni. Mtu huyu ambaye sio katika Ahl as-Sunna anatambulikana kama ni kafiri au mtu mzushi kwa mujibu wa Imam Rabbani katika barua zake alizoandika, hasa kwenye juzuu ya kwanza barua ya mia mbili themanini na sita (286) **(Maktubat)** vile vile katika vidokezo vya **Tahtawi** kwenye kitabu **Durr ul-Mukhtar**, somo lake la **Zebayikh**, na katika kitabu **al-Besair li-munkir-it-tawassul-i-bi-ahl-il-maqabir**, aliandika kwa kutoa ushahidi. Vitabu vyote viwili ni vya kiarabu. Hikichabili kiliandikwa na kuchapishwa India mnamo mwaka 1395 (1975 A.D). Na baadae Hakikat Kitabevi walioko Istanbul, Uturuki, kwa njia ya offset walitoa tena kitabu hicho na kukichapisha.

Wanaotekeleza ibada zao Kulingana na moja katika madhehebu haya manne, wanapofanya dhambi au wakafanya makosa ya aina yoyote kwenye ibada zao, halafu wakafanya tawba (wakamuomba Allah msamaha) basi Allahu taala akitaka atawasamehe na hatowaadhibu na moto wa jahannam. Na Akitaka pia kuwaadhibu kutokana na madhambi yao atawaadhibu halafu atawaokoa na kuwatoa kwenye adhabu.

Kwa wale ambao hawakuamini hata kwa mambo yale yaliokuwa wazi na lazima kuaminiwa katika Uislamu, kwa mfano yale yanayofahamika hata na wajinga, basi hao wanaitwa **makafiri** na **murtadi** na watakaa kwenye jahannam milele. Kuna aina mbili za makafiri: makafiri wenye kitabu (Ahl-il-kitabu) na makafiri wasiokua na kitabu. Mtoto akizaliwa na wazazi Waislamu halafu baadae akatoka kwenye Uislamu, huyu anaitwa **“murtadi”**. Ibn Abidin "rahmatullahi alaih" alipokuwa anaelezea sababu za shirk na ndoa haram alisema kwamba, “Murtadi, Muldidu, Zindiq, majusi (wanaoabudu moto), wenye kuabudu viumbe (sanam), wanafalsafa wa zamani wa Ugiriki, wanafiki, kwenye makundi sabini na mbili (72) ambao walipindukia (wabarahima, wafuasi wa budha),

[1] Makundi manne (madhehebu) ni 1.Madhehebu ya Hanafi, 2.Madhehebu ya Shafi, 3. Madhehebu ya Malik, 4. Madhehebu ya Hanbali.

wabatin, maibaha, na maduruzi wote ni makafiri wasiokuwa na kitabu. Makomunisit, ma freemason nao ni mfano wa makafiri bila kitabu. Wakristu na wayahudi ambao wana vitabu kama **Tawrat** na **Bibilia** vilivyoteremshwa kutoka mbiguni baadae wakavifanyia marekebisho na kuwiharibu ni makafiri wenye kitabu. Mtu kama huyu akiabudu kiumbe au viumbe kwa kuvipa sifa za kiungu basi atakua **mushrik**. Sifa zake Allahu taala **(Sifaat adh-Dhaatiyya)** pamoja na **(Sifaat ath-Thubuutiyya)** zake huitwa **(Sifaat Uluhiyya)** yani sifa za Kiungu.

Watu wenye kitabu na wale wasiokua na kitabu wote ni makafiri, lakini wakiukubali na wakaingia kwenye Uislamu wanakua wameokolewa kuingia moto wa jahannam. Wanakua Waislamu safi bila dhambi yoyote lakini ni lazima wawe Waislamu wa Sunni (Ahl as-Sunna). Wakisilimu halafu wakajiunga na makundi mengine kama mashia, ahmadia na kadhalika basi wanakua hawajaokolewa na wataadhibiwa. Kuwa Sunni maana yake ni: kusoma na kujielimisha kupitia vitabu vilivyoandikwa na mmoja wa maulamaa wa Ahl as-Sunna na kufuata yalioandikwa kwenye vitabu hivyo. Katika dunia mtu anafahamika kama ni Muislamu au sio Muislamu kutokana na matamshi yake pale anaposema bila kulazimishwa. Mtu huyu akiondoka duniani kuelekea akhera basi kutokana na pumzi za mwisho anajulikana kwamba ameondoka na iman au hapana. Muislamu mwenye madhambi chungu nzima akifanya tawba kwa madhambi hayo, atapata msamaha kutoka kwa Allahu taala na atakuwa Muislamu safi bila dhambi. Kuhusu tawba maana yake na inafanywa vipi yamelezewa zaidi katika vitabu ilm al-hal', kwa mfano cha kiarabu **Iman wal-Islam (Iman na Uislamu)** na cha kituruki **Se'adet-i ebediyye (Furaha isioisha)**.

## IMAN NA UISLAMU

Katika kitabu hiki, **Itiqad-nama**, hadithi as-sharifu ya mtume "swallallahu alaihi wa sallam" inayohusiana na Iman na Uislamu itafafanuliwa. Na matumaini kwamba, kwa njia ya baraka za hadithi as-sharifu (hadithi tukufu) hii, iman ya Waislamu itakamilishwa, na baadae watapata uokovu na furaha. Na ninatumai tena itanifanya

mimi Khalidi, ambaye madhambi yake ni mengi, kuokolewa (kasema vile sio eti ni mfanya maovu lakini kwakua binadamu hajakamilika katika utendaji wake wa ibada na unaweza ukajihisabu katika wema wakati humo kutokana na mambo tofauti unayoyafanya kimakusudi na kimakosa yani bila kujua). Namuomba Allahu taala ambaye nina iman kubwa na yeye kwamba hataki chochote kutoka kwa mja, na baraka na neema zake ni nyingi mno, na anawaonea huruma sana waja wake, kumsamehe Khalid ambaye ni maskini ambaye ni kiachache alichokichuma na moyo wake una giza, kutokana na maneno yake yasiofaa, kukubali ibada zake zenye kasoro. Tunamuomba Allah atulinde dhidi ya maovu ya udanganyifu na uongo wa shetani (na pia dhidi ya kudanganywa na uongo, maneno na maandishi yenye makosa yanayoletwa na maadui wa Uislamu) na atupe furaha, kwani yeye ndio mwenye rehma zaidi.

Wanazuoni wa Kiislam wanasema kila **Mukallaf** (mtu aliefikisha umri wa kujiamulia) awe mume au mke ambaye ni Uislamu, aliefikisha umri wa kubaleghe na kufanya uamuzi, anapaswa kujua na kuamini Sifaat adh-Dhaatiyya[1] na Sifaat ath-Thubuutiyya za Allahu taala kwa usahihi. Fardhi ya msingi kwa kila mtu ndio hii.

Kutojua sio udhuru, ni kosa. Khalidi ibn Ahmad al-Baghdadi aliandika kitabu hiki sio kuonyesha ushujaa wake na elimu yake kwa wengine au kuingia kwenye daftari la watu maarufu lakini lengo lake ni kuacha kumbusho ambalo litakua huduma kwa watu baada yake. Allahu taala amsaidie Khalid[2] mwenye upole na Waislamu wengine kupitia nguvu na rehma zake ameen.

---

[1] Allahu taala ana sifa sita zinazoitwa **Sifaat adh-Dhaatiyya: al-wujud** (kuwepo), **al-Qidam** (kutokua na mwanzo), **al-Baqaa** (kutokua na mwisho na kuendelea kuwepo milele), **al-wahdaaniyya** (kutokua na mshirika), **al-mukhaalafatu li-l-hawaadith** (kuwa tofauti na viumbe wote kwa namna yoyote), **al-Qiyaamu-bi-nafsihi** (kutotegemea kitu katika kuwepo kwake). Hakuna kiumbe mwenye sifa kama yeye sifa sita hizi, wala mwenye uhusiano na moja kati ya sifa hizi. Ni za Allahu taala pekee. Baadhi ya wanzuoni walisema kwamba al-Mukhallafatu li-l-hawaadith na al-Wahdaaniyya zilikuwa pamoja na idadi ya Sifaat adh-Dhaatiyya ni tano.

[2] Khalidi Baghdad alifariki mnamo mwaka wa 1247 (1826 A.D) kwenye mji wa Damascus.

Kila kitu zaidi ya Allahu taala kinaitwa **ma-siwaa** au a'lam (uumbaji, Ulimwengu), kinachoitwa kwa sasa **(maumbile)**. Viumbe vyote havikuwepo. Allahu taala ndiye alieviumba vyote. Viumbe vyote ni **mum-kin** (kitu kinachoweza kutokea hali yakuwa hakikuwepo mwanzo) na **hadithi** (ni kitu kinachotokea baada ya kutokuepo); yaani, vinaweza kutokea haliyakuwa havikuwepo na vilevile vinatokea baada ya kutokuepo. Hadithi as-sharifu inaonesha ukweli kwamba **Allahu taala alikuepo, kipindi ambacho hakukua na kitu.**

Ushahidi wa pili unaonesha kwamba ulimwengu wote na viumbe waliomo wote ni hadithi. Ni ukweli kwamba viumbe wote wanaendelea kubalilika kutoka kwenye sura moja kwenda nyengine muda wote; kwa kweli, kitu kilicho qadiim (kutokua na mwanzo) hakitobadilika kamwe.

Sifa za Allahu taala ni qadiim (hazina mwanzo) na hazijawahi kubadilika.[1] Mabadiliko kama hayo ndani ya viumbe hayawezi yakatokea kwenye kitu cha milele. Ni lazima yawe na mwanzo na vile vile kutengenezeka kutokana na vipengele au dutu, ambavyo vimeumbwa kutokana na kutokuepo.

Ushahidi mwengine kuhakikisha kwamba ulimwengu ni mumkin, ni kwamba unaweza kuwepo kutokana na kutokuwepo mwanzo, kwa hivyo viumbe kama tunavyoona ni hadithi, yaani vinatokea wakati wakutokuwepo.

Kuna aina mbili za viumbe: **mumkin** na **wajib**.[2] Ingekuepo mumkin tu peke yake, au wajib al-wujud isingekuepo, kila kitu

---

[1] Hata hivyo, katika ulimwengu hali ya vitu inabadilika kwenye tukio ya kimwili. Katika mmenyuko kemikali, mfumo wa dutu huwa namabadiliko. Tunaona molekuli hutokea na baadae hubadilika kwenda sura nyingine. Leo kwenye mabadiliko ya atomiki na mmenyuko ya nyuklia, ambavyo vimevumbuliwa hivi karibuni, hutoweka na kubadilika kwenda hali ya nishati.

[2] Wujud maana yake ni **'kuwepo'**. Na kuna aina tatu za kuwepo. **Ya kwanza ni wajib al-wujud**, ni lazima awepo. Na daima yupo. Amekuepo tokea zamani na hakutokana na kitu chochote, na hatosita kuendelea kuepo. Allahu taala peke yake ndio wajib al-wujud. Ya pili ni mumtani al-wujud, kitu ambacho kamwe hakiwezi kutokea. Na hakijaweza kutokea. Kwa mfano shariik al-barii (msaidizi wa Allah) ni kitu kisichowezekana. Mungu zaidi ya Allah au anayemfanana hawezi kutokea. Na ya tatu ni

kisingeweza kuepo.[1] Kwa sababu hii, mumkin haikuweza kutokea au kwenda katika hali ya kutokea yenyewe. Kama haikuathiriwa na nguvu fulani, basi ingebaki katika hali ya kutokuepo na isingeweza kutokea. Kwakua mumkin haiwezi kujiumba yenyewe, isingeweza na haiwezi kimaumbile kuumba mumkin nyingine. Aliyeumba mumkin yote ni lazima awe wajib al-wujud. Kuepo kwa ulimwengu ni ishara kubwa kwamba kuna muumbaji aliyeuumba wakati haukuepo. Sasa muumbaji wa kipekee aliyeweza kuumba mumkin yote, viumbe wote ni wajib al-wujud tu bila ya kuwa hadithi wala mumkin, lakini mda wote alikuepo na ni qadiim (hana mwanzo). 'Wajib al-wujud' maana yake ni kuepo kwake hakujatoka kwenye kitu chengine bali kitu chenyewe. Hii inashiria kwamba wajib al-wujud mda wote tokea mwanzo ipo na haikuumbwa na kitu chengine. Kama si hivyo basi nacho itakuwa ni kiumbe (mumkin na hadithi) kilichoumbwa na muumbaji mwengine. Na haya yanapingana na yaliothibitishwa juu. Katika lugha ya kiajemi neno **'Khudaa'** (hutumika kama jina la Allah) linalomaanisha 'aliopo mwenyewe milele. Tunaona kwamba tabaka la viumbe liko kwenye mpangilio wa kushangaza, na wanasayansi kila mwaka wanakuja (wanavumbua) sheria mpya zinazoendana na mpangilio huo. Muumbaji wa mpangilio huo ni lazima awe **Hayy** (mda wote yupo hai), **Aliim** (mjuaji wa kila kitu), **Qaadir** (mwenye uwezo), **Muriid** (mwenye kutaka), **Samii** (mwenye kusikia kila kitu), **Baswiir** (mwenye kuona kila kitu), **Mutakallim** (mwenye kusema) na **Khaaliq** (mwenye kuumba).[2] Kwa sifa kama kifo, ujinga, kutoweza au kuondolewa na wengine, kulazimishwa, uziwi, upofu na ububu zote ni sifa zenye kasoro na hazijakamilika. Kwa hivyo basi sifa zenye kasoro kama hizo haziwezi kuwa za Mungu aliyeumba

---

mumkin al-wujud, ni kitu kinachoweza au kutoweza kutokea. Mfano, ulimwengu, viumbe wote bila istisna. Wujud Kinyume chake ni **Adamu** (kutokuepo). Viumbe wote vilikuwa katika hali ya 'adamu'(yani havikuepo) mwanzo lakini vilikuja kutokea tu.

[1] Haya ni mabadiliko, tukio kutokea kuepo kutototokana na kitu chochote, na katika elimu yetu ya fizikia, ili mabadiliko yaweze kutokea kwenye dutu, dutu hiyo itabidi ibadilike.

[2] Hizi ndio sifa nane za Allahu taala zinazoitwa Sifaat ath-Thubuutiyya.

ulimwengu na viumbe wote kwenye mpangilio mzuri na analinda viumbe wote dhidi ya kuangamia.[1]

Zaidi ya hayo, sifa za ukamilifu tulizozitaja juu tunaona pia kwenye viumbe alivyoumba. Sifa hizo ameziumba akaziweka tena kwenye viumbe wake. Kama sifa hizi hazipatikani kwake yani ingekuwa hana sifa hizo, angewezaje tena kuziumba na kuziweka kwenye viumbe wake wakawa ndio wanaomiliki sifa hizo! Laa sivyo viumbe wake wangegeuka kuwa wa juu kuliko yeye. Na tunafaa kuongeza kwamba muumbaji wa vyote vilivyomo kwenye ulimwengu anapaswa kuwa mwenye sifa zenye ukamilifu kama hizo na lazima awe mwenye ukuu kuliko kitu chochote na hana sifa yoyote yenye upungufu, kwa sababu mtu ambaye ana upungufu hawezi kuwa mbunifu kiasi hicho.

Mbali na ushahidi wa kiakili huu, Aayatul karima (aya tukufu za Quran) na hadithi sharif (hadithi za mtume) zinafafanua vizuri kwamba Allahu taala ana sifa zenye ukamilifu zisizokua na kasoro hata kidogo. Kwa hiyo, hairuhusiwi kuwa na shaka yoyote juu ya hilo. Na shaka juu ya sifa za Allahu taala husababisha mtu kuwa kafiri. Sifa nane za ukamilifu zilizotajwa hapo awali zinaitwa **Sifaat ath-Thubuutiyya**. Allahu taala ni mwenye sifa nane hizo zenye ukamilifu. Hakuna kasoro, mchanganyiko wala mabadiliko kwenye

[1] Her kiumbe kuanzia atomi hadi nyota, vimeumbwa kutokana na mahesabu na kanuni maalumu. Utaratibu wa ndani ya kanuni zinazojulikana za fizikia, kimia, astronomy (falaki) na biolojia huchanganya akili za binadamu. Hata Darwin alilazimika kusema kwamba anapofikiria kwenye utaratibu na unyeti wa jicho, anahisi kama anaingia wazimu. Hewa ni mchanganyiko wa naitrojeni (78%), oxygen (21%) na noble gas ambayo ni (1%). Hewa sio kitu kimoja bali ni mchanganyiko. Basi oksijeni ingezidi kipimo cha 21% ingeweza kuyachoma mapafu yetu. Na ingekuwa chini ya 21% isingeweza kuchoma rutuba za damu. Na isingewezekana kwa binadamu na wanyama kuishi. Kipimo hiki hakibadiliki kutoka kwenye sehemu kwenda nyingine hata mvua ikinyesha. Na hii ni neema kubwa. Sasa basi neema hii haionyeshi upatikanaji wa Allah, uwezo wake na rehma zake juu ya viumbe hai? Muundo wa jicho sio kitu ukilinganisha na makubwa haya. Je inawezekana kwa muumbaji wa kanuni zote zinazoendesha na kufundishia maisha ya kisayansi na mahisabu nyeti awe mwenye kasoro?

dhati, sifa wala vitendo vyake. **Sifaat ath-Thubuutiyya** na **Sifaat adh-Dhaatiyya** zinaitwa **Sifaat** za **Uluhiyya** (sifa za kiungu). Mtu akiamini kwamba kuna kiumbe ambacho kinamiliki sifa za kiungu, basi mtu huyu anakuwa **Mushrik**.

## NGUZO ZA UISLAMU

Kwa usaidizi na nguvu zinazotolewa na Allahu Taala (Mwenyezi Mungu) mwenye kulinda ulimwengu na vilivyomo vyote, na ndiye anayetoa neema zote na zawadi na ndie asiyelala, sasa tunaanza kufafanua maneno ya mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam".

Kipenzi chetu Hadhrat Umar ibn al-Khattab "radiyallahu anhu" na ambae alikuwa kiongozi shujaa wa Uislam, na mwenye cheo cha juu miongoni mwa masahaba zake mtume "swallallahu alaihi wa sallam", na alikuwa maarufu kwa ukweli wake anaeleza kwamba:

Ilikuwa ni siku ambayo baadhi yetu (masahaba) tulikuepo mbele ya mtume "swallallahu alaihi wa sallam". Siku hiyo na muda huo ulikuwa wenye baraka, siku yenye thamani kadir kwamba kila mtu angependa kuishi katika siku hiyo mara kwa mara akipata fursa tena. Katika siku hiyo, sote tulijaa furaha na heshima ya kukusanyika pamoja masahaba wa mtume na kukaa karibu nae na tukaona uso wake na maneno yake mazuri ambayo yalikuwa ni chakula cha roho na kutuliza nyoyo. Kusisitiza thamani, heshima ya siku hiyo, Masahaba waliobarikiwa wanasema: ”ilikuwa ni siku.... ni siku ambayo haikadiriki kwasababu ni siku ambayo Jibril "alaihis-salaam" alijitokeza mbele ya binadamu na sote tukamuona, tukapata kusikia sauti yake na kusikia elimu nzuri mtu anayopenda kujisikilizia mwenyewe kwa makini kupitia mdomo wa Rasulullah "swallallahu alaihi wa sallam"“.

Katika muda huo, mwanaume alikuja karibu nasi kana kwamba mwezi kamili unajitokeza. Nguo zake zilikua nyeupe kabisa na nywele zake zilikuwa nyeusi. Hakuwa na alama yoyote ya safari kama vumbi mwilini kwake, na hakuna yoyote aliekuwa anamtambua miongoni mwetu (yani masahaba za mtume "swallallahu alaihi wa sallam") kwa mfano hakuwa mtu ambaye

tuliwahi kumuona kabla ya hapo au kumjua. Alikaa chini mbele ya mtume "swallallahu alaihi wa sallam", na akaweka magoti yake karibu na magoti ya mtume "swallallahu alaihi wa sallam". Mtu huyu pamoja na kujitokeza katika sura ya binadamu lakini alikuwa malaika Jibril. Pamoja na kwamba muundo wa kukaa kwake haukuendana na adabu, lakini ilituonyesha ukweli kwamba wakati tunajifunza elimu ya dini, aibu au haya havina nafasi, na wala kiburi au jeuri kupewa fursa ya kuongoza. Jibril "alaihis-salaam" alitaka kuwaonesha maswahaba kwamba kila mtu anaweza kuuliza suala lolote analotaka kufahamu kuhusu dini ya Uislam bila yakupata aibu/haya, kwahivyo hakuna kuona aibu wakati tunajifunza Uislam au kudhalilisha katika utendaji, mafundisho au mtu kujielimisha wajibu wake mbele ya Allahu taala.

Mtu mtukufu huyu, akaweka mikono yake kwenye magoti ya mtume "swallallahu alaihi wa sallam". Akamuuliza mtume: **‘ewe mtume wa Allah! Ebu niambie maana ya Uislam na vipi unaweza kuwa Muislam.’**

**Uislam** maana yake ni ‘kujisalimisha’. Mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alifafanua kwamba neno Uislam ni mkusanyiko wa nguzo tano za Uislam kama ifuatavyo:

1– Mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alisema kwamba nguzo ya kwanza katika nguzo tano za Uislam ni **“kutamka kalimat ash-shahada (kutamka neno la shahada)”**, na neno hili ni mtu lazima aseme, **“Ash’hadu an la ilaha illallah wa ash’hadu anna Muhammadan abduhu wa rasuluh.”** Kwa maneno mengine, mtu mwenye upambanuzi ambaye amebaleghe na anayeweza kuongea anafaa kusema kwa mdomo wake, **“ardhini na mbiguni, hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Allahu taala. Allahu taala pekee ndie anayefaa kuabudiwa**. Yeye ndie wajib al-wujud. Ukuu wa aina yoyote unapatikana kwake. Hana kasoro ya aina yoyote ndani yake. Na jina lake ni **Allah**,” na kuamini ukweli huu kwa nyoyo zao. Na pia mtu anafaa kusema na kuamini: “Mtu mtukufu zaidi aliyekuwa mwenye ngozi ya waridi, mweupe-mwekundu, mwenye kung’aa na mwenye uso wenye kupendeza, mwenye macho na nyusi nyeusi, mwenye paji la uso pana, mwenye tabia na mwenendo mzuri, na kivuli chake hakikuanguka chini hata siku moja, alikuwa mwenye sauti laini na alikuwa anaitwa Muarabu kwa

sababu alizaliwa Makka kwenye kizazi cha banu Hashim na akapewa jina **Muhammad ibn Abdullah, ni mtumwa (abd) wa Allahu taala na vile vile mtume (Rasul)**. Mama yake mtume alikuwa akiitwa Amina bint Wahb. Alizaliwa kwenye mji wa Makka (alfajir ya jumatatu, 20th mwezi wa nne mwaka 571 A.D). Mwaka wa 611 alipotimiza miaka arubaini (40) alijulishwa kwamba yeye ni mtume (nabii) na mwaka huu unaitwa sanatul bi'itha (mwaka wa utume/unabii). Na baada ya tukio hilo alianza kufanya da'awa ya kuwaita watu wa Makka kwenye dini ya Uislam kwa muda wa miaka kumi na mitatu (13). Halafu baadae kwa amri ya Allahu taala alihamia mji wa Madina. Huko akausambaza Uislam kila sehemu. Miaka kumi (10) baada ya Hijrat (kuhama) siku ya jumatatu 12, Rabi´al-Awwal (July,632)[1] alifariki dunia na kuelekea kwa rafiki yake wa juu.

2– Nguzo ya pili katika nguzo tano za Uislamu ni kusali sala (namaz) tano kila siku, pamoja na kutimiza masharti ya msingi wakati muda wa kila sala unapokaribia. Ni farz (wajibu) kwa kila

---

[1] Kulingana na wana historia, mtume aliingia pangoni kwenye mlima wa Sawr jioni mwa Alhamisi, 27 Safar, mwaka wa 622 A.D (milad), wakati alipokuwa anahama kutoka Makka al-Mukarramah kwenda Madina al-Munawara. Aliondoka tena kwenye pango siku ya jumatatu usiku na akaigia Quba kijiji kilicho karibu na mji wa Madina, kwenye siku ya jumatatu 8 Rabi'al-Awwal sawa na (20 mwezi wa Septemba kwenye kalenda ya gregori na sawa na 7 mwezi wa Septemba ukilinganisha na kalenda ya juliyan. Siku hii yenye furaha ndio chanzo cha kalenda ya Waislamu inayoitwa Hijriyyah-shemsı (solar) calendar. Mwanzo wa Kalenda ya hijri ambayo inafuatwa na mashia imeanza miezi sita (6) kabla ya hii. Na sherehe za Nawruz zinazofanywa na Majusi (wanao abudu moto) inaanza mwezi mach 20. Kwenye siku ya Alhamisi, wakati sehemu zote za ulimwengu zinakua kwenye hali ya usawa kati ya mchana na usiku kwa urefu, alikaa Quba na akaondoka siku ya Ijumaa, kuingia mji wa Madina siku hiyo hiyo. Na kuanzishwa kwa mwezi wa Muharram kwenye mwaka huo (Ijumaa 16 juni) ilikubaliwa kuwa mwanzo wa kalenda ya Hijri Qamarı. Siku mpya ya mwaka huo wa Qamarı ilikuwa 16 july, Ijumaa. Mwaka wa Hijri shemsi unaolingana na siku ya kwanza kwa mujibu wa miaka ya kimagaribi ni mwaka wa 622.

Muislamu kutekeleza ibada hii ya sala mara tano kila siku, pamoja na kusali kila sala katika wakati wake uliowekwa, sio mapema sana wala sio kuchelewa na kujua kwamba mda ndio huo.[1] Ni dhambi kubwa kusali sala kabla ya wakati wake. Na makosa haya mara nyingi husababishwa na kutumia kalenda mbovu zilizoandaliwa na wajinga na wale akina La-madhhabi (wasio na madhehebu). Sala (namaz) hiyo inayosaliwa kabla wakati wake kuingia au baada ya wakati kumalizika sio sahihi. La-madhhabi ni watu ambao hawajafungamana na moja katika madhehebu manne. Kutokana na upotofu huu, wanawasababisha Waislamu kusali sunna adhuhuri na alasiri kwenye muda ambao ni karaha (kerahat) kusali.

Muda wa karaha kusali umeelezewa katika kitabu **Endless Bliss** (neema bila kikomo) juzuu ya nne, na pia kwenye gamba la kitabu **Miftah-ul-Janna**. Sala (namaz) inafaa kusaliwa kwa kutia nia na kuzingatia faradhi zake, wajibu, vile vile sunna zake, na kusalimisha moyo mbele ya Allahu taala kabla muda wake haujamalizika. Katika Quran tukufu namaz huitwa ‘sala’. Sala maana yake ni kitendo cha binadamu kuomba, na Malaika kuomba istighfar, na Allahu taala kupata huruma juu ya waja wake. Katika Uislam Salat maana yake ni kutenda vitendo fulani, na kusoma vitu fulani kama vinavyooneshwa kwenye vitabu vya İlm al-hal. Sala inaanza na maneno **‘Allahu akbar,’** na hii inaitwa **‘takbir al-iftitah,’** na husemwa baada ya kuinua mikono hadi kwenye masikio na humalizika baada ya kufunga mikono chini ya kitovu (kwa wanaume). Sala pia inamalizika na salam, inayofanywa kwa kugeuza kichwa kwa upande wa kulia na kushoto baada ya sujudi ya mwisho.

3– Nguzo mahitaji yake na imefikia idadi fulani inayoitwa **nisab** kwa kuitenganisha na mali yake halafu kuitoa kwa waisilam waliotajwa ndani ya Quran tukufu. Zaka inapewa aina ya watu saba. Kuna aina nne za zaka katika madhehebu yote manne. Zaka kwenye dhahabu na fedha, zaka ya Uislam ya tatu ni **“kutoa zakat.”** Neno zakat kimsamiati ni ‘usafi’, kusifu, kuwa mzuri na mwema. Katika

---

[1] Soma juzuu ya nne kitabu Endless Bliss kwa maelezo zaidi kuhusu namaz (sala). Pia angalia kwenye kitabu miftah-ul-janna. Toleo lake la kingereza lipo katika Hakıkat kitabevi, İstanbul, Uturuki.

Uislam **zakat** maana yake ni mtu mwenye miliki za zakat ambazo ni ziada ya kwenye bidhaa za biashara, zaka kwenye mifugo (kondo, mbuzi, ng´ombe) inayofugwa kwenye mashamba kwa muda wa zaidi ya nusu mwaka, na zaka ya vitu vyote muhimu vinavyotolewa (kulimwa) kwenye ardhi. Aina hii ya nne ya zakat inaitwa **'ushr** na inatolewa mara tu baada ya mavuno. Zile aina tatu za zaka hulipwa mwaka mmoja baada ya kutimiza kiwango kinachoitwa nisab.

4– Nguzo ya nne ya Uislam ni **"kufunga mwezi wa Ramadhani".** Na kitendo cha kufunga kinaitwa 'sawm.' Sawm maana yake ni kulinda kitu dhidi ya kitu kingine. Katika Uislam, sawm maana yake ni kujizuia/kujilinda dhidi ya vitu vitatu wakati wa mchana ndani ya mwezi wa Ramadhani kama alivyo amrisha Allahu taala. Na vitu vitatu hivyo ni: kula, kunywa na kufanya kitendo cha ndoa. Mwezi wa Ramadhani unaanza pale mwezi unapoonekana. Mwezi huu wa Ramadhani hauwezi kuanza kwa kutumia mahisabu ya kalenda.

5– Nguzo ya tano ni **"kwa mtu mwenye uwezo (mali) kufanya hija mara moja maishani mwake."** Kwa mtu mwenye uwezo (mali) kwenda Maka na kurudi bila ya watu wake waliobaki nyumbani kuhangaika na kupata matatizo kimali, basi kwa mtu kama huyu ni wajibu kutekeleza nguzo hii na ni wajibu kufanya tawaf (kuzunguka Ka'ba) na kufanya waqfa kwenye kiwanja cha Arafa, pindipo afya yake ni nzuri mara moja katika maisha yake.

"Baada ya kusikia majibu haya kutoka kwa Rasulullah (mtume wa Mungu) "swallallahu alaihi wa sallam", mtu huyu alisema, **'Ya Rasulullah! (mtume wa Mungu) umesema ukweli'.** Sahaba Umar Mungu awe radhi nae anasema kwamba maswahaba wote waliokuepo wakati huo walishangazwa na tabia za mtu huyu ambaye aliuliza suali halafu baadae anasadikisha kwamba majibu ni sahihi. Mtu anauliza kwa nia ya kujua lakini kusema, "umesema ukweli," inaonyesha kwamba muulizaji alikuwa tayari anajua jibu la suali alilouliza. Nguzo kuu miongoni mwa hizo zilizotajwa hapo juu ni kalimat ash-shahada na kuamini maana yake. Na inayofuata ni kusali sala (namaz). Hii inafuatwa na funga (sawm). Halafu inakuja hija. Na ya mwisho ni kutoa zaka. Inakubaliwa kwamba kalimat ash-shahada ni nguzo ya juu kabisa. Kuhusu mpangilio wa nguzo zile nne, wanazuoni wa kiislamu wanasema kama tulivyosema hapo juu. Kalimat ash-shahada ndio iliofaradhishwa kwanza, mwanzoni mwa Uislam. Namaz (sala) tano za kila siku zilikuja kuwa faradhi

kwenye siku ya Miraj usiku katika mwaka wa kumi na mbili wa Bi'that (mwaka wa utume), mwaka mmoja na miezi kadhaa kabla Hijri (kuhama). Kufunga mwezi wa Ramadhani kulifaradhishwa kwenye mwezi wa Shaaban, mwaka wa pili baada ya kuhama (hijri). Kutoa zaka kulifaradhishwa kwenye mwezi wa Ramadhani ndani ya mwaka huo huo ambao funga (sawm) ilifanywa fardhi. Na hija kwenye mwaka wa tisa baada ya hijri[1] kuhama) ilifaradhishwa.

Mtu akikataa, akikufuru, akikanusha, akifanya mzaha/masihara kwenye moja ya nguzo za Uislam, basi anakuwa kafiri, tunamuomba Allah atuepushe! Vile vile, yule asiekubali kitu chochote ambacho kilikubaliwa na kuwekwa wazi kwamba ni halali au haramu au anayehalalisha vilivyowekwa haramu na kuharamisha vilivyo halali, basi na yeye anageuka kuwa kafiri. Mtu akikanusha au akichukia moja ya mafunzo yanayojulikana kuwa ya kiislam kwa mfano, mafunzo yanayofundishwa na yanayojulikana na kila mtu hadi watu wa kawaida wanaoishi ndani ya nchi za Waislamu, basi anakuwa kafiri.[2] Mtu wa kawaida anapokuwa hajui

---

[1] Maelezo zaidi kuhusu namaz (salat), funga (sawm), zakat, hija na kuhusu Miraj yanapatikana kwenye kitabu Endless Bliss (furaha bila kikomo) juzuu ya nne. Bi'that maana yake ni kipindi ambacho Allahu taala alimtuma malaika wake Jibril kwenda kumuambia mtume wake kwamba yeye ni mtume wa mwisho. Hijri maana yake ni kuhama kwa Rasulullah "swallallahu alaihi wa sallam" kutoka Makka kwenda Madina.

[2] Kwa mfano, kula nyama ya nguruwe, kulewa au kutumia vinywaji vyenye pombe, kamari, mwanamke au binti kujionyesha mbele ya watu wakati hajafunika kichwa, nywele, mikono pamoja na miguu yake na mwanamme pia kujionyesha mbele ya wengine wakati hajasitiri viungo vyake kati ya magoti na kitovu vyote hivyo ni haramu. Hivi ni vitendo ambavyo Allahu taala ameviharamisha. Katika Madhehebu manne ambayo yanaelezea maamrisho na makatazo ya Allahu taala, wana mitazamo tofauti kuhusu mwanzo na mwisho wa utupu (awrat) wa mwili wa mwanaume, kwa mfano sehemu ya mwili wa mwanaume ambayo ni haram kuonyesha wengine na ni haram pia kwao kuangalia kwenye sehemu hizo. Ni lazima kwa kila Muislam kufunika/kuficha sehemu hizo kulingana na madhehebu anayofata. Na ni haramu pia kwa wengine kuangalia wale ambao hawajafunika sehemu zao hizi. Imeandikwa kwenye Kimya-a-yi Saadet kwamba ni haram kwa wanawake au wasichana kwenda nje bila kufunika vichwa vyao, nywele zao, mikono

yao, miguu yao na pia ni haram kwao kwenda nje wakati wamevaa nguo nyembamba, zenye kupambwa, zenye kuwabana na ambazo zimejazwa manukato. Mama zao, baba zao, waume na ndugu zao ambao wanawaruhusu kwenda nje kama vile na wakidhani kwamba inafaa na wakiwaunga mkono watagawana kwenye madhambi yao na pia adhabu watakazozipata, hii ni kwamba watachomwa wote motoni. Na wakitubu, watasamehewa na hawatochomwa. Allahu taala anapenda waja wanaotubu. Katika mwaka wa tatu wa hijri, wanawake na wasichana wenye akili na waliokuwa wamebaleghe waliamrishwa kutojionesha kwenye wanaume wageni. Lakini majasusi wakiingereza na wajinga ambao walianguka kwenye mitego yao wanadanganya watu kwamba kabla aya ya hijabu haijashuka wanawake wake walikuwa hawajistiri na kujifunika walidanganywa tu na wanazuoni wa fik'hi. Mtu anaposema kwamba ni Muislamu, mambo atakayoyafanya ni lazima kwake kujuwa kwamba yanaruhusiwa na Uislam au hayaruhusiwi. Asipojuwa basi anafaa kuuliza mmoja wa wanazuoni wa Ahl as-Sunna au kutafuta moja ya vitabu vilivyoandikwa na wanazuoni wa Ahl as-Sunna akasoma na kujifunza ni lazima kwake. Anayoyatenda yakiwa hayafai katika Uislam basi hatoepuka madhambi wala kukufuru. Kila siku ni lazima kwake kufanya toba ya kweli. Madhambi na mambo ya kikafiri yanayotubiwa yanasamehewa. Mfanya maovu asipotubu atazipata adhabu za hapa duniani na jahannam. Adhabu hizi zimeandikwa kwenye sehemu tofauti katika kitabu chetu. Waislamu wenye kufanya madhambi makubwa baada ya kuchomwa kulingana na makosa yao watatolewa kwenye moto wa jahannam. Wale ambao hawakumuamini Allahu taala na wanafanya juhudi za kuuondoa Uislam kama makafiri na zindiki, hawa watadumu milele ndani ya jahannam.

Sehemu zinazofaa kufunikwa kwa wanaume na wanawake wanapokuwa ndani ya sala au pahala pengine huitwa (sehemu za siri). Kufunua sehemu za siri na kuangalia sehemu za siri za mwengine ni haram. Mtu anayesema kwamba Uislam hauna mambo kuhusiana na sehemu za siri basi anakuwa kafiri. Ijma'a yani katika medhehebu manne anayesema kwamba ni halali kufunua au kuangalia sehemu za siri za mwengine au asielipa umuhimu jambo hili yani asieogopa adhabu za kufanya makosa ya kufunua na kuangalia sehemu za siri za wengine anakuwa kafiri. Halini hiyo hiyo wanawake kufunua sehemu zao za siri na kuwa karibu na wanaume wakiimba kama inavyofanywa wanaposoma mawlid. Kwa wanaume kati ya magoti na nyonga kulingana na madhehebu ya Hambali sio utupu (sehemu za siri).

mafunzo ambayo yameenea au yanayofaa kwake kujua, basi hawi kafiri anakuwa faasiq.

## NGUZO ZA IMANI

Mtu huyu akauliza tena, ya Rasulallah "swallallahu alaihi wa sallam" hebu nijulishe **Imani ni kitu gani**. Baada ya kuuliza Uislamu ni nini na kupata majibu, Jibril "alaihis-salaam" alitaka kutoka kwa bwana wetu Rasul "swallallahu alaihi wa sallam" ufafanuzi kwa upana wa ukweli na umuhimu wa Imani. Imani katika lugha maana yake ni kumtambua mtu kuwa mkweli na kumuamini. Katika Uislam, imani ni kuamini kwa ukamilifu kwamba Rasulullah "swallallahu alaihi wa sallam" ni mtume wa Allahu taala, kwamba yeye ni Nabii, mjumbe aliyechaguliwa na Allah, na kusema haya kwa imani moyoni; na kuamini kwa ufupi yale aliopewa mtume kwa ufupi na kuamini kwa jumla yale aliopata kwa undani kutoka kwake

---

Kwa yeyote anayejiita Muislam, ni lazima kujifunza nguzo za Uislam na za İman kisha mafunzo kuhusu haram na halali kulingana na madhehebu manne na kuyapa umuhimu. Kutojua kwake sio hoja, yaani ni kama anayejua halafu akakataa kuamini. Wanawake kulingana na madhehebu manne,mwili wao ni utupu isipokuwa uso wao na viganja vyae. Katika ijma'a yaani kulingana na madhehebu mengine sehemu zisizochukuliwa kama utupu na kutopewa umuhimu akiziangalia mtendaji hawi kafiri, lakini ikiwa inazingatiwa kwenye madhehebu yake kwamba ni utupu, basi anapata dhambi. Mfano mwanaume kuacha wazi paya lake kuanzia magoti hadi nyonga. Asipofahamu kujielimisha ni lazima. Anapojua anapaswa kufanya toba na kuanza kujifunika. Kusema uongo, kusengenya, kukashif, uizi, kufanya njama, kusingizia, kuvunja mwoyo, kusambaza fitina, kutumia mali ya mwenzako bila ruhusa, kutolipa wafanya kazi mishahara yao, kuasi serikali, yani kutofuata sheria, kwenda kinyme na sheria za serikali, kutolipa ushuru pia ni dhambi. Haya kuyatenda dhidi ya makafiri hata ukiwa kwenye dola isio ya Uislam kuyafanya ni haram. Kwa wajinga vitu visivyo maarufu au lazima vitu hivo wajinga kutovijua kwao hakuwafanyi makafiri.

Allahu taala, na kutamka Kalimat ash-shahada pale inapofaa. Imani ya kweli ni sawa sawa kama tunavyojua kwamba moto unachoma, nyoka anaua kwa sumu na tukaepuka vitu hivyo. Hivyo basi tunafaa kumtambua Allahu taala na sifa zake zenye ukubwa, kujua haya kiukamilifu wa moyo, kutamani neema zake na kukimbilia uzuri wake (jamal), na kujitahadhari na hasira zake na adhabu zake. Tunafaa kuiandika imani hii kwenye moyo kama maandishi yanayoandikwa kwenye marumaru (gololi).

Kama alivyofundisha Muhammad "alaihis-salaam" imani na Uislamu ni kitu kimoja. Maana ya kalimatu shahada ni kuamini na katika zote mbili, yani imani na Uislamu kupo. Hata hivyo zinatofautiana kiujumla na kimalengo na pia maana yake kilugha lakini havina tofauti katika Uislamu.

Imani ni kitu kimoja au ni mchanganyiko wa vipande? Na kama ni mchanganyiko, imeundwa kutoka kwa vipande vingapi? Amal, ibadat, hutoka kwenye imani au la? Unaposema kwamba nina imani, inaruhusiwa kuongeza inshaallah au la? Ni kweli Imani inapungua na kuongezeka? Imani ni kiumbe? Ni uwezo wa mtu kuamini? Au waumini walilazimishwa kuamini? Kama kuna nguvu au kulazimishwa mtu kuamini kwa nini kila mtu aliamrishwa kuamini? Haya yote kuyafafanua moja moja itachukuwa muda. Kwasababu hiyo, sitoyajibu moja moja hapa. Lakini inafaa kujulikana kwamba, kwa mujibu wa madhehebu ya Ash'ari na Mu'tazila, haijuzu kwa Allahu taala kutuamrisha kufanya kitu ambacho hakiwezekani. Na kulingana na Mu'tazila haijuzu kwa Allahu taala kuamrisha kitu ambacho kinawezekana lakini hakilingani na uwezo wa mtu. Kwa mujibu wa Ash'ari inajuzu lakini hajaamrisha. Mfano huu ni kama kumuamrisha mtu kuruka hewani. Katika Imani, kufanya ibada au katika amali zote Allahu taala hajaamrisha waja wake zaidi ya uwezo wao. Kwa sababu hiyo, mtu akipoteza akili au kasahau au kalala au kafa wakati ni Muislamu basi ataendelea kwa hali ya Uislamu hata asipokuwa katika hali ya kuthibitisha.

Tusifikiriye maana ya hadithi hii kilugha kwa sababu katika enzi za kijahiliya hakuna muarabu yeyote asiejua kwamba maana yake ni 'kuthibitisha na kuamini'. Kwa hakika masahaba "radiyallahu taala anhum ajma'in" walijua maana yake pia lakini Jibril "alaihis-

salaam" alitaka kuwafundisha masahaba kwa kuuliza imani ina maana gani katika Uislamu. Na Rasulullah "swallallahu alaihi wa sallam" alisema kwamba imani ni kuamini mambo sita yenye ukweli.

1. **“Mwanzo wa vyote, ni kumuamini Allahu taala”;** alisema, iman ni kuwa na imani ya kweli kwenye mambo sita kwa njia ya utume au ilham au kwa kutumia akili kwa kupata ushahidi au kuamini na kufuata maelezo sahihi yaliothibitishwa na kuthibitisha kwa ulimi.

Ya kwanza kati ya nguzo sita ni kwamba Allahu taala ni wajib al-wujud na ndio muabudiwa wa kweli na ndiye muumbaji wa viumbe wote. Inafaa kuaminiwa kwamba ndiye pekee alieumba kila kitu [kila dutu, atomi, elementi, molekuli, misombo/maungano, oganik, seli, uhai, kifo, kila tukio, kila mmenyuko, nguvu za aina zote na nishati za aina zote, harakati, sheria, roho, malaika na viumbe wote wenye uhai au wasio na uhai nje ya kitu chochote, na akavifanya viweze kuishi] kote hapa duniani na baadae bila kufa, zamani au mfano wake, nje ya hali ambayo haijawahi kutokea. Kama alivyoumba viumbe wote kwenye ulimwengu [katika wakati mmoja hali yakua vilikua havijatokezea], hivyo hivyo aliumba baadhi yao kutoka kwa vingine, na wakati wa kiama utakapofika, kwa wakati mmoja atateketeza kila kitu. Yeye ndiye muumbaji, mmiliki, mtawala kabisa wa viumbe wote. Inafaa kuamini na kukubali kwamba hakuna yoyote anayemtawala, anayempa amri au yuko juu yake yeye. Ubora wa kila aina, sifa zote za ukamilifu, ni zake peke. Hana kasoro, hana sifa zenye upungufu. Ana uwezo wa kufanya anachotaka. Hafanyi kitu kwa ajili ya malipo. Katika kila anachofanya, basi kuna hekima, faida, baraka na neema ndani yake.

Allahu taala halazimiki kuwafaidisha waliowema au kuwapa thawabu hawa na kuwaadhibu wale. Ingefaa kwa ubora wake na ukarimu wake akiwaingiza wenye maovu wote peponi. Na ingekuwa haki yake akiwatia wote wanaomtii na kumuabudu kwenye moto. Ila ameshasema na kutangaza kwamba Waislamu wanaomuabudu atawaingiza peponi na atawapa neema, na atawaadhibu makafiri kwenye moto. Yeye hakiuki maneno yake. Hapati faida kama viumbe hai wote wangeamini na kumuabudu

wala hapati madhara kama viumbe hai wote wakiamua kumuasi kwa wingi. Mtu anapotamani kufanya jambo, basi yeye Allah nbie anaunda jambo hilo akitaka. Ndio yeye pekee anayeunda kila kitendo kinachotendwa na binaadamu na vitu vyote. Asipotaka au asipounda, hakuna kinachoweza kupiga hatua. Asipotaka hakuna anayeweza kuwa kafiri au mpinzani. Anaunda ukafiri na makosa/madhambi hali yakua hayuko radhi nayo. Hakuna anayeweza kuingilia kazi zake. Hakuna mwenye haki kuuliza kwa nini kafanya hili au lile au kutoa maoni kwa jinsi gani anavyopaswa kufanya kazi zake. Atamsamehe atakapotaka mtu aliefanya dhambi kubwa na akafa bila kufanya toba, isipokuwa mushriku au kafiri. Mwenye madhambi madogo atamuadhibu atakapotaka. Alishatangaza kwamba kafiri na murtadi hatowasamehe na atawaadhibu milele.

Atawaadhibu pia Waislamu wanaomuabudu lakini imani yao haiambatani na imani ya **Ahl-as-Sunna** na wanaokufa bila kutubu. Lakini Waislamu hao wenye bid'a hawatokaa kwenye moto milele.

Inawezekana (ja'iz) kumuona Allahu taala kwa macho hapa duniani, lakini hakuna mtu yeyote aliewahi kumuona. [Allahu taala hajawahi kujionyesha. Hata kwa hisia hajawahi kutambulika. Kwa hali hiyo ni rehma kubwa kwa watu. Laiti angeonwa, watu wabaya wangemuudhi na kumkejeli, na ingekuwa sababu tena ya kukasirishwa na kutuadhibu.] Kwenye siku ya kiama ataonwa na makafiri na Waislamu wenye kufanya madhambi kwenye hali ya ghadhabu na hasira, na waumini Waislamu watamuona katika hali yake ya ukarimu na uzuri. Malaika na wanawake nao watamuona pia. Makafiri watanyimwa fursa ya kumuona katika hali hii. Kuna nakala mbali mbali zinazoonesha kwamba majini nao pia watanyimwa haki ya kumuona Allah. Kulingana na wanazuoni walio wengi, waumini wa daraja la juu watamuona kila asubuhi na jioni, na wale wa daraja la chini watakuwa wanamuona ijumaa tu, na kwa wanawake watakuwa wanamuona kwa mwaka mara kadhaa kama siku za sherehe katika mwaka, kwa uzuri na heshima yake. [**Sheikh Abdulhak-i Dehlewi**[1] farisi katika kitabu chake **(Tekmil-ul-iman)** anasema kwamba: hadithi tukufu inasema, (siku ya kiama Mola

[1] Abdulhak-i Dehlewi alikufa 1052 (1642 m) katika mji wa Delhi.

wenu mtamuona kama munavyouona mwezi kwenye siku kumi na nne zake!). Allahu taala kama anavyojulikana kwa njia isiyoeleweka hapa duniani, na siku ya kiama pia ataonekana kwa njia hiyo. Wanazuoni wakubwa kama Abu al-Hasan al-Ashʿari, Imamu Suyuti na Imamu Bayhaki walisema kwamba malaika nao pia watamuona Allah. Imamu A'zam Abu Hanifa pamoja na wanazuoni wengine wanasema majini hawatolipwa thawabu na hawataokolewa na jahannam, lakini waumini miongoni mwao wataokolewa na jahannam. Kwa wanawake watamuona Allah mara kadhaa kama inavyotokea siku za sherehe hapa duniani. Waumini kamili watapata kumuona kila asubuhi na jioni, wengine watamuona ijumaa tu. Wanawake waumini, malaika na majini nao wamo katika habari njema hii ya kumuona siku ya ijumaa. Wanawake waliokamilika kama Fatima uz-zahara, Khadija ul-kubra, Aisha al-siddiqa na wengine wake zake mtume, Mariam na Asiya radhi zake Allah ziwe juu yao watapewa fursa ya kipekee kuliko wanawake wengine. Na Imamu Suyuti alimaanisha haya.] Inafaa kuaminiwa kwamba Allahu taala ataonwa. Lakini hatupaswi kutaswiri namna ambavyo itatokea, kazi zake hazifahamiki kwa njia ya akili. Hazifanani na masuala ya kidunia. [Hazipimwi kwa kutumia vigezo vya kimwili au kikemikali.] Dhana kama muelekeo, kuwa kinyume chake havina uhusiano na Allahu taala. Mungu sio kifaa wala sio mwili [sio elementi/kipengele, mchanganyiko wala sio muungano wa vitu]. Haisabiwi, hawezi kupimwa wala hapigiwi mahesabu. Hana mabadiliko. Yeye sio mahali, sio eneo, hayupo kwenye muda, hana iliopita wala ijayo, mbele au nyuma, chini au juu, kulia au kushoto.

Kwa hivyo hakuna kitu chake kinachofahamika na fahamu ya mtu, wala akili za binaadamu au akili tosha kufanya hivyo. Kwa hivyo mtu hawezi kutafakari Allah ataonwa vipi. Hata hivyo maneno kama mkono, mguu, mwelekeo, mahali na kadhalika, ambavyo havifai kwa Allahu taala, vipo katika aya na hadithi, lakini maana yake sio kama tunavyofahamu na kutumia sasa. Aya na hadithi kama hizo zinaitwa **mutashabihat**. Tunapaswa kuziamini, lakini hatufai kujaribu kujua jinsi zilivyo. Au zinaweza kufafanuliwa kwa njia ya **Ta'wil** kwa upana au kwa maelezo; na zinaweza zikapewa maana inayofaa kwa Allahu taala. Kwa mfano, neno mkono linaweza kutafsiriwa kama nguvu/mamlaka.

Mtume Muhammad "alaihis-salaam" alimuona Allahu taala kwenye Miraj. Lakini kuona hapa hakukua kwa macho kama hapa duniani. Mtu anayedai kwamba kamuona Allahu taala hapa duniani anakuwa zindik. Kuona kunakotokea kwa kina awliya ni tofauti na kuona kwa hapa duniani au kuona katika akhera. Kwa mambo mengine, sio ru'yat (kuona) lakini ni **ushahidi** unaojitokeza kwao, [kwa kusema, wanaona mifano (mithal) kwa njia ya macho ya nyoyo zao]. Baadhi ya awliya walisema kwamba walishamuona. Hata hivyo walichanganya ushahidi uliojitokeza wakati wako katika hali ya sekr, tuseme wakati wamepoteza fahamu na ru'yat au maneno yao haya yanahitaji ufafanuzi.

**Swali:** "Hapo juu imetajwa kwamba inawezekana (ja'iz) kumuona Allahu taala kwa macho hapa duniani. Kisha kwa nini tena mtu anayesema kitu kinachowezekana kutokea anakuwa zindiq? Kama mtu anayesema hivyo anakuwa kafiri, kuna uwezekano wakusema kwamba kinawezekana?"

**Jawabu:** Neno **'ja'iz'** kilugha maana yake ni 'kuwezekana kutokea au la'. Hata hivyo kulingana na madhehebu ya al-Ash'ari [Abu al-Hasan Ali ibn Ismail, alikufa katika mji wa Baghdad mwaka 330 sawa na 941 milad.], uwezekano wa ru'yat ina maana kwamba Allahu taala ana uwezo wa kuumba hisia tofauti ndani ya mtu inayomuwezesha kuona kwenye dunia hii ambayo ni tofauti na kuona kwa karibu au uso kwa uso na yeye, na tofauti na kuona kwa sheria za kimaumbile alizo umba katika dunia hii. Kwa mfano: Ana uwezo, hivyo inawezekana, kumuonesha kipofu aliyoko china mbu aliyoko Andalus, na kitu kilicho kwenye mwezi au nyota kwa mtu ambaye yupo ardhini. Nguvu kama hizo ni za kipekee kwa Allahu taala tu. Jawabu la pili, ni kusema, "nimemuona kwenye dunia hii", amekwenda kinyume na Aya'tul karim pamoja na maulamaa. Kwahiyo, yule anayetamka kauli hiyo basi anakuwa **mulhid** au **zindiq**.[1] Jawabu la tatu, tunasema kwamba, neno "inawezekana kumuona Allahu taala kwenye dunia hii" haina maana kwamba "inawezekana kumuona ardhini kwa sheria za kimaumbile". Hata

[1] Mulhid au zindiq anasema kwamba ni Muislamu. Mulhid kwa maneno yake anaamini kwamba ni Muislamu pia kwamba yupo kwenye njia sahihi. Hata hivyo Zindiq yeye ni adui wa Uislamu. Anadai kuwa Muislamu ili aweze kudhuru Uislamu kwa ndani na kupoteza Waislamu.

hivyo mtu anaposema kamuona Allahu taala inamaana kwamba kamuona kama anavyoona vitu vingine; huku ni kuona ambako hakuwezekani (ja'iz). Mtu anayetamka maneno ya kikafiri anaitwa **mulhid** au **zindiq**. [Baada ya majibu haya, Hadhrat Mawlana Khalid alisema kwamba: "kuweni waangalifu" hiyo akawa anatilia mkazo jibu la pili].

Kupita kwa muda, mchana au usiku, haviwezi kulinganishwa na Allahu taala. Kwa namna yoyote hakutokei mabadiliko kwake, wala haisemekani kwamba alikuwa katika hali hii nyuma au atakuwa katika hali fulani baadae. Habadiliki kwenda kitu kingine (hulul/ incarnation) umwilisho. [Kundi moja la washiia wanaojiita **Nusayriyya** wanaamini na kusema kwamba Allahu taala aliingia kwa Ali. Itikadi mbovu hii inawafanya kuwa makafiri.] Haungani na kitu chochote. Hajawahi kuwa na kinyume, mgeuko, kufanana, mpenzi, msaidizi au mlinzi. Hana baba, mama, mtoto wa kiume, mtoto wa kike au mke. Daima yuko pamoja na kila mtu, amezunguka na anaona kila kitu. Kwa kila mtu yuko karibu naye sana kuliko mshipa kwenye shingo yake. Hata hivyo, kuzunguka kwake kwetu, upatikanaji wake au umoja au ukaribu, sio kama tunavyofahamu sisi kutokana na maneno haya. Ukaribu wake hauwezi kufahamika na maarifa ya wanazuoni, na akili za wanasayansi, au na kashfu au shuhud ya kina awliya. Akili za binaadamu haziwezi kuelewa maana yake kwa undani. Allahu taala ni wakipekee kwa dhati yake na sifa zake. Hakuna mabadiliko wala tofauti zinazojitokeza katika dhati na sifa zake.

Majina yake Allahu taala yanaitwa **Tawqifi**, kwa kusema, inaruhusiwa kutumia majina yake yaliooneshwa na Uislamu na hairuhusiwi kutumia maneno mengine kwa kumaanisha Yeye. [1] Majina yake Allahu taala hayana kikomo. Inajulikana vizuri kwamba ana majina elfu moja na moja (1001), kwa kusema majina yake hayo

---

[1] Kwa mfano, Allahu taala anaweza kuitwa "Alim" lakini hatuwezi kutumia neno 'fiqih' ambalo nalo lina maana ya Alim, Uislamu hautumii 'fiqih' kumanisha Allahu taala. Hivyo hivyo, hairuhusiwi kutumia neno God badala ya Allah, kwa sababu 'god' maana yake ni 'sanam'; "ng'ombe" ni god (mungu) wa wahindi, kwa mfano. Inaruhusiwa kusema "Allah ni mmoja; hakuna mungu isipokuwa Yeye." Maneno kama Dieu (kifaransa) na Gott (kijerumani) yanaweza kutumika kwa mungu lakini sio kwa Allah.

elfu moja na moja aliyadhihirisha/kuyatangaza kwa binaadamu. Katika dini ya Muhammad "alaihis-salaam"; majina tisin na tisa (99) yanayoitwa **Asma’ ul husna** yalidhihirishwa.

Kuna sifa nane za Allahu taala yaitwayo **Sifaat ath-Thubuutiyya**, kulingana na madhehebu ya **Maturidiyya** na pia saba katika madhehebu ya **Ash’ariyya**. Sifa zake hizi ni za milele kama dhati yake, tuseme kwamba yapo daima. Sifa hizo ni tukufu. Haziko kama sifa za viumbe. Haziwezi kufahamika kwa kutoa hoja au kudhania au kwa kuzilinganisha na binaadamu hapa duniani. Allahu taala amewajaalia watu mfano wa kila sifa yake. Kwa kuona mifano hii, kidogo sifa zake Allahu taala zinaweza kufahamika. Kwa vile mtu hawezi kumfahamu Allahu taala basi hairuhusiwi kumtasawari au kujaribu kumfahamu. Sifa zake nane hizi haziko sawa na yeye; yani sifa zake hazimfanyi kuwa yeye, wala hazimzidi. Sifa nane ndio hizi:

**Hayat** (uhai), **Ilm** (mjuaji), **Sam’u** (kusikia), **Baswar** (kuona), **Qudra** (uwezo), **Kalam** (kuzungumza), **Irada** (matakwa) na **Tekwin** (ubunifu). Kwenye madhehebu ya Ash’ariyya, Takwin na Qudra ni sifa moja. Mashiyya na Irada ni sawa.

Kila moja ya sifa nane za Allahu taala ni ya aina yake na katika hali yake. Hakuna mabadiliko yanayoweza kutokea katika moja ya sifa hizo. Lakini kila moja inatofautiana kulingana na uhusianu wake katika viumbe. Sifa zake kutofautiana kulingana na uhusiano wake kwa viumbe hakuna madhara yoyote kwenye upekee wake. Vile vile, hata hivyo Allahu taala ameumba viumbe vingi na anavilinda dhidi ya kuangamia, bado yeye ni mmoja tu. Hakuna mabadiliko yaliyowahi kujitokeza Kwake. Kila kiumbe kinamuhitaji yeye kila muda kwa hali yoyote. Lakini yeye hamuhitaji yoyote.

2. **Nguzo ya pili katika nguzo za iman ni kuamini malaika Wake**; malaika, maana yake ni, mjumbe, mtoa habari au nguvu. Katika hali ya umbo pia ni latif. Wapo katika hali ya mwangaza. Wana uhai. Ni wenye akili. Malaika hawana ubaya kama wa watu. Wana uwezo wakubadilika kwa kila sura. Kama ilivyo kwa gesi kubadilika kuwa kioevu (majimaji) na kuwa imara baadae na kugeuza sura, vile vile malaika nao wanaunda muundo mzuri. Malaika sio nafsi zilizotokana na miili ya watu mashujaa. Wakristu wanadhani kwamba malaika ni kama roho. Wao sio kama nishati au nguvu, ambavyo havina mwili. Baadhi ya wanafalsafa wa zamani

walidhania hivyo. Wote huitwa **malaika**. Malaika waliumbwa kabla ya viumbe hai vyote. Ndio sababu tumeamrishwa kuwaamini kabla hatuja amini vitabu vilivyoteremshwa. Vitabu navyo tunaviamini kabla ya mitume; katika Quran vitu vya kuaminiwa vinapangwa kwa mtiririko.

Kuamini malaika kunafaa kuwa kama ifuatayo: malaika ni viumbe wa Allahu taala. Sio wapenzi wake wala sio watoto wake wa kike kama makafiri na washirikina wanavyodhania. Allahu taala anawapenda malaika wote. Wanatii amri zake na hawajawahi kufanya dhambi wala kuasi amri zake. Malaika sio wanaume wala wanawake. Hawaoi wala hawaolewi. Hawana watoto. Wana uhai yaani wako hai. Pamoja na kwamba habari kutoka kwa Abdullah ibn Masud "radiyallahu anhu", inasema kwamba baadhi ya malaika walikuwa na watoto na miongoni mwao ni iblis na majini. Swali hili limejibiwa kwa kina kwenye vitabu. Allahu taala Alipotangaza mbele ya malaika kwamba anaumba kiumbe binaadamu, malaika waliuliza, "Ya Rabbi! Unataka kuumba viumbe ambavyo watafisidi kwenye ardhi na kumwaga damu?" maswali kama haya yanaitwa **dhella**.

Katika viumbe wote malaika ndio wengi zaidi. Hakuna zaidi ya Allahu taala anayejua idadi yao. Hakuna sehemu faragha mbinguni isipokuwa malaika wapo wanamuabudu Mwenyezi Mungu. Mbinguni kila mahali pamejaa malaika wanao rukuu au kusujudu. Kwenye mbingu, ardhini, kwenye majani, kweye nyota, kwenye kila kiumbe kilicho hai na kisicho hai, kila kwenye tone la mvua, majani ya mimea, atomi, molekuli, kwenye kila mmenyuko, mwendo, kwenye kila kitu, malaika wana kazi. Wanatekeleza amri za Allahu taala kila mahali. Ni waunganishi kati ya Allahu taala na viumbe. Baadhi yao ni viongozi wa malaika wengine. Baadhi yao walikuwa wanaleta ujumbe kwa mitume miongoni mwa watu. Baadhi ya malaika wanaleta dhana nzuri zinazoitwa **"ilham"** kwenye moyo wa binadamu. Baadhi yao hawana habari yoyote kuhusu binadamu na viumbe wengine na wamepoteza fahamu kutokana na hisia zao juu ya uzuri wa Allahu taala. Kila mmoja wa malaika hawa yupo kwenye

sehemu yake na hawezi kuondoka kwenye sehemu hiyo. Baadhi ya malaika wana mbawa mbili na wengine wana nne au zaidi.[1]

Malaika wanaohusika na pepo wapo kwenye pepo. Kiongozi wao anaitwa **Ridhwan**. Malaika wanaohusika na jahannam wanaitwa **Zabani** wanatekeleza kazi wanazoamrishwa huko. Moto wa jahannam hauwadhuru, kama ilivyo bahari na samaki. Kwenye jahannam hawa malaika wanaoitwa Zabani idadi yao ni kumi na tisa lakini kiongozi wao anaitwa **Malik**.

Kwa kila mtu, kuna malaika wanne wanaoandika matendo mema na mabaya anayotenda. Wawili kati yao wanakuja usiku na wengine wawili wanakuja wakati wa mchana. Malaika hao wanaitwa **Kiraman Katibin** au malaika wa **Hafaza**. Inaripotiwa kwamba hawa hafaza ni tofauti. Malaika ambaye yuko kwenye upande wa kulia ni kiongozi wa yule kwenye upande wa kushoto na anaandika matendo mema. Yule kwenye mkono wa kushoto anaandika matendo maovu. Kuna malaika wataowaadhibu makafiri na Waislamu wapotofu kwenye makaburi yao, na kuna malaika watakaouliza maswali kwenye kaburi. Malaika wenye majukumu ya kuuliza maswali kwenye kaburi wanaitwa **Munkar** na **Nakir**. Malaika watakaouliza Waislamu wanaitwa **Mubashir** na **Bashir**.

Malaika miongoni mwao kuna wenye vyeo vya juu kuliko wengine. Wenye vyeo vya juu zaidi ni wanne. Wa mwanzo ni **Jibril** "alaihis-salaam". Huyu kazi yake ni kuteremsha **Wahy** kwa mitume na kuwajulisha maamrisho na yaliokatazwa. Wapili ni **Israfil** "alaihis-salaam" ambaye kazi yake ni kupuliza baragumu (Sur). Atapuliza baragumu mara mbili. Mara ya kwanza kila kilicho hai kitakufa isipokuwa Allahu taala. Na mara ya pili kila kitu kitafufuka.

---

[1] Kama ilivyo mbawa za kila ndege (birds) na mbawa za ndege (airplane) zina muundo wake na ni tofauti na mbawa za vitu vingine, vile vile mbawa za malaika nao zina muundo wake. Tunaposikia jina la kitu ambacho hatujawahi kuona au hatukijui, tunadhani kwamba kinafanana na vile tunavyovijua. Kitu ambacho siyo sahihi. Tunaamini kwamba malaika wana mbawa lakini hatujui zikoje. Picha za wanawake wenye mbawa zilizopo kwenye makanisa, machapisho au sinema, ambazo hujulikana kama malaika ni uongo mtupu. Muislamu hafanyi picha kama hizo. Tusizingatie picha za uongo hizi ambazo zinatengenezwa na wasio Waislamu kuwa za kweli na hatupaswi kuwaamini maadui zetu.

Watatu ni **Mika'il** "alaihis-salaam" jukumu lake ni kufanya urahisi, ughali, uhaba, wingi [kiuchumi, kuleta faraja na raha] na kukiendesha kila kitu. Wanne ni **Izrail** "alaihis-salaam" na kazi yake ni kutoa roho za watu. Baada ya malaika hawa wanne, kuna tabaka lengine ambalo liko juu yao nao ni mbeya nne: kuna malaika wanne wanoitwa **Hamalat al-Arsh**, kwenye siku ya kiama watakuwa wanane; Malaika waliopo mbele ya Allahu taala wanaoitwa **Muqarrabun**; malaika wenye kuadhibu wanaoitwa **Karubiyun**; malaika wa rehma wanaoitwa **Ruhaniyun**. Malaika wote hawa wenye vyeo vya juu ni wenye daraja la juu kuliko watu wote isipokua mitume "alaihimus-salaam". Waumini na maawliyai miongoni mwa Waislamu ni wenye vyeo vya juu kuliko malaika wa daraja la chini. Na malaika wa daraja la chini ni wenye vyeo vya juu kuliko Waislamu wa daraja la chini kwa mfano: wanaomuasi Allahu taala. Makafiri ndio wenye daraja la chini kabisa miongoni mwa viumbe vyote.

Baada ya kupulizwa baragumu mara ya kwanza, malaika wote watakufa isipokuwa Hamalatul-arshi na wale malaika wanne wakubwa. Halafu hamalatul-arsh na wale malaika wanne wakubwa nao watakufa. Kupulizwa baragumu mara ya pili malaika wote watafufuka na watakuwa hai kabla ya kila kitu. Hamalatul-arsh na malaika wanne wakubwa watafufuka kabla ya kupulizwa baragumu mara ya pili. Yaani malaika hawa kama walivyoumbwa kabla ya viumbe hai vyote, basi watakufa baada ya kufa viumbe wote.

3. **Nguzo ya tatu ni kuamini vitabu vilivyoteremshwa na Allahu taala kwa mitume**. Vitabu hivi, Allahu taala Aliviteremsha kwa mitume kupitia kwa Malaika. Baadhi ya mitume aliwasikilizisha kwa masikio yao matukufu, tena baadhi yao, ujumbe uliandikiwa kwenye karatasi. Wengine wakisikilizishwa ujumbe bila malaika. Vitabu hivi vyote ni maneno yake Allahu taala. Ni abadi (daima) na azali (milele). Hayakuumbwa. Vitabu hivi sio maneno ya malaika wala maneno ya mitume. Maneno ya Allahu taala sio kama maneno haya tunayoandika, tunayoweka kwenye akili zetu na tunayosema, Sio kama yalioandikwa, yanayosemwa na yanayopatikana kwenye akili, sio yenye herufi wala sauti, Mtu hawezi kufahamu Allahu taala jinsi alivyo na sifa zake. Ila maneno hayo watu wanayasoma. Wanayaweka kwenye akili na

wanayaandika. Maneno hayo yanapokuwa nasi, basi yanakuwa hadithi (tukio). Maneno ya Allahu taala yanapokuwa pamoja na watu basi ni kiumbe na ni tukio. Maneno ya Allahu taala yanapokuwa katika hali ya kutafakari basi hapo yanakuwa kadim (zamani).

Vitabu vilivyoteremshwa na Allahu taala vyote ni vya haki na kweli. Havina uongo wala udanganyifu. Allah anaposema ataadhibu, kutesa au kusamehe inategemea na kutaka kwake kwa sababu sisi hatujui sharti zake au irada yake. Au maana yake ni kwamba mja ambaye alistahiki kuadhibiwa anaweza akasamehewa. Maneno yanayoeleza kuhusu adhabu na mateso dhidi ya dhambi fulani yanakuwa sio uongo iwapo Allah anaamua kusamehe. Kama ilivyo kwamba haijuzu kwa Allahu taala kutotekeleza neema alizoahidi, ni inajuzu kusamehe madhambi. Akili na aya tukufu vyote vinaonesha hivyo.

Ni muhimu kufafanua aya tukufu na hadithi sharif kwa maana yake inayofahamika isipokuwa tukihisi uwezekano wa hatari au usumbufu kutokea. Hairuhusiwi kutumia maana iliokaribu au kufanana na maana yake.[1]

Aya zinazoitwa **Mutashabihat** hazifahamiki, zina maana ya siri. Ni Allahu taala pekee anayefahamu na wachache ambao walijaaliwa kwa kupewa **İlmu-lladuni** ndio wanaoweza kufahamu maneno yake kama ilivyoelezwa. Hakuna mwengine anayeweza kufahamu. Ndio sababu, tunapaswa kuamini aya Mutashabihat kwamba ni maneno ya Allahu taala bila kuchunguza maana yake.

Katika madhehebu ya Ash'ar wanasema inaruhusiwa kufafanua aya kama hizi kwa ufupi au kwa kina kama **Ta'wil**. Ta'wil maana yake ni kuchagua maana moja katika maana nyingi inayofafanua neno moja, na maana ambayo sio ya kawaida. Kwa mfano, kuhusu aya hii, **"Mkono wa Allah uko juu ya mikono yao,"** katika maana ya aya, neno la Allahu taala. Tunapaswa kusema kwamba nimeamini

---

[1] Quran tukufu na hadithi sharif vipo katika lugha ya Kuraish na lahaja hiyo hiyo. Lakini maneno yanafaa kufafanuliwa kulingana na maana iliotumika kwenye mji wa Hijazi miaka elfu moja mia nne iliopita. Sio sahihi kutafsiri maneno hayo kwa kuyapa maana tunayotumia sasa, kwasababu yamebadilika kutokana na mda.

maana Allahu taala aliokusudia katika aya hii. Siwezi kufahamu maana yake Allahu taala pekee ndio Anaejua, hii ndio njia bora. Au kusema elimu yetu sio kama elimu yake Allahu taala. Irada yake haifanani na irada yetu. Mkono wake Allahu taala pia sio kama mikono ya watu.

Kwenye vitabu alivyoteremsha Allahu taala, aidha matamshi au maana ya baadhi ya aya tukufu au vyote, vilibadilishwa (naskh) na Yeye. Quran tukufu ilichukua nafasi ya vitabu vyote na kukomesha uhalali wa sheria za vitabu hivyo. Hakutatokea kosa lolote, ongezeko, kusahau au kukosa nukta yoyote kwenye Quran tukufu hadi mwisho wa dunia, wala haitosahaulika. Elimu ya zamani na ya baadae yote ipo kwenye Quran tukufu. Kwa sababu hii, iko juu na ina thamani kubwa kuliko vitabu vyengine. Muujiza mkubwa wa mtume "swallallahu alaihi wa sallam" ni Quran tukufu. Ikiwa Watu wote na majini wangeungana kwa pamoja kujaribu kusema kitu kinachofanana na sura fupi zaidi kwenye Quran tukufu, basi wangeshindwa. Kwa kweli, washairi fasihi wa Arabia waliungana na kutamani sana, lakini walishindwa kusema kilicho kama aya tatu fupi. Hawakuweza kushindana na Quran tukufu. Walifanywa kuonekana wajinga. Allahu taala anawafanya maadui wa Uislamu kutoweza na kushindwa mbele ya Quran tukufu. Ufasaha wa Quran tukufu uko juu ya uwezo wa binaadamu. Binaadamu hawana uwezo wa kusema kama inavyosema aya katika Quran tukufu sio kama mashairi, nathari au nyimbo za binadamu. Hata hivyo, herufi zake zilitumika na washairi fasihi na watu wa Arabia.

Vitabu vilivyoteremshwa kutoka mbiguni kwetu ni mia na vinne. Katika vitabu hivi Suhufi kumi (10) alipewa **Adam** "alaihis-salaam", hamsini (50) suhuf **Shith (shet)** "alaihis-salaam", thelathin (30) suhuf **Idris** "alaihis-salaam", kumi (10) **Ibrahim** "alaihis-salaam" ndio maarufu. **Taurat** iliteremshwa kwa Musa "alaihis-salaam", **Zabur** iliteremshwa kwa Dawud alaihis-salaam, **Injil** iliteremshwa kwa Issa "alaihis-salaam" na **Quran tukufu** iliteremshwa kwa Muhammad "alaihis-salaam".

Mtu anapotaka kutoa amri au kukataza kitu, kuuliza kitu au anapotaka kutoa habari, kwanza anafikiria kuhusu kitu hicho na anakiandaa kwenye akili yake. Mchakato huo wa kufikiria kwenye akili huitwa **“kalam nafsi,”** neno ambalo halisemwi kuwa la kiarabu,

kiajemi au kingereza. Kupitia kwake kwenye lugha tofauti tofauti hakufanyi maana yake kubadilika. Maneno yanayoeleza maana hii yanaitwa **“kalam lafzi.”** Kalam lafdhi yanaweza kuelezwa kwenye lugha Tofauti. Kutokana na haya tunafahamu kwamba, kalam nafsi ni kama sifa zingine kama elimu, irada, kuona... Zinakaa kwenye akili za mwenyewe hazibadiliki. Lakini kalam lafdhi, ni mkusanyiko wa herufi zainazoelezea kalam nafsi kutoka kwenye mdomo wa msemaji na kuelekea sikio. Vile vile, neno la Allahu taala ni la milele, daima, lenye sauti na sio kiumbe. Ni sifa tofauti na Sifaat adh-Dhaatiyya na Sifaat ath-Thubutiyya za Allahu taala, kama Elimu na Irada.

Sifa kalam (kusema/neno) ni basit (simpol), Hayabadiliki. Sio yenye herufi wala sauti. Haiwezi kupangwa au kuainishwa kama amri, kukataza, kusimulia kama kiarabu, kiajemi, kiyahudi, kituruki au kishamu. Haichukuwi sura kama hizi. Haiandikiwi. Haihitaji vifaa kama akili, sikio au ulimi. Inasemekana kwa kutumia lugha yoyote. Kwa hivyo, muarabu akisema basi inaitwa Quran tukufu. Muyahudi akisema inaitwa Tawurat. Msiriya akisema inaitwa Injil. [Katika kitabu **sher-ul-makasid**[1] kinaeleza kwamba, ikisemwa kwa kiyahudi inakuwa Injil, na ikiwa kishamu ni Zabur.]

Kalam al-ilahiyya (maneno ya Allahu taala) yanaeleza mada mbali mbali, ikisimulia matukio yaliokuepo au yatakayokuepo, hapo inaitwa khabar (simulizi) Isipokua hivyo inakuwa insha. Ikitangaza mambo yanayofaa kufanywa, inaitwa amri (kuamrisha). Ikitanganza makatazo inaitwa **nahy** (kukataza). Lakini hakuna mabadiliko wala muongezeko unaotokea kwenye Kalam al-ilahiyya. Kila kitabu au kila ukurasa ulioteremshwa ni kati ya karatasi ya maneno ya Allahu taala, kwa kusema ni Kalam an-nafsi Yake. Inapokua kwenye kiarabu inaitwa Quran tukufu.

Wahy unapokuwa katika hali yenye herufi, kuandikwa, kusemwa au kusikika na kuhifadhika kwenye akili inaitwa **kalam lafdhi** na **Quran karim**. Kwa kuwa Kalam lafdhi inaashiria Kalam nafsi, basi inaruhusiwa kuitwa Kalam al-ilahiyya na Sifaat ilahi.

---

[1] Kiliandikwa na Sa’d ad-din at-Taftazani, ambaye alifia kwenye mji wa Samarkand mwaka 792 (1389 miladi).

Kama ilivyo kwa kitabu chote kinaitwa Quran tukufu. Vile vile vipande vyake navyo vinaitwa Quran tukufu.

Wanazuoni wa njia sahihi kwa pamoja walisema kwamba Kalam nafsi sio kiumbe lakini ni kadim (milele). Hakuna kauli ya pamoja kwamba Kalam al-lafzi ni hadithi (tukio) au Kadim (milele). Kundi moja waliosema kwamba ni hadithi baadae walisema kwamba inafaa kutosemwa kwamba kalam al-lafzi ni hadithi. Kwa sababu itakaposemwa hivyo itaeleweka kwamba kalam nafsi nayo ni hadithi. Na hii ndio kauli nzuri zaidi kuhusu maada hii. Akili za binadamu zinaposikia kitu kinachoashiria maana ya kitu kingine basi hukumbuka kitu hicho. Ilielezewa kwamba mmoja kati ya wanazuoni wa Ahl as-Sunna anaposikika akisema kwamba Quran ni hadithi, tunafaa kufahamu kwamba anakusudia sauti na maneno tunayosoma kwa midomo yetu. Wanazuoni wa Ahl as-Sunna kwa pamoja walisema kwamba yote Kalam nafsi na Kalam al-lafzi ni maneno yake Allahu taala. Hata hivyo baadhi ya wanazuoni walisema kwamba majaz, kinachojulikana hapa ni Kalam nafsi maana yake ni maneno ya Allah ambayo ni sifa ya kuzungumza kwake Allahu taala. Kalam al-lafzi ni maneno ya Allahu taala maana yake ni kwamba yaliumbwa na Allahu taala.

**Swali:** Kulingana na maelezo hapo juu inaeleweka kwamba maneno ya Allahu taala ya milele hayasikiki. Mtu anayesema kwamba ‘nimesikia neno la Allahu taala’ maana yake ni kwamba nimesikia sauti na maneno yaliotamkwa au nimefahamu Kalam nafsi kupitia maneno haya. Mitume yote, hata kila mtu anaweza kusikia katika hali mbili hizi. Ni sababu gani kutofautisha Musa "alaihis-salaam" kama Kalimullah (aliesemeshwa na Allahu taala)?

**Jawabu:** Musa "alaihis-salaam" alisikia neno la milele bila herufi wala sauti, kwenye hali iliyotofauti na Adat al-ilahiyya (sheria ya usababisho). Alisikia kwa njia ambayo haiwezekani kufafanua, kama ilivyo kwamba Allahu taala ataonwa kwenye pepo kwenye hali ambayo haifahamiki kiakili wala haielezeki. Hakuna mtu mwingine aliesikia katika hali hii. Au alisikia neno la Allahu taala kwa sauti lakini sio kwa njia ya masikio tu lakini kwa chembe zote za mwili wake, kutoka kwenye kila pande. Au alisikia tu kutokana na mwelekeo wa mti, lakini kwenye muundo wa sauti au vibration ya upepo au kwa njia nyengine. Kwa kuwa alisikia kupitia moja kati ya

hali hizi, aliheshimiwa kwa jina **‘Kalim-u-llah’**. Muhammad "alaihis-salaam" nae kwenye usiku wa Miraj, Kalamu ilahiyyi aliisikia hivi na Jibril "alaihis-salaam" nae wakati wa kuchukuwa Wahy (ujumbe) alichukuwa kwa njia hii.

4. **Nguzo ya nne ni “Kuamini mitume wa Allahu taala”** ambao walitumwa kuongoza watu kufuata njia anayotaka Allah. Kilugha ‘rusul’ (ni wingi wa rasul) ni ‘watu waliotumwa, mitume’. Katika Uislamu, **‘rasul’** ni mtu mtukufu, anaeheshimika ambaye maumbile yake, tabia, maarifa na akili ni juu kuliko watu wengine katika zama hizo, na ambaye hana sifa mbaya kitabia. Mitume walikuwa na cheo cha **‘Iswima**‘ yaani, hawakutenda dhambi kubwa wala ndogo kabla au baada ya kuteuliwa kuwa mitume. [Makafiri wanaotaka kuharibu Uislamu kwa ndani, wanasema kwamba Muhammad "alaihis-salaam" kabla ya kuwa mtume, alichinja mbele ya masanam na wanaonesha dalili kutoka kwenye vitabu vya watu wasio na madhehebu. Uongo wakusingizia huu tunaufahamu kutokana na mistari ya hapo juu.] Baada ya kuteuliwa kuwa mitume hadi pale utume uliposambazwa na kujulikana hawakuwa na kasoro kama upofu, uziwi na kadhalika. Ni lazima kuamini kwamba mitume walikuwa na sifa saba: **Amanat** (amana), **Swidik** (ukweli), **Tablig** (kufikisha), **Adala** (uwadilifu), **Iswimat** (kulindwa dhidi ya maovu), **Fatanat** (smart sana), **Amnul-adha** (kutoachishwa utume).

Mtu mwenye kuleta dini mpya anaitwa **Rasul** (mjumbe). Asiekuja na dini mpya ila anaongoza watu kwa dini iliotangulia anaitwa **Nabii** (mtume). Kueleza watu sheria na kuwaita kwenye dini ya Allahu taala hakuna tofauti kati ya rasul (mjumbe) na nabii (nabii/mtume). Kuamini mitume maana yake ni kuamini mitume yote bila kutofautisha kati yao na kuamini kwamba wote ni wakweli. Anayekataa kuamini mmoja wao basi anakuwa hajawaamini wote.

Utume huupati kwa kufanya kazi, kujiumiza njaa au kujitesa na kufanya ibada sana. Ila unapatwa kwa ihisan na chaguo lake Allahu taala. Dini ilitumwa kwa njia ya mitume ili waweze kuandaa maisha muhimu kwa watu hapa duniani na baadae, na kuwatahadharisha dhidi ya vitendo hatari na kuwafanya wapate uokovu, muongozo, amani na furaha. Ingawa walikuwa na maadui wengi na kufanyiwa masihara na kutendewa kiunyama, mitume hawakuogopa maadui

zao na hawakuonesha kusita katika kuwaambia watu amri za Allahu taala kuhusu mafundisho ya imani na desturi za kidini. Allahu taala aliwaunga mkono mitume yake kwa kuwapa miujiza kuonesha kwamba wametumwa na waukweli. Hakuna yoyote aliyeweza kutoa changamoto dhidi ya miujiza yao. Watu wanaomfuata mtume fulani wanaitwa **umma** wake. Siku ya kiama mitume wataruhusiwa kuombea umma zao, hasa wale waliotenda dhambi kubwa, na maombezi yao yatakubaliwa. Allahu taala pia atawaruhusu wanazuoni, watu wema na walio miongoni mwa umma wao kuomba na maombezi yao yatakubaliwa. Mitume "alaihimus-salaam" wapo hai ndani ya kaburi zao katika uhai ambao hatuwezi kuujua, miili yao tukufu haiozi na udongo. Kwa sababu hii, inaelezwa katika hadithi tukufu: **"Mitume wanasali na kuhiji ndani ya kaburi zao"**.[1]

Kama macho yake mtume yaliobarikiwa yalilala, macho ya moyo wake hayajalala. Mitume wote "alaihimus-salaam" walikuwa sawa katika kutekeleza kazi zao kama mitume na kuwa na ukamilifu wa nubuwwa (utume). Sifa za kipekee saba zilizotajwa hapo juu wote walikuwa nazo. Mitume hawajavuliwa utume kamwe. Lakini awliya wanaweza kuvuliwa uawliya. Mitume walikuwa watu, sio majini au

---

[1] Katika Saudi Arabia siku hizi kuna watu wanaoitwa mawahabi. Watu hao hawaamini hadithi tukufu hizi. Wanaita Waislamu waukweli wanaoamini hadithi tukufu hizi kwamba ni "makafiri". Wao hawawi makafiri kwa tafsiri potofu ya aya tukufu na hadithi za mtume kwa kutumia maana isiowazi na yenye utata. Ni watu wenye uzushi (bid'at). Wanadhuru Waislamu sana. Uwahabi uliazishwa na Muhammad ibn Abd al-Wahhab kutoka mji wa Najdi. Jasus wa kingereza Hempher, alimpotosha kwa kutumia dhana mbaya za Ahmad ibn Taymiyyah (alikufa 728/1328 miladi, kwenye mji wa Damascus). Na ilisambazwa miongoni mwa waturuki na kila sehemu kwa kupitia vitabu vya mmisri Muhammad Abduh (alikufa 1323/1905 miladi, Misir). Wanazuoni wa Ahl as-Sunna katika mamia ya vitabu vyao walithibitisha kwamba mawahabi sio wafuasi wa dhehebu la tano, na kwamba ni watu wenye uzushi wanofuata njia mbaya. Maelezo zaidi yametolewa kwenye vitabu Furaha ya milele na kiama na Akhirat. Allahu taala awasaidie vijana wa kiislamu wasianguke kwenye uzushi wa Wahabi, na asitufanye kuacha njia sahihi ya wanazuoni wa Ahl as-Sunna, ambao wamepongezwa sana kwenye hadithi tukufu nyingi! Amin.

malaika, ambao hawawezi kuwa mitume wa watu au kupata cheo cha utume. Mitume walikuwa wanazidiana. Kwa mfano, umma wa mtume fulani unaweza ukawa na watu wengi au nchi aliotumwa inaweza ikawa kubwa kuliko ya mtume mwengine au wengine, au anaweza akawa amepewa zawadi na neema nyingi, au miujiza yake ikawa mingi na ya daima. Mtume wa mwisho, **Muhammad** "alaihis-salaam" ndio wa juu kuliko mitume wengine. Mitume wanoitwa Ulul-azm walikuwa juu kuliko wengine. Na Rasul (wajumbe) walikua juu kuliko mitume ambao hawakuwa Rasul.

Idadi ya mitume "alaihimus-salaam" haijulikani. Lakini ni maarufu kwamba idadi yao walikuwa zaidi ya **124,000**. Kati ya hao **313** au **315** walikuwa Rasul (wajumbe); **sita** miongoni mwao waliitwa **Ulul-azm**, nao ni: **Adam, Nuh, Ibrahim, Musa, Issa na Muhammad Mustafa** "alaihis-salaam".

Thelathini na tatu miongoni mwa mitume walikuwa maarufu nao ni: **Adam, Idris, Shith, Nuh, Hud, Swalih, Ibrahim, Lut, Ismail, Ishaq, Yaqub, Yusuf, Ayyub, Shuaib, Musa, Harun, Khidr, Yusha ibn Nun, Ilyas, Alyasa, Dhul-kifl, Shamun, Ishmoil, Yunus ibn Mata, Dawud, Sulaiman, Luqman, Zakariyya, Yahya, Uzair, Issa ibn Mariam, Dhul-qarnain** na **Muhammad** "swallallahu alaihi wa sallam".

Kati ya hao majina ya mitume ishirini na nane tuu yametajwa kwenye Quran tukufu. Shit, Khidr, Yusha’, Sham’un na Ishmoil hayajaandikwa. Miongoni mwa hao ishirini na nane haijulikani kama Dhul-qarnain, Luqman na Uzair walikuwa mitume au la. Imeandikwa kwenye **Maktubat-i-Ma’thumiyya** volume ya pili kwamba kuna dalili zinazosema kwamba Khidr "alaihis-salaam" alikuwa mtume. Na imeandikwa hivi kwenye barua ya mia moja na thamanin na mbili kama ifuatavyo: “Khidr "alaihis-salaam" yupo kwenye sura ya binaadamu mda wote na anafanya baadhi ya kazi, haionyeshi kwamba yuko hai. Allahu taala aliipa roho yake kama alivyozipa roho za mitume wengine na mawalii, ruhusa ya kuonekana katika sura ya binaadamu. Kuwaona sio ishara kwamba wako hai.” Dhul-kifl "alaihis-salaam" pia aliitwa Harqil, ndie anayesemekana pia kuwa Ilyas, Idris au Zakariyya.

Ibrahim "alaihis-salaam" ni Khalil-Allah, kwa sababu hakuwa na mapenzi ya viumbe katika moyo wake isipokuwa mapenzi ya Allahu taala peke yake. Musa "alaihis-salaam" ni Kalim-Allah, kwa sababu

alizungumza na Allahu taala. Issa "alaihis-salaam" ni Kalimat-Allah, yeye hakuwa na baba na alizaliwa kwa Kalimat al-ilahiyya (neno la Mungu) ‘kuwa’. Zaidi alihubiri maneno ya Allahu taala ambayo yalikuwa yenye hekima kubwa na akayafikisha kwenye masikio ya watu.

Muhammad "alaihis-salaam" ambaye ndie sababu ya kuumbwa kwa viumbe wote na mwenye cheo cha juu, ndie maarufu zaidi, mwenye heshima kubwa miongoni mwa binadamu, ni Habibu Allah (kipenzi cha Allahu taala). Kulikuwa na ushahidi mwingi kuthibitisha ukubwa wake na ndio maana akaitwa Habibu-Allah. Kwa sababu hii, maneno kama ‘kashindwa’ hayasemwi kwake. Katika siku ya kiama atafufuka kutoka kwenye kaburi lake kabla ya watu wote. Atakuwa wa mwanzo kwenda kuhukumiwa. Ataingia peponi kabla ya watu wote. Ingawa miujiza yake tukiihisabu haiishi, na kuihisabu nguvu za mtu hazitoshi, acha tuuandike muujiza wake wa Miraj kwa kupamba maandishi yetu.

Moja katika miujiza yake ni kwenda kwake **Miraj**: alipokuwa kitandani Makka al-Mukarramah, aliamshwa na mwili wake mtukufu ulipelekwa masjid ya Aqsa mji wa Jerusalem (Quds), na kuelekea mbinguni, na kuipita mbingu ya saba, kuelekea kwenye maeneo ambayo Allahu taala alikusudia. Tunapaswa kuamini Miraj hivyo.[1] Miraj ilitokea vipi imeandikwa kwa maelezo kwenye vitabu vyenye thamani vingi, hasa katika **Shifa’-sharif**.[2] Yeye na Jibril "alaihis-salaam" walikwenda kutoka Makka hadi **Sidrat al-muntaha**, mti uliopo kwenye mbingu ya sita na saba. Zaidi ya hapo hakuna ndio kikomo cha maarifa na kupanda juu. Hapo kwenye Sidra, mtume "alaihis-salaam" alimuona Jibril "alaihis-salaam" kwenye sura yake halisi akawa ana mbawa mia sita. Jibril "alaihis-salaam" alibaki kwenye Sidra. Kutoka Makka kwenda Jerusalem, na

---

[1] Wazushi wenye madhehebu ya Isma’ili na maadui wa Uislamu waliojificha kama wanazuoni wakiislamu, wanajaribu kuwadanganya vijana kwa kusema na kuandika kwamba Miraj mtume hakupanda kimwili lakini kiroho (kama ndoto). Tunafaa kutonunua vitabu hivi vyenye uongo. Tusiwape fursa ya kutudanganya.

[2] Qadi Iyad al-Maliki, mtunzi wa kitabu Shifa’, alifia Morocco mwaka 544 H. [1150 miladi].

kuelekea mbingu ya saba Rasulullah "alaihis-salaam" alipanda **Buraq**, ambaye ni mweupe, mwenye kasi sana, hana jinsia sio dume wala jike na ni mnyama asiekua wa hapa duniani lakini kutoka peponi, ni mkubwa kuliko nyumbu tena mdogo kuliko farasi. Anakanyaga pale macho yake yanapoishia kuona. Kwenye masjid ya Aqsa Rasulullah "alaihis-salaam" na mitume wengine walisali jamaat, mtume "alaihis-salaam" akawa imamu, ilikuwa sala ya usiku au alfajir. Roho za mitume zilikuwepo pale katika sura zao za kibinadamu. Kutoka Jerusalem kwenda mbingu ya saba alipanda kwa kutumia ngazi ziitwazo **Miraj**. Wakati yupo njiani Malaika walipiga foleni kulia na kushoto, wakiwa wanamsifu na kumtaja. Katika kila mbingu, Jibril "alaihis-salaam" alikuwa anatangaza habari njema za kufika kwa Rasulullah "alaihis-salaam". Katika Kila mbingu alimuona mtume na akamsalimia. Kwenye **Sidra**, aliona vitu vingi vya kushangaza, neema za peponi na adhabu za motoni. Kutokana na hamu kubwa ya kumuona Allahu taala, hakutizama kwenye neema za pepo. Baada ya Sidra alikwenda peke yake, katikati ya muangaza. Alisikia sauti za kalam za malaika wakiandika. Alipitia pazia elfu sabini. Umbali kati ya pazia mbili ulikuwa kama safari ya miaka mia tano. Baada ya hapa, kwenye kitanda kiitwacho **Rafraf**, ambacho kilikua kinang'aa kuliko jua, alipitia Kursi na akafika sehemu iliopo Arsh. Alikwenda mbali na Arsh, mbali na wakati, anga na masuala ya dunia. Alifika sehemu na kusikia mazungumzo yake Allahu taala.

Alimuona Allahu taala katika hali ambayo haieleweki wala haifafanuliki, kama Allahu taala atakavyoonwa siku ya kiama bila wakati wala anga. Alizungumza na Allahu taala bila herufi wala sauti. Akamtakasa, kumsifu na kumtaja Allahu taala. Alipewa zawadi zisizohisabika na heshima. Yeye na umma wake (Waislamu) waliamrishwa kusali sala hamsini kila siku. Hata hivyo sala za kila siku zilipunguzwa hadi tano kwa upatanishi wa Musa "alaihis-salaam". Kabla ya haya, namaz (sala) zilikuwa zinasaliwa katika wakati wa asubuhi na jioni au usiku tu. Baada ya safari ndefu kama hiyo, baada ya kuwa amepata zawadi na neema na kuona na kusikia vitu vya kushangaza vingi, alirudi kwenye kitanda chake ambacho kilikuwa bado hakijapoteza ujotojoto wake. Tuliofahamisha hapo juu sehemu moja tuliitoa kwenye aya tukufu na sehem nyingine kutoka kwenye hadithi. Hata sio wajibu kuamini vyote lakini

kulingana na mafundisho ya wanazuoni wa Ahl as-Sunna mtu anayekanusha ukweli huu anakuwa ametengana na Ahl as-Sunna. Na yule asieamini aya au hadithi anakuwa kafiri. Acha tuangalie baadhi ya ushahidi usiohisabika unaonyesha Muhammad "alaihis-salaam" kuwa yeye ni **Sayyidul-Ambiya’** wa mitume "alaihimus-salaam" wote.

Siku ya kiama mitume wote "alaihimus-salaam" watajikinga chini ya kivuli cha bwana wao. Allahu taala alimwambia kila mtume ‘alaihis-salaam’ kwamba wangekuwa wanaishi hadi wakati atakapochaguwa miongoni mwa viumbe kipenzi chake Muhammadi ‘alaihis-salaam’ wangestahiki kumuamini na kuwa wasaidizi wake. Vile vile kila mtume aliuambia uma wake hivyo.

Muhammad "alaihis-salaam" alikuwa **Khatam al-ambiya** (mtume wa mwisho); kwamba hakuna tena mtume atakae mrithi. Roho yake yenye kubarikiwa iliumbwa kabla ya mitume wote. Alipewa cheo cha nubuwwa (utume) mwanzo. Nubuwwa (utume) ulikamilishwa na kuja kwake kuipa dunia heshima. Wakati wa mwisho wa dunia ukikaribia, katika enzi za Hadhrat al Mahdi, Issa "alaihis-salaam" atateremka kutoka mbinguni kwenye mji wa Damascus (Syria) na kuungana na umma wa Muhammad "alaihis-salaam" na kutangaza Uislamu duniani. Watu wenye uzushi wanaoitwa **Qadiyani** au **Ahmadiyya**, ambao waliandaliwa na waingereza huko India mnamo mwaka wa 1296 hijri [1880 A.D], wamesema uongo na maneno maovu kuhusu Issa "alaihis-salaam". Ingawa wanajiita Waislamu, wanajitahidi sana kuuharibu Uislamu kwa ndani. Fatwa ilipita ya kuwabainisha kwamba sio Waislamu.

Kundi lengine la mazindik lenye uzushi ambalo lilijitokeza nchini India ni kundi la **Jama’atul-tablighiyya**. Kundi lao lilianzishwa mnamo mwaka 1345 [1926 A.D], na Ilyas. Alisema kwamba Waislamu walikuwa wamepoteza Uislamu wa kweli na ili kuwanusuru alipata amri kwenye ndoto. Alisema alipata mafunzo kutoka kwenye vitabu vya walimu wake ambao pia ni wazushi kama Nazir Huseyn, Rashid Ahmed Gangohi na Khalil Ahmad Saharanpuri. Njia wanayotumia kupoteza Waislamu ni kwamba kila wakati wanazungumzia umuhimu wa sala na jamat. Hali ya kuwa wenye uzushi (wasiofuata madhehebu ya Ahl as-Sunna) sala na ibada zao zengine hazikubaliwi. Wanafaa kusoma vitabu vilivyoandikwa na

wanazuoni wa Ahl as-Sunna wajiokoe kwenye bid'at kisha wawe Waislamu wa kweli. Watu wanaotafsiri vibaya aya za Quran tukufu ambazo hazina maana ya moja kwa moja wanaitwa wenye **bid'at** au **wazushi**. Maadui wa Uislamu wanaotafsiri aya za Quran tukufu kulingana na fikira zao potofu na wakatoa maana ambayo sio sahihi wanaitwa **Zindiq**. Mazindik hawa wanajaribu kubadilisha Quran tukufu na Uislamu. Adui mkubwa alieanzisha na kuwalea na kuwasambaza ulimwenguni kote na kuwapa mamilioni ya pesa ni muingereza. Wanachama wa **Jamat tabligh** kwa ujinga wao wameanguka kwenye mtego wa makafiri waingereza, wanajitahidi kuwadanganya Waislamu kwa kujiita **Ahl as-Sunna** na kusali kila siku sala tano na kusema uongo. Abdullah ibn Masud anasema kwamba, (ingawa hawana dini watakuwa wenye kusali). Watu hawa watakuwa ndani kabisa kwenye moto. Baadhi yao ni kama korongo alioko kwenye mnara juu ya mlima , ana kilemba kikubwa, ndevu na juba lake, wanasoma aya tukufu na wanatoa maana sio sahihi na wanapoteza Waislamu. Hata hivyo hadithi sharif inasema: **(Innallaha la yandhuru ila suwarikum wa thiyabikum walakin yandhuru ila kulubikum wa niyyatikum)**, Allahu taala hatizami sura zenu wala mavazi yenu lakini anatizama nyoyo zenu za niya zenu. Shairi:

***Kad-du buland dared, dester para, para.***
***Chun ashiyani laklak, ber kalla-i-minara.***

Kwakuwa watu hawa wameshindwa kujibu vitabu vinavyochapishwa na **Hakikat Kitabevi** ambavyo vinathibitisha kwamba watu hawa ni waongo, basi wanasema "Vitabu vinavyochapishwa na Hakikat Kitabevi ni vya uongo na uzushi. Msisome vitabu hivyo." Alama kubwa ya kuwatambuwa maadui wa Uislamu na mazindik ni kusema kwamba vitabu vilivyoandikwa na wanazuoni wa Ahl as-Sunna vinavyoeleza dini ya kweli ni vya uongo, na kuwaambia watu wasisome vitabu hivyo. Kitabu chetu **Faideli Bilgiler** (Habari muhimu) kimetoa maelezo zaidi kuhusu madhara ya watu hawa kwa Waislamu na majibu ya wanazuoni wa Ahl as-Sunna.

Muhammad "alaihis-salaam" ndie wa juu kabisa miongoni mwa mitume wote, ndie rehma ya ulimwengu. Ulimwengu elfu kumi na

nane wote wanafaidika kutoka kwenye bahari yake rehma. Kwa muungano wa wanazuoni walisema kwamba ni mtume wa watu wote na majini. Na kuna kauli nyingi zinazoeleza kwamba pia ni mtume wa Malaika, mimeya, wanyama na kila dutu. Mitume wengine walitumwa kwa umma fulani na nchi zao tu. Lakini Rasul karim "alaihis-salaam" alitumwa kwa ulimwengu wote, na viumbe wote walio hai na wasiokuwa hai. Allahu taala aliwataja mitume wengine kwa majina yao. Lakini Muhammad "alaihis-salaam" alimtaja kwa njia ya Ewe mjumbe wangu. Ewe mtume wangu wakati wa utume. Alioneshwa miujiza aliopewa kila mtume. Allahu taala alimpa zawadi nyingi na akampa miujiza mingi kuliko aliyowapa mitume wake wengine. Alifanywa kuwa wa juu ya mitume wote kwa kupewa heshima na ubora. Mwezi uligawika vipande viwili alipofanya ishara kua kidole chake chenye baraka; jiwe ndani ya mkono wake lilitamka jina la Allah; miti ilimsalimia kwa kusema, “Ya Rasullah”; mti mkavu unaoitwa Hannana ulilia kwa kuwa Rasulullah ameuwacha; maji yalitiririka kutoka kwenye vidole vyake vyenye baraka; vyeo vya juu vya **al-Maqam al-Mahmud, ash-Shafa’at al-kubra, al-Hawdh al-Kawthar, al-Wasila** na **al-Fadila** aliahidiwa kupewa vyote siku ya kiama; na alipata heshima ya kuona uzuri wake Allahu taala kabla ya kuingia peponi; alikuwa mwenye tabia nzuri duniani, mwenye imani iliokamili, mwenye elimu, mwenye upole, mwenye uvumilivu, mwenye shukrani, mwenye zuhdi, mwenye usafi wa moyo, mwenye uadilifu, mwenye ukarimu, mwenye hayaa, shujaa, mwenye adabu, mwenye hikma, mzuri wa tabia, mwenye kusaidia, mwenye huruma na heshima bila kikomo. Hakuna mtu anaejua miujiza aliopewa isipokuwa Allahu taala. Dini yake ya Uislamu ilifuta dini nyengine zote zilizomtangulia. Dini yake ndio bora zaidi na ya juu kuliko zote. Umma wake ni wa juu kuliko umma mwengine. Mawalii wa umma wake wanaheshimika kuliko mawalii wa umma mwengine.

Miongoni mwa maawliya wa umma wa Muhammad "alaihis-salaam", aliestahiki kuwa halifa wa kwanza **Abu Bakr as-Siddiq** "radiyallahu anhu", ndie aliependwa zaidi na maawliya na maimamu na ndie aliekuwa anafaa kuwa Khalifa kuliko wengine. Baada ya mitume, ndie anaefuata kuwa na cheo cha juu na bora zaidi miongoni mwa binadamu waliowahi kuishi na watakaokuja.

Ndie wa kwanza kupata cheo na heshima ya Khalifa. Kama neema na baraka kutoka kwa Allahu taala, hajawahi kuabudu masanamu kabla ya Uislamu kuja. Alilindwa dhidi ya ukafiri na tabia za kijinga. [Kutokana na haya inafahamika jinsi gani walivyo wajinga na duni wale wanaoandika na kusema kwamba Rasulullah "alaihis-salaam" aliwahi kuabudu masanamu kabla ya utume.] Baada ya huyu anayefuata kuwa na cheo cha juu miongoni mwa binadamu ni Khalifa wa pili **Umar ibn al-Khattab** "radiyallahu anhu" ambaye Allahu taala alimchaguwa kuwa rafiki wa karibu wa mpendwa wake mtume. Baada ya huyu anayefuata kuwa na cheo cha juu miongoni mwa binadamu ni Khalifa wa mtume "alaihis-salaam" wa tatu **Dhu´nurain Uthman ibn Affan** "radiyallahu anhu", hazina ya neema na baraka na chimbuko la hayaa, imani na maarifa ya kiroho.

Baada ya yeye, anafuata mtu bora sana ndani ya watu na ni Khalifa wa mtume "alaihis-salaam" wa nne **Ali ibn Abi Talib** "radiyallahu anhu", mwenye nguvu za kutisha na ndie simba wa Allahu taala. Hadhrat **Hasan ibn Ali** "radiyallahu anhu"[1] alikuwa Khalifa baada yake. Mda wa miaka thelathini ya khilafat iliotajwa na hadithi sharif ilikamilishwa na yeye. Baada yake mtu mwengine wa juu ni Hadhrat **Huseyn ibn Ali** "radiyallahu anhu", mwangaza wa macho yake Rasulullah "alaihis-salaam".

Ubora huu ulitokana na wingi wa thawabu mtu alizokusanya, kuachana na makazi yao na wapendwa wao kwa ajili ya Uislamu, kutangulia kwenye Uislamu, kuwa karibu na mtume "alaihis-salaam", kwa hali ya juu; kutekeleza sunna za mtume; jitihada zao kwenye kusambaza Uislamu; na kuepuka ukafiri, fitina na ufisadi.

Hadhrat Ali "radiyallahu anhu" alikubali Uislamu kabla ya masahaba wote isipokuwa Abu Bakr "radiyallahu anhu". Lakini alikuwa bado mtoto na hakuwa na mali na alikuwa anaishi kwenye nyumba ya Mtume "alaihis-salaam" na kumtumikia. Kwa hivyo kukubali kwake Uislamu hakujafanya makafiri kukubali Uislamu, ili kufuata mfano wake, au kushindwa. Kwa upande mwengine, kukubali Uislamu kwa makhalifa watatu wengine kuliufanya Uislamu kupata nguvu. Kwa kuwa Hadhrat Ali na wanawe

[1] Hasan bin Ali alikufa kwa sumu mnamo mwaka 49 [669 A.D] kwenye mji wa Madina al-Munawara.

"radiyallahu anhum" walikuwa karibu sana na mtume "alaihis-salaam" kiudugu na damu, wangesemwa kuwa wenye cheo cha juu kuliko Hadhrat Abu Bakr na Hadhrat Umar, lakini ubora wao haukuwa ubora katika kila nyanja na haukuwasaidia kuwapita watu wakubwa hawa kwa njia yoyote. Ilikuwa kama Khidr "alaihis-salaam" kumfundisha Musa "alaihis-salaam" baadhi ya vitu. [Ingekuwa tunazingatia ukaribu kidamu kwa ubora wa mtu basi Hadhrat Abbas angekuwa mbora zaidi kuliko Hadhrat Ali. Waliokaribu kidamu Abu Talib na Abu Lahab wao kiheshima wako chini ya waumini wote na hawana ubora wowote.]

Hadhrat **Fatima** alikuwa na cheo cha juu kuliko Hadhrat **Khadija** Hadhrat **Aisha** "radiyallahu anhunne" kwasababu alikuwa karibu sana na mtume kidamu. Lakini ubora wa namna nyengine hauoneshi ubora wa kila namna. Wanazuoni wetu walisema kauli tofauti tofauti kuhusu watatu hawa ni yupi ambaye yuko juu. Kama ilivyofahamika kwenye hadithi tukufu, hawa watatu, Hadhrat **Mariam** na mke wake Firauni Hadhrat **Asiya**, ni wenye vyeo vya juu miongoni mwa wanawake duniani. Na hadithi tukufu nyengine inasema: **“Fatima ni mbora zaidi miongoni mwa wanawake walioko peponi, na Hasan na Huseyn ni vijana wa juu peponi,”**

Baada ya hawa, miongoni mwa maswahaba waliobora zaidi ni **al-Asharat al-Mubasshara**, yaani kumi waliobashiriwa pepo wakati wapo hai. Baada ya hawa ni mia tatu kumi na tatu (313) walioshiriki kwenye vita vya Badri. Wanaofuata ni mashujaa mia saba (700) walioshiriki kwenye vita vya Uhud. Baada ya hawa ni wale elfu moja mia nne (1400) wanaojulikana kama **Bi’at ar-Riddwan**, walioapa kuungana naye Rasulullah "alaihis-salaam" chini ya mti.

Maswahaba "radiyallahu anhu" walijitolea kwa uhai wao na mali zao kwa ajili ya Rasulullah "alaihis-salaam" na kumsaidia. Ni wajibu kwetu tunapotaja jina la mmoja wao, kulitaja kwa upendo na heshima. Hairuhusiwi kusema maneno yanayopunguza ukubwa wao. Ni uzushi yaani bid’a kutaja majina yao bila heshima.

Yule anayempenda Rasulullah "alaihis-salaam" ni lazima kuwapenda masahaba wake wote. Hadithi tukufu inasema: **“Anayewapenda masahaba wangu anawapenda wote kwasababu ananipenda mimi. Asiewapenda hanipendi. Anayewaumiza ananiumiza. Tena anayeniumiza anamuumiza Allahu taala. Mtu anayemuumiza Allahu taala bila shaka**

**ataadhibiwa."** Katika hadithi tukufu nyengine mtume alisema: **"Allahu taala anapotaka kumbariki mmoja katika umma wangu, anatia moyoni mwake mapenzi ya masahaba wangu, na akawapenda wote."**

Kwa hivyo, isitazamwe kwamba masahaba walipigana wao kwa wao kwa ajili ya ukhalifa au kwa nia zao mbaya au kwa tamaa zao. Ni unafiki mkubwa unaosababisha mmoja kuwasema vibaya kutokana na dhana kama hizo, hali ya kuwa wivu na tamaa ya cheo na kupenda dunia ilikuwa ishafutwa kabisa kwenye nyoyo zao baada ya kukaa na mtume "alaihis-salaam" na kusikiliza maneno yake yenye baraka. Walirekebishwa na kuwa huru kutokana na uchoyo, matamanio, chuki na nia mbaya, walikuwa safi kabisa. Kuzingatia ukweli kwamba mtu anayekaa siku chache mbele ya mmoja kati ya mawalii wa umma huu wa mtume aliyetukuka anafaidika kutoka kwa walii huyu kwa tabia nzuri na ubora na anakuwa msafi kutokana na matamanio ya dunia, inakuwaje ikadhaniwa kwamba masahaba wa mtume, ambao ni mabwana wetu, waliompenda mtume kuliko mtu mwengine yoyote na wakatoa mali zao na uhai kwa ajili yake na wakaacha nchi zao kwa ajili yake na wakazoea urafiki wake, ambao ulikuwa ni chakula cha moyo, hawakuwa huru dhidi ya tabia mbaya, nafsi zao hazikuwa safi na kwamba walipigana kwa ajili ya mzoga huu kama maisha ya mda tu? Watu wakubwa hao walikuwa wasafi sana kuliko mtu mwengine. Sio haki kufananisha kutoelewana kwao na kupingana kati yao na masuala yanayotokea miongoni mwetu, watu wenye uhasama au kusema kwamba walipigana kutosheleza ubaya wao, hisia na tamaa za kidunia. Hairuhusiwi kuwa na dhana mbaya kama hiyo dhidi ya masahaba. Mtu anayesema kitu chochote dhidi yao anapaswa kujuwa kwamba kuwa na uadui na masahaba ni sawa na kuwa na uadui na mtume "swallallahu alaihi wa sallam", na kusema maovu juu yao ni sawa na kusema maovu juu yake, ambaye aliwafundisha na kuwapa mafunzo. Kwa sababu hii, watu wakubwa Waislamu wanasema kwamba asiyeheshimu na asiyetambua ukubwa wa masahaba hajamuamini mtume wa Allah bado. Hatuwezi kutumia vita vya "Jamal" na "Siffin" kama chanzo cha kuwakashifu. Kwa sababu za kidini, hakuna sahaba aliesimama dhidi ya Ali "radiyallahu anhu" katika vita hivyo mwenye makosa; wote wanasitahiki kulipwa kwenye siku ya kiama. Hadithi tukufu

inasema: **“thawabu moja itapewa mujitahidi mwenye kukosea, na mbili au kumi kwa yule ambaye anasawazisha. Moja kati ya thawabu mbili ni ya kufanya jitihada. Na nyengine ni ya kusawazisha na kupata ukweli.”** Migogoro na mapambano miongoni mwa watu wakubwa Waislamu hawa haikuwa ukaidi au uadui lakini kutokana na tofauti zao katika ijtihad, matumaini yao ya kuendeleza yale yanayoamrishwa na Uislamu. Kila sahaba alikuwa mujtahid.[1]

Ilikuwa wajibu kwa kila mujtahid kutekeleza kulingana na matokeo aliopata wakati wa ijtihada yake, hata ikiwa matokeo ya ijtihadi yake hayalingani na ya mujtahidi alioko juu yake. Ilikuwa hairuhusiwi kufuata ijtihad ya mwengine. Abu Yusuf na Muhammad Shaybani, wanafunzi wa al-Imam al-A’zam Abu Hanifa Nu’man ibn Thabit (alikufa 150 [767 A.D, kwenye mji wa Baghdad]), na Abu Thawr na Ismail ibn Yahya al-Muzani ambao ni wanafunzi wa Imam Muhammad ibn Idris al-Shafi’i (alikufa 204 [820 A.D, Misr]) katika masuala mengi hawajakubaliana na walimu wao, na kuhusu mambo mengine walimu wao walioyataja kuwa ‘halali’ wao walisema ‘haram’ na mengine walimu waliotaja kuwa ‘haram’ wao wakasema ni ‘halali’. Kutokana nayo hawawezi kusemwa kwamba walifanya kosa au ni wabaya.

Na hakuna aliyesema hivyo. Kwasababu nao ni mujtahid kama walivyokuwa walimu wao.

Ni kweli kwamba Hadhrat Ali "radiyallahu anhu" alikuwa wa juu na kujifunza zaidi kuliko Hadhrat Mu’awiya na Hadhrat Amr ibn al-As "radiyallahu anhu". Alikua na sifa nyingi za juu zinazomtofautisha nao, na ijtihad yake ilikuwa na nguvu na umakini zaidi kuliko ijtihad zao. Hata hivyo, kwa kuwa masahaba wote walikua mujtahid, ilikuwa hairuhusiwi kwao kufuata ijtihadi ya kiongozi wa dini mkubwa huyu. Ilifaa kwao kutenda kulingana na ijtihadi zao.

**Swali:** “katika vita vya ‘Jamal’ na Siffin’ idadi kubwa ya Muhajirun na Ansar miongoni mwa masahaba walishiriki, walimtii

[1] Kwamfano kwenye Hadithi sharif kwenye ukurasa wa 298 wa kitabu al-Hadiqa inaeleza kwamba ‘Amr ibn al-As "radiyallahu anhu" alikuwa mujtahid.

na kumfuata Ali. Ingawa wote walikuwa mujtahid, walifikiria kuwa ni wajibu kumfuata Imam Ali. Hii inatuonyesha kwamba ilikuwa wajibu pia kumfuata Imam Ali. Walifaa kumfuata japokuwa ijtihad zao zilikuwa hazikubaliani na yeye, sio?

**Jawabu:** Waislamu waliomfuata Imam Ali na wakapigana pamoja naye waliungana naye sio kwamba walifuata ijtihad yake lakini kwa sababu matokeo ya ijtihadi zao ndio yalikubaliana na ya Imam Ali na ikaonyesha kwamba ilikuwa wajibu kumfuata Imam Ali. Vile vile, ijtihadi za masahaba wa mtume wakubwa wengi hazikukubaliana na Hadhrat Ali na ikawa wajibu kupigana dhidi yake. Ijtihadi za masahaba zilitokea kwenye njia tatu tofauti: Baadhi yao walifahamu kwamba Ali "radiyallahu anhu" alikua ni sahihi, na ikawa wajibu kwao kumfuata Ali "radiyallahu anhu". Kundi lengine wakaona kwamba ijtihadi ya wale waliopigana dhidi ya Ali ni sahihi, na ikawa wajibu kwao kuwafuata waliopigana dhidi ya Ali "radiyallahu anhu". Kundi la tatu waliona haifai kuunga mkono mmoja kati yao na kuamua kutopigana, na ijtihadi yao iliwaambia kutoingia kwenye vita. Makundi yote matatu haya walikuwa sahihi na walipewa thawabu.

**Swali:** Kutokana na maandishi hapo juu inaonesha kwamba wale waliopigana dhidi ya Imam Ali "radiyallahu anhu" pia walikuwa sahihi. Kwa upande mwengine, baadhi ya wanazuoni wa Ahl as-Sunna walisema kwamba Ali "radiyallahu anhu" alikuwa sahihi, na wapinzani wake walikosea, na walisamehewa au walipata thawabu kwa sababu walikuwa na ‘udhr’. Inazungumzwaje kuhusu hili?

**Jawabu:** Watu wakubwa wawili ndani ya Uislam Al-Imam Shafi’i na Umar ibn Abd al-Aziz walisema kwamba hairuhusiwi kusema kwamba masahaba walikosea. Kwa sababu hii, waliamrisha kwamba kusema kwamba wakubwa wamekosea ni kosa. Hairuhusiwi kwa wadogo kutoa hukumu juu ya wakubwa kama amefanya sahihi, amekosea, tunakubali, hatukubali. Kwa kuwa Allahu taala hakupaka mikono yetu damu ya watu wakubwa hao, inabidi tuzilinde ndimi zetu kwa kutamka maneno kama ‘alikuwa na haki’ na ‘hakuwa na haki’. Wanazuoni wa kina waliosoma ushahidi na matukio na kusema kwamba Imam Ali "radiyallahu anhu" alikuwa sahihi (alikuwa na haki) na wapinzani wake hawakuwa na

haki (walikosea), kwa kweli walikusudia kwamba laiti Imam Ali angepata fursa ya kuzungumza nao waliokuwa kwenye upande mwingine, angewaongoza kutumia ijtihadi kwa kulinganisha na ijtihadi yake. Kusema kweli, az-Zubayr ibn al-Awam "radiyallahu anhu" alikuwa dhidi ya Ali "radiyallahu anhu" katika vita vya 'Jamal' lakini baada ya kufikiria kwa kina kwenye matukio alibadilisha ijtihadi na kuacha mapigano. Maneno ya wanazuoni wa Ahl as-Sunna wanaochukulia kosa kama ruhusa basi wanafaa kuchukuliwa hivyo. Na hairuhusiwi kusema kwamba Ali "radiyallahu anhu" na wale walioungana naye walikuwa kwenye ukweli na wale waliokuwa dhidi yao kwenye kundi la mama yetu Aisha al-siddiqa, walikuwa kwenye njia batili.

Mapambano ya masahaba haya yalitokana na kutofautiana kwa ijtihadi kwenye matawi ya Ahkam as-Shar'iyya (hukumu za sheria ya kiislamu). Hawakutofautiana kwenye misingi ya Uislamu. Leo, baadhi ya watu wanawasema vibaya na kutowaheshimu watu wakubwa wa Uislamu kama Mu'awiya na Amr ibn al-As "radiyallahu anhu". Hawajui kwamba kwa kuwakashifu na kuwadhalilisha masahaba ni kumkashifu na kumdhalilisha mtume "swallallahu alaihi wa sallam". Imeandikwa kwenye Shifa as-sharif kwamba Imam Malik ibn Enes alisema "Mtu anayeapa na kuwakashifu Mu'awiya[1] na Amr ibn al-As[2] anastahiki maneno aliosema dhidi yao kumrudia. Inafaa kuwaadhibu vikali hao wanaosema na kuandika dhidi yao na kutoonesha heshima juu yao". Tunamuomba Allahu taala ajaze nyoyo zetu mapenzi ya masahaba wake. Watu wenye imani ya kweli na wanaomuogopa Allahu taala wanawapenda mashujaa hao lakini wanafiki na wenye madhambi hawawapendi.

Watu wanaotambua umuhimu na ukubwa wa masahaba wa mtume "swallallahu alaihi wa sallam" na wanaowapenda na kuwaheshimu wote na kuwafuata wanaitwa Ahl as-Sunna. Wale wanaodai kuwapenda baadhi yao na kuwachukia wengine na kuwakashifu wengi wao, na wale wasiokuwa wafuasi wao

---

[1] Hadrat Muawiya ibn Abu Sufyan alikufa mnamo mwaka wa 60 [680 A.D] kwenye mji wa Damascus.

[2] Amr Ibn al-As alikufa mwaka wa 43 [633 A.D] nchini Misr.

wanaitwa Shia (mashia) na Rawafiz. Iran, India na Iraq Rawafizi ni wengi. Uturuki hakuna hata mmoja. Baadhi ya hawa Rawafiz, ili kuwapoteza Waislamu wa kweli wa Alawi (wanaopatikana Uturuki) na wao wanajiita Alawi. Hali ya kua Alawi maana yake ni Waislamu wanaompenda Ali "radiyallahu anhu". Kumpenda mtu ni lazima kufuata nyayo zake na kuwapenda wale aliowapenda.

Hawa wangekuwa wanampenda Ali "radiyallahu anhu" wangefuata nyayo zake. Aliwapenda masahaba wa mtume wote. Alikuwa mshauri wake Khalifa Umar "radiyallahu anhu" ambaye ni Khalifa wa pili. Alimuozesha Umar "radiyallahu anhu" mwanawe na bi Fatima Umm Kuluthum. Kwenye hotuba, alisema kuhusu Mu'awiya "ndugu zetu hawakukubaliana nasi. Lakini sio makafiri wala wenye madhambi. Ijtihad yao iliwambia kufanya vile." Talha "radiyallahu anhu" aliepigana dhidi yake alipokufa, yeye mwenyewe alimsafisha vumbi kwenye uso wake na akawa imam wakati wa kumsalia baada ya kifo chake. Allahu taala anasema: **"Waumini wote ni ndugu."** Na aya ya mwisho kwenye sura al-Fatihah Inasema: **"Masahaba wa mtume wanapendana."** Kutompenda hata mmoja kati ya masahaba wa mtume na kujenga uadui juu yake, ni kukanusha Quran tukufu. Wanazuoni wa Ahl as-Sunna walifahamu ukubwa wa masahaba "radiyallahu anhum" kiukweli na kuamrisha Waislamu kuwapenda wote ili kuokolewa kutoka kwenye hatari.

Watu waliowachukia na kuwatendea uadui Ahlul bayt yaani Ali "radiyallahu anhu" na wanawe na kizazi chake ambao wanapendwa sana na Waislamu wakisunni wanaitwa **Khawarij**. Leo hawa makhawarij wanaitwa Yazidiyya. **Yazidiyya** dini yao na imani zao ni potofu.

Wanaosema sisi masahaba wote tunawapenda halafu badala ya kufuata nyayo zao wakafuata fikira zao potofu na kusema kwamba njia ya masahaba ndio hii wanaitwa **Wahhabiyya**. Uwahabi wanatumia fikira potofu zilizomo kwenye vitabu vilivyoandikwa na Ahmed ibn Taymiyya ambaye hana madhehebu na Hempher jasusi wa uingereza. Mawahabi hawawataki wanazuoni wa Ahl as-Sunna, wasufi wakubwa na mashie, wote wanawaona wabaya. Wanadhani wao pekee ndio Waislamu. Wasiokuwa kama wao wanasema ni washirikina. Wanasema mali zao na uhai wao ni halali. Inakuwa

(Ibaha). Kwenye nassi yaani Quran tukufu na Hadithi sharif wanatoa tafsiri ya uongo, mbovu na wanadhani kwamba tafsiri sahihi kwa Uislamu ndio hii. Wanakanusha Adillatu-shar'iyya pamoja na hadithi nyingi. Wanazuoni wa madhehebu manne waliandika vitabu vingi kuhakikisha kwa kutoa ushahidi kwamba wale wanaotengana na Ahl as-Sunna wamepotea na wana madhara makubwa kwa Uislamu. Kupata maelezo zaidi, soma vitabu kama: **kwa lugha ya kituruki**, **Kiyamet ve Ahiret, Se'adet-i Ebediyye** kwa lugha ya kiarabu, **Mihna-tulwahbiyya**, **At-Tawassul-u bin-Nabi wa bis-Salihin**, **Sabil-unnajat** na Kiajemi **Seyf-ul-abrar**. Vitabu hivi viliandikwa na kujibu wenye uzushi, vitabu vingi muhimu vilichapishwa Istanbul na (Hakikat Kitabevi). Ibn Abidin (Muhammad Emin ibn Abidin) alikufa mwaka wa 1252 [1836 M] Sham (Syria) kwenye kitabu chake volume ya tatu wakati anaelezea 'Baghi' na kwa Kituruki **(Ni'met-i islam)** mlango wa "Nikah", ameweka wazi kwamba mawahabi ni Ibahi. Sultan Abdulhamid han wa pili mmoja kati ya ofisa wake Ayyub Sabri Pasha[1] katika vitabu vyake **(Mir'at-ul haramain)** na **(Tarihi wahhabiyyun)** na Ahmad Jawdat pasha tarihi yake kwenye volume ya saba, kwa kituruki kimeelezea kuhusu mawahabi kwa urefu. Yusuf Nabhan naye kwenye kitabu chake cha kiarabu **(Shawahidulhakk)** amewajibu mawahabi na Ibn Taymiyya kwa urefu. Kurasa hamsini kutoka kwenye kitabu chake zipo kwenye kitabu chetu **(Islam alimleri ve vahhabiler)** wanazuoni wakiislamu na mawahabi (Istanbul, 1972).

Ayyub Sabri Pasha "rahmatullahi alaih" alisema: "Uwahabi ulijitokeza pamoja na umwagaji damu, mateso na uasi wa vitisho katika Peninsula ya Uarabu mnamo mwaka 1205 [1791 A.D]." Muhammad Abduh wa Egypt (Misr) alikuwa mmoja wa watu waliojaribu kueneza Uwahabi na wasiokuwa na madhehebu kupitia vitabu vyake kote duniani. Wakati wa chama cha muungano na maendeleo, vitabu vya Abdu vilitafsiriwa kwa lugha ya Kituruki na vilizawadiwa vijana kama kazi ya mwanazuoni wa kiislamu mkuu, mwenye fikira za kimaendeleo, mujaddid maarufu 'Abduh'. Hata hivyo, Abduh alikuwa keshaandika wazi kwamba anavutiwa na Jamal ad-Din al-Afghani (aliekufa mwaka 1314 H. [1897 A.D]), ambaye alikuwa mmasoni na alikuwa mkuu wa Cairo Masonic

[1] Ayyub Sabri Pasha alikufa mwaka 1308 [1890 M].

Lodge. Maadui wa Uislamu, ambao walitaka kuifuta njia ya ukweli inayoitwa Ahl as-Sunna na baadae kuangamiza Uislamu kwa kutumia sifa za unafiki kwenye Uislamu, na kutengeneza njama za fitina kwa kujiita watu wa dini. Abduh alipongezwa hadi mbinguni. Wanazuoni wakubwa wa Ahl as-Sunna, a'immat al-madhahib, walitangazwa kuwa wamekuwa watu wajinga. Majina yao yalikuwa hayatajwi tena. Lakini vizazi vya kweli vya babu zetu, ambao walijitolea uhai wao kwa ajili ya mtume "swallallahu alaihi wa sallam" na Uislamu, watoto wa mashahidi, wasingedanganywa na matangazo pamoja na propaganda ambayo mamilioni ya fedha zimetumika. Hata wasingesikiliza au kutambua 'mashujaa wa Uislamu' wa uongo hawa. Allahu taala aliwalinda watoto wa mashahidi dhidi ya uvamizi huu wa kikatili. Leo, vitabu vya watu wasiokuwa na madhehebu vilivyotafsiriwa kama Mawdudi[1], Sayyid Qutb[2], kundi liitwalo 'Jama'at Tablighi' na Hamidullah vinapewa vijana.

Vitabu hivyo vina fikira potofu zinazopingana na mafundisho ya wanazuoni wa Ahl as-Sunna na fikira hizo wanazitolea matangazo makubwa. Tunafaa kuwa tayari na makini. Tunamuomba Allahu taala kuwaamsha Waislamu kutokana na kughafilika kwa neema za mtume wake Muhammad "alaihis-salaam" na tunamuomba atulinde dhidi ya kudanganywa na uongo na masingizio ya maadui, Amin. Tusijidanganye wenyewe kwa kuomba tu! Kuomba bila kufuata Adat al-ilahiyya (maagizo ya Allahu taala), bila kuweka sababu, bila kutenda ni kuomba miujiza kutoka kwa Allahu taala. Muislamu anapaswa kuomba na kutenda. Ni lazima tuweke sababu kwanza halafu tuombe. Njia ya kwanza kukuwezesha kujikomboa kutoka kwenye ukafiri ni kusoma Uislamu na kuufundisha. Ukweli wa mambo ni lazima kwa kila mwanamme na mwanamke kupata mafunzo kuhusu itikadi ya Ahl as-Sunna, anayowajibika kufanya na yalio haramu kwake. Hii ndio kazi ya kwanza. Leo, kupata mafunzo hayo ni wepesi tu. Kwa sababu kuna uhuru wa kuandika na

---

[1] Mawdudi ndio muanzilishi wa kundi la Jama'atul-islamiyya. Alikufa mwaka 1399.

[2] Sayyid Qutb alinyongwa mwaka 1386 [1966 M] nchini Misr.

kuchapisha vitabu vya dini sahihi. Ni lazima kila Muislamu kusaidia serikali ambayo imewapa Waislamu uhuru huu.

Watu wasiosoma itikadi na ilm al-hal ya Ahl as-Sunna na wasioelimisha watoto wao, wako kwenye hatari kubwa ya kujitenga na Uislamu na kutumbukia kwenye janga la ukafiri. Dua za watu kama hawa hazikubaliwi, hivyo watawezaje kulindwa dhidi ya ukafiri. Mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alisema: **“mahali penye elimu Uislamu upo. Mahali pasipo patikana elimu Uislamu haupo.”** Kama ilivyo muhimu kwetu kula na kunywa ili kutokufa njaa, vile vile ni muhimu kupata elimu kuhusu dini yetu ili kutodanganywa na makafiri na kutokuwa Waislamu. Mababu zetu mara kwa mara walikuwa wanakusanyika na kusoma vitabu vya ‘ilm al-hal na kwa hivyo walibaki kuwa Waislamu na wakafurahia Uislamu, na kwa njia hii waliweza kufikisha mwangaza wa neema kwetu sisi. Kwa hiyo ili kubaki Waislamu na watoto wetu kutodanganywa na maadui wa ndani au nje, jambo la kwanza na muhimu kufanywa ni kusoma na kujifunza vitabu vya ‘İlm al-hal’ vilivyoandaliwa na wanazuoni wa Ahl as-Sunna. Wazazi wanaopenda watoto wao kuwa Waislamu ni lazima kuwapeleka kwa mwalimu kuwafundisha kusoma Quran tukufu. Hebu tusome, tujifunze na tuwafundishe watoto wetu na wale ambao tunawajibika juu yao wakati nafasi bado ipo. Itakuwa vigumu pengine haitowezekana kwao pale watakapokwenda shule. Janga litakapokuja kuomboleza hakutokuwa na faida. Tusiwaamini maadui wa Uislamu, kwa udanganyifu wao na vitabu vyao vyenye uongo, magazeti, majarida, runinga (television) na vipindi vya radio, filamu na tovuti. Ibn Abidin "rahmatullahi alaih" aliandika katika kitabu **Radd al-muhtar** juzuu ya tatu kwamba wale makafiri ambao licha ya kutoamini dini yoyote, wanajifanya kuwa Waislamu na kufundisha vitu vinavyomfanya mtu kuwa kafiri kana kwamba ni vya kiislamu, na wanaojitahidi kuwapoteza Waislamu na kuwaongoza kwenda nje ya Uislamu wanaitwa **Mazindiq**.

**Swali:** Mtu anayesoma tafsiri ilioandikwa kwenye vitabu vibaya vya wasiokuwa na madhehebu anasema kwamba: Ni lazima tusome tafsiri ya Quran tukufu. Kazi ya kujifunza dini yetu na Quran tukufu kuikabidhi wanazuoni ni hatari na fikira ya kutisha. Quran tukufu haisemi “Enyi wanazuoni.” Lakini inasema, “Enyi Waislamu” na “Enyi watu.” Kwasababu hii, kila Muislamu ni lazima kuielewa

Quran tukufu mwenyewe na asitarajie jukumu hili kutoka kwa mwengine.” “Mtu huyu anataka kila mtu kusoma vitabu vya tafsiri na hadithi. Hatowi mapendekezo ya kusoma vitabu vya Kalam, Fiqh na ilm al-hal vilivyoandikwa na wanazuoni wa kiislamu na wanazuoni wakubwa wa Ahl as-Sunna. Katika kitabu cha Rashid Ridha[1] **Islamda Birlik ve Fikh Mezhebleri** kilichochapishwa na ofisi ya mkuu wa masuala ya dini (nambari 157;1394/1974) kinachanganya sana wasomaji. Sehemu nyingi katika kitabu hiki, mfano kwenye “mazungumzo ya sita” anasema kwamba:

“Hawa (mukallid wanaofuata moja kati yamadhehebu manne) wanawataja kina imamu mujitahdiina hadi daraja la mitume "alaihis-salaam". Na wanapendelea kauli za mujtahidi ambaye hata hafuati hadithi za mtume na kuacha hadithi za mtume. Wanasema kwamba hadithi huenda ikawa ilifutwa (naskh) au imamu huyu huenda akawa ametumia hadithi nyingine. Kwa kufuata maneno ya watu hao ambao wanaweza kuwa walikosea katika hukumu yao na huenda wakawa hawajafahamu jambo, na kwa kuiweka hadithi ya mtume upande yaani kuiacha, ambaye hakuwa na kosa lolote, mukallid hawa pia wanakwenda kinyume na mujtahdiin. Na kwa kufanya hivyo wanakwenda kinyume na Quran pia. Wanasema kwamba hakuna mtu anayeifahamu Quran isipokuwa mujtahid. Maneno kama haya mafakih na mukallid wengine inaonyesha kwamba yametolewa kwenye uyahudi au ukiristu. Kinyume chake ni rahisi sana kufahamu Quran na hadithi kuliko kufahamu vitabu vilivyoandikwa na watu wa fiqh. Watu waliosoma kiarabu na nahau hawatopata ugumu katika kufahamu Quran na hadithi. Nani hapa duniani anayekanusha ukweli kwamba Allah ana uwezo wa kuafanuwa dini yake kwa urahisi? Nani anayepinga ukweli kwamba mtume "alaihis-salaam" alikuwa mwenye uwezo zaidi kuliko mtu yoyote kufahamu makusudio ya Allah na kuweza kuwafafanulia watu kuliko wengine? Kwa kusema maelezo ya mtume hayakutosha kwa Waislamu ni kudai kwamba hakuweza kutekeleza kazi yake ya utume kiukamilifu.

[1] Rashid Rida ni mwanafunzi wa Muhammad Abduh. Alikufa mnamo mwaka wa 1354 [1939 A.D.].

Kama watu walio wengi hawajaweza kufahamu Quran na Sunna, Allah asinge wahukumu watu wote kwa kutumia sheria ndani ya kitabu na sunna. Ni lazima mtu ajue kile anachoamini kwa kutumia dalili. Allah anayakataa mambo ya taklid na anasema kwamba kwa kuiga baba na babu zao haitokuwa udhuru kusamehewa. Aya nyingi zinaonyesha kwamba taqlidi haijakubaliwa na Allah. Ni rahisi sana kufahamu kile kipande cha dini kinachohusiana na tawi kutoka kwenye dalili kuliko kipande kinachohusiana na imani. Wakati analazimisha kufanya yalio magumu je itakuwaje kwa mepesi? Itakuwa vigumu kuweka sheria kutoka kwenye mambo ambayo ni nadra, halafu tena itachukuliwa kuwa udhuru kwa kutojua au kutoyatekeleza. Watu wa fiqh walivumbua mas'ala mengi wenyewe. Walitoa sheria ya mas'ala hayo. Walijaribu kuanzisha vitu kama ra'y, qiyas jali na qiyas khafi kama dalili kwao. Vitu hivi vilifanywa kufurikwa katika nyanja ya 'ibadat, hali ya kua ni vigumu kupata elimu kwa kuhoji. Hivyo walipanua dini kwa mara kadhaa. Waliwatia Waislamu kwenye matatizo. Mimi sikanushi qiyas, nasema kwamba katika nyanja ya ibada hakuna qiyas. Yanayohusiana na Imani na ibada yalikamilishwa kwenye enzi za mtume. Hakuna anayeweza kuongeza chochote kwa hayo. Maulamaa (mujtahdiin) walikataza watu kuiga (taqlid) na wakaifanya taqlid kuwa haramu. Maandishi ya hapo juu tuliotoa kwa muhtasari ni kutoka kwenye kitabu (İslamda Birlik ve Fikh Mezhebleri) cha Rashid Ridha asiekuwa na madhehebu. Kama ilivyo kwa vitabu vya watu wasio na madhehebu, wanakataza watu kuiga maimamu wa madhehebu manne. Wanaamrisha kila mtu kujifunza tafsiri na hadithi. Unasemaje kuhusu hili?

**Jawabu:** Ikiwa vifungu vinavyoandikwa na watu wasio na madhehebu vimesomwa kwa uangalifu, unaweza kujua kwamba wanajaribu kuwadanganya Waislamu kwa kupamba fikira zao potofu na za kutenganisha kwa kutumia hoja mbali mbali na kauli za uongo. Wajinga wanaofikiri kwamba maandishi hayo yameandikwa kutokana na elimu kwa kutumia mantiki au hoja, wanaweza kuanguka kwenye mtego, lakini wale wenye elimu, walio makini hawatoweza kukamatwa kwenye mitego yao. Ili kuwaonya vijana dhidi ya hatari ya watu wasio na madhehebu au maadui wa Ahl as-Sunna, ambao wamekuwa wanawaendesha Waislamu kuwaelekeza kwenye kupotea kwa milele, wanazuoni wa kiislam

"rahmatullahi alaihim" wameandika maelfu ya vitabu vyenye thamani kwa karne kumi na nne. Yafuatayo ni tafsiri ya baadhi ya vifungu kutoka kwenye kitabu **Hujjat-Allahi 'ala-l-alamin** kilichoandikwa na Yusuf an-Nabhani (alikufa mwaka 1350 A.H [1932 M] Beirut) kama jibu kwa swali hapo juu "Sio kila mtu anaweza kuchambua ahkam (sheria) kutoka kwenye Quran tukufu. Kwa kua hata maimamu mujitahidiin hawakuweza kuchambua sheria zote kutoka kwenye Quran tukufu, mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alifafanua sheria zilizo kwenye Quran tukufu kwa kutumia hadithi sharif. Kama Quran tukufu ilivyofafanuliwa na yeye peke yake, vile vile hadithi sharif nazo zilifahamika tu na kufafanuliwa na masahaba wa mtume na maimamu wenye ijtihada. Ili waweze kuyafahamu hayo, Allahu taala aliwajaalia ma imamu wenye kufanya ijtihada elimu ya kisayansi, ya kidini, nguvu za kufahamu, kuona mbele, akili za hali ya juu, na mengine mengi. Mbele ya sifa zote hizi ilitangulia taqwa. Baada ya hayo inafuata nuru ya Allah kwenye nyoyo zao. Maimamu wetu wenye jitihada kwa msaada wa vipaji hivi, walifahamu maana ya maneno yake Allahu taala na mtume wake, na yale ambayo hawakuyafahamu waliyaripoti kwa njia ya **kiyasi**. Kila mmoja miongoni mwa maimamu wa madhehebu manne alieleza kwamba hakusema kulingana na akili yake (ra'y) na alikuwa anawaambia wanafunzi wake 'ukikuta hadithi sahihi basi maneno yangu yaache na fuata hadithi ya mtume'. Maimamu wetu wa madhehebu kauli hiyo waliwambia watu mujitahidi wenye elimu kama wao. Maulamaa hawa, walikuwa wenye Tarjih na wenye kujua dalili za wanazuoni wa madhehebu manne. Mujitahid wanawafahamu Maulamaa, kwa kusoma hadithi sahihi na sanadi zake, riwayat na kutambua ipi iliotangulia mwanzo na ipi iliofuata na kuchunguza sharti nyingi za Imamu walizotumia wakati wanafanya ijitihad. Au Mujtahid imamu aliamua kuhusu suala fulani kwa njia ya kiyasi kwa sababu hakujua hadithi inayohusiana na tatizo lake, tena baadae wafuasi wake (wanafunzi wake) wakakuta hadithi ya mtume na wakatoa hukumu tofauti. Pamoja na hayo wakati wanafunzi wanaagalia ijtihadi kama hii, hawakwenda kinyume na sheria alizotumia Imamu wakati wa ijtihada yake. Na baadae Mufti waliofuata nao walitoa fatwa, hivyo maandishi haya yote inafahamika kwamba, Waislamu ambao wamefuata madhehebu manne na mujtahid waliofundishwa

kwenye madhehebu yao, wamekuwa wakifuata sheria za Allahu taala na mtume wake. Mujtahid hawa walielewa sheria kutoka kwenye Quran tukufu na hadithi za mtume, ambazo hakuna mwengine alieweza kuelewa, na kufikisha kile walichofahamu. Waislamu nao wameiga na kufuata mujtahid vile walivyofahamu kutoka kwenye Quran na sunna za mtume, kwasababu katika sura an-Nahl aya ya 43 maana yake inaeleza kwamba **(msipojua ulizeni wanaojua)**.

Aya hii inaonyesha kwamba sio kila mtu anauwezo wa kufahamu Quran na Hadithi kwa usahihi. Inaamrisha wale watu ambao hawawezi kuzifahamu wasijaribu wao wenyewe kufahamu Quran au hadithi sharif lakini wajifunze kwa njia ya kuuliza wale ambao wamevifahamu. Ikiwa kila mtu angeweza kufahamu maana ya Quran tukufu na ya hadithi sharif ipasavyo, basi makundi 72 yenye uzushi yasingejitokeza. Watu wote waliosababisha makundi haya kutokea walikuwa wasomi, lakini hakuna hata mmoja kati yao aliyeweza kufahamu makusudio ya Quran na hadithi ipasavyo. Kutoyaelewa, walikwenda kinyume na njia sahihi na kusababisha mamilioni ya Waislamu kupotea. Baadhi yao wamekuwa kipao mbele kutoa tafsiri ya uongo kuhusu aya na hadithi mpaka wamekuwa wazushi kiasi kwamba wanaita watu walioko kwenye njia sahihi 'makafir' na 'washirikina'. Katika kitabu kiitwacho **Kashf ashshubuhat**, cha mawahabi kilichotafsiriwa kwenye lugha ya kituruki na kupenya kuingia nchini Uturuki kinaeleza kwamba kuua na kupora mali ya watu wa Ahl as-Sunna ni mubaha (inarusiwa). Kufanya ijtihad kwa maimamu wa madhehebu na kuanzisha madhehebu yao na Waislamu wote kuungana kwao juu ya madhehebu haya ni ihsan aliompa Allahu taala kipenzi chake mtume "swallallahu alaihi wa sallam" peke yake. Allahu taala kwa upande mwengine kama alivyowaumba maimamu wa Itiqad ili wazuie itiqadi za wapotofu, mazindiki, mulhid na watu wa shetani kutoharibu elimu inayoeleza imani, vile vile maimamu wa madhehebu waliumbwa kulinda dini isiharibiwe. Neema hii kwa kutopatikana katika uyahudi na ukrisitu, dini zao ziliharibiwa na kuwa kitu cha kuchezea.

Kwa mkusanyiko wa wanazuoni wa kiislam walisema kwamba, miaka mia nne (400) baada ya kufa kwa mtume "swallallahu alaihi

wa sallam" hajatokea mwanazuoni mwenye uwezo wa kufanya ijtihad. Mtu anayesema kwamba inafaa kufanya ijtihadi hivi sasa basi mtu huyu atakuwa mwenda wazimu au ana elimu ndogo kuhusu Uislam. Mwanazuoni mkubwa Jalal ad-Din al-Suyuti 'Abd ar-Rahman "rahmatullahi alaih" (alikufa mwaka 911 H [1505 M], kwenye nchi ya Misr) aliposema kwamba amefika katika daraja la ijtihad, wanazuoni wengine walimuuliza kuhusu swali ambalo lina majibu mawili tofauti na kumuuliza jibu gani ambalo linafaa zaidi. Hakuweza kuwajibu. Alisema kwamba anashughuli njingi sana kuweza kujibu swali hilo. Hata hivyo, alichoulizwa kufanya ni kutumia ijtihadi juu ya fatwa, iliyotolewa ambayo hii ni ijtihadi ya daraja la chini.

Kwa kuona kwamba mwanazuoni mkubwa kama al-Suyuti alishindwa kutumia ijtihadi juu ya fatwa iliyotolewa, sasa tutawapa jina gani wale wanaolazimisha watu wa kawaida kutumia ijtihad! Hawa watu tusipowaita wenda wazimu basi ni wajinga. Al-Imam al-Ghazali "rahmatullahi alaih" (alikufa mwaka 505 [1111 A.D]) alisema kwenye kitabu chake **Ihya' Ulum ad-Din** kwamba katika enzi zake hakukuwa na mjitahid yoyote. Endapo Muislam ambaye sio mjitahdi anajifunza hadithi sahihi na baadae akaanza kukosa utulivu kuhusu namna imam wa madhehebu yake alivyofundisha kwa sababu namna alivyofundisha imam wa madhehebu yake haikubaliani na hadithi, anafaa kutafuta ndani ya madhehebu manne mujtahid mwengine ambaye ijtihadi yake inalingana na hadithi na kufanya vitu kulingana na madhehebu ambayo mjtahid huyu anatoka. Mwanazuoni mkubwa al-Imam Yahya an-Nawawi "rahmatullahi alaih" (alikufa mwaka 676 H. [1277 M], kwenye mji wa Damascus) alielezea haya kwenye kitabu chake **Rawdat at-talibin**, kwamba hairuhusiwi kwa watu ambao hawajafikia daraja la ijtihad kuchambua sheria kutoka kwenye Nass, mfano: Quran na Sunna. Hivi sasa watu wajinga wanadai kwamba wamefikia daraja la ijtihad, kwamba wanaweza kuchambua sheria kutoka kwenye Nass na kwamba hawana haja tena ya kufuata moja kati ya madhehebu manne, na kuachana na madhehebu ambayo wamefuata kwa miaka. Wanajaribu kukanusha madhehebu kwa kutumia sababu zao zisizo na msingi. Wanatoa matamshi ya kijinga kama 'hatutofuata mawazo ya watu wa dini ambao walikuwa wajinga kama tulivyo sisi'.

Wanashawishiwa na shetani na kuharibiwa na nafsi zao na kudai kwamba wako juu. Hawazingatii kwamba kwa kusema hivyo hawaoneshi ukubwa wao bali wanaonesha ujinga wao. Miongoni mwao, tunaona pia baadhi ya wajinga wenye uzushi wanaosema na kuandika kwamba kila mtu anafaa kusoma na kuchambua sheria kutoka kwenye vitabu vya tafsir na sahihi al-Bukhari. Enyi ndugu Waislamu! Kwa kweli epukeni na kujenga urafiki na watu wajinga kama hao na kuwadhania kuwa ni watu wa dini. Fungamaneni kwanza na madhehebu ya imam wenu! Kila mtu ana haki ya kuchagua moja kati ya madhehebu manne atakayo. Lakini hairuhusiwi tena kujumuisha na kufuata tu masuala mepesi kwenye madhehebu yote yani hii inaitwa mfarakano (telfiq)[1].

Muislam mwenye uwezo wa kusoma na kuelewa hadithi sharif vizuri anafaa kusoma hadithi ambazo zinathibitisha madhehebu yake, baadae afanye vitendo vilivyoamrishwa na kuepuka vile vinavyokatazwa na hadithi sharif na ajifunze ukubwa na umuhimu wa dini ya kiislam, ukamilifu wa mtume "swallallahu alaihi wa sallam" na majina yake Allahu taala na sifa zake, maisha yake mtume, vitendo na miujiza yake, malengo ya kuishi hapa na baadae, kufufuliwa, kuhusu siku ya kiama pepo na moto, malaika, majini, ummat waliotangulia, mitume na vitabu walivyopewa, sifa za kipekee alizopewa mtume na Quran tukufu, maisha ya watu wa nyuma yake na ya masahaba zake, dalili za siku ya mwisho na mengine mengi kuhusu maisha ya dunia na baadae. Habari zote zinazohusiana na ulimwengu huu na baadae zimekusanyika kwenye hadithi za mtume. Yale ambayo tumeandika hapa yakieleweka, itakuwa dhahiri jinsi gani walivyo wajinga wale wanaosema kwamba sheria za Uislam ambazo hazijatolewa kwenye hadithi hazina maana. Miongoni mwa habari mbalimbali zilizotolewa na hadithi, hadithi zinazofundisha ibadat na mu'amalat ni chache sana. Kulingana na baadhi ya wanazuoni, kuna kama mia tano. [Hata na zilizorejewa zikijumuishwa kwa pamoja basi hazivuki elfu tatu.] Haiwezekani ya kwamba mmoja kati ya maimamu wa madhehebu anaweza kuwa hajapatapo kusikia moja kati ya hadithi sahihi chache hizi. Kila hadithi sahihi ilitumika kama ushahidi wa

---

[1] Mfarakano maana yake ni kufuata madhehebu yote manne kwa kuchagua njia ambazo ni nyepesi kulingana na madhehebu hayo.

maandishi angalau na mmoja kati ya maimamu wanne wa madhehebu. Muislam anayeona kwamba jambo fulani katika madhehebu yake haliendani na hadithi sahihi basi anafaa kufuata madhehebu mengine yanayolingana na ijtihad kwa mujibu wa hadithi. Labda imam wa madhehebu yake pia kasikia hadithi, lakini kafuata hadithi nyengine alioifahamu ilioonekana kuwa karibu na sahihi au ilifutwa na nyengine baadae, au kwa baadhi ya sababu nyengine zinazojulikana kwa mujtahid, hakuchukuwa hadithi ya mwanzo kama ushahidi wa maandishi. Ni vizuri kwa Muislamu ambaye kafahamu kwamba hadithi ya mwanzo ni sahihi kuachana na ijtihadi ya madhehebu yake ambayo hayaendani na hadithi na kufuata hadithi. Katika hali hii bado anafaa kuiga madhehebu mengine ambayo wametumia hadithi hii kwenye ijtihad ya kutatua suala lake. Kwa sababu imam wa madhehebu ya pili, kwa kujua mafundisho kuhusu sheria (ahkam) ambazo mtu huyu hakujua, aligundua kwamba hakukuwa na kitu kumshawishi mtu huyu kuamua kutekeleza kulingana na hadithi hiyo. Pamoja na hayo, inamruhusu pia kutekeleza kulingana na madhehebu yake, kwasababu hakuna wasiwasi kwamba imam huyu katekeleza kulingana na ijtihadi yake. Mukallid kutojua dalili hizi Uislam unampa udhuru. Kwasababu maimamu wote hakuna aliyekwenda kinyume na kitabu na sunna wakati anafanya ijtihad. Madhehebu yao ni ufafanuzi wa kitabu na sunna. Walifafanua maana na sheria katika kitabu na sunna kwa Waislamu. Waliyafafanua kwa njia kwamba Waislamu wanaweza kuelewa na wakayaandika kwenye vitabu. Kazi hii ya a’immat almadhahib "rahmatullahi alaih" ilikuwa kazi kubwa kwa Uislam kiasi ambacho nguvu za binadamu zisingetosha kutekeleza, Allahu taala angekuwa hajawasaidia. Upatikanaji wa madhehebu haya ni ushahidi kamili kuhakikisha kwamba Rasulullah "swallallahu alaihi wa sallam" ni mtume wa kweli na Uislam ni dini ya kweli.

Kutofautiana kwa ijtihad ya a’immat al’madhahib wetu kuhusu masuala ya dini ipo katika furu’ ad-din tu, kwa kusema masuala yanayohusiana na fiqh. Hakujatokea tofauti kati yao kulingana na usul ad-din, kwa mfano, kuhusu elimu ya itiqad au iman. Wala hawajatofautiana kwenye mafunzo ya furu’ ambayo inajulikana kuwa ya msingi katika dini na inayotolewa kwenye hadithi ambazo dalili zake zililetwa kwa njia ya tawatur. Walitofautiana tu kwenye

baadhi ya masuala ya elimu kuhusu furu’ ad-din. Hili lilitokea kutokana na tofauti zao kwenye kufahamu dalili kuhusu mambo haya. Na tofauti ndogo hii miongoni mwao ni rehma ya Allahu taala juu ya umma. Inaruhusiwa kwa kila Muislam kufuata moja kati ya madhehebu manne analopenda na kuona ni rahisi kwake. Rasulullah "swallallahu alaihi wa sallam" alitabiri tofauti hizi kama habari njema, na zimetokea kama alivyotabiri.

Hairuhusiwi kutumia ijthadi katika masuala ya **itiqadi** kwa mfano masuala yanayohusiana na iman. Hii inasababisha kupotea kutoka kwenye njia sahihi na uzushi. Tena ni dhambi kubwa mno. Kuna njia moja ilio sahihi kuhusiana na masuala ya itiqadi nayo ni: **Ahl as-Sunna wal-jamaat**. Tofuauti ambazo zilielezwa kuwa huruma ya Mungu kwenye hadithi sharif zilikuwa tofauti kwenye furu’ au ahkam. Katika suala ambalo madhehebu manne yametofautiana kwenye hukumu yake, basi hukumu moja tu ni sahihi. Wale wanaotekeleza kulingana na hukumu hii iliosahihi watapewa thawabu mbili, na wale wanaotekeleza kulingana na ile isio sahihi watapewa thawabu moja. Katika madhehebu kuna huruma kiasi kwamba unaruhusiwa kuacha madhehebu fulani na kufuata dhehebu jengine. Lakini hairuhusiwi kufuata madhehebu yoyote zaidi ya haya manne ambayo ni ya Ahl as-Sunna, hata madhehebu ya masahaba kwa sababu madhehebu yao hayakuwekwa kwenye maandishi na yamesahaulika. Hivi sasa hakuna uwezekano wa kufuata madhehebu yoyote zaidi ya haya manne. Imam Abu Bakr Ahmad ar-Razi "rahmatullahi alaih", alikufa mwaka 370 H. 980 M], pia alikariri kwamba imetangazwa kwa ujumla wa wanazuoni wa kiislam kwamba hairuhusiwi kufuata masahaba moja kwa moja. Napendekeza kwamba wale wanaotaka kufahamu vizuri ubora wa madhehebu ya mjitahid, hasa ya a’immat al-madhahib wanne, kwa ukweli kwamba madhehebu yao hayakwenda mbali (kinyume) na kitabu na sunna na sheria ambazo walizitumia wakati wanafanya ijma’a na qiyas hazijatokana na mawazo yao lakini zilitolewa kwenye Kitabu na Sunna, anafaa kusoma vitabu kama **Al-mizan al-kubra** na **mizan al-Khidriyya**

kilichoandikwa na Imam Abd al-Wahhab al-Sha'rani "rahmatullahi alaih".[1]

Si sahihi kusema, "Quran tukufu haisemi au haijataja wanazuoni wa dini". Kuna aya nyingi zinazowasifu wanazuoni (ulamaa) na elimu. Hadhrat Abd al-Ghani al-Nablusi [alikufa 1143 H. (1731 M.)] aliandika katika kitabu chake **Al-hadiqa** "aya ya 7 ya sura al-Anbiyaa inaeleza **'waulizeni wenye dhikri ikiwa nyinyi hamjui'** hapa 'dhikri' maana yake ni 'Elimu'. Aya hii inaamrisha watu wasiojua kutafuta wataalamu na kuwauliza na kujifunza kutoka kwao. Imeelezwatena kwenye aya ya 7 ya sura aali-Imran: **"wenye elimu tu ndio wanaofahamu maana ya aya za mutashabihat"**. Kwenye aya ya 18 katika sura hiyo hiyo **"kuwepo kwa Mungu na umoja wake inafahamika na kuelezwa na wenye elimu"** kwenye aya ya 81 sura al-Qasas **"Na wakasema wale walio pewa elimu: Ole wenu! Malipo ya Mwenyezi Mungu ni bora kwa mwenye kuamini na akatenda mema. Wala hawatapewa hayo isipokuwa wenye subira".** Kwenye aya ya 56 ya sura ar-Rum **"Na wale waliopewa elimu na iman watasema, 'hii ndio siku ya kufufuliwa mliokua mnaikanusha duniani"** kwenye aya ya 108 ya sura Isra **wenye elimu, wanaposikia Quran al-karim, watasujudu na kusema, hana kasoro Mola wetu ambae havunji ahadi yake"** kwenye aya ya 54 sura al-Hajj **"Wenye elimu wanafahamu kwamba Al-Quran al-karim ni neno la Allah"**, kwenye aya ya 50 ya sura al-Ankabuut **"Al-Quran al-karim imetulia kwenye vifua vya watu wenye elimu",** kwenye aya ya 6 ya sura Saba **"wenye elimu wanafahamu kwamba al-Quran al-karim ni neno la Allah na kumfanya mmoja kupata mapenzi ya Allahu taala"**, kwenye aya ya 11 ya sura al-Mujadilah **"vyeo vya juu vitapewa wale wenye elimu peponi"**, kwenye aya ya 27 ya sura Fatir **"wenye elimu tu ndio wanaomuogopa Allahu taala"**, kwenye aya ya 14 ya sura al-Hujurat

---

[1] Yusuf an-Nabhani, Hujjat-Allahi ala l-almin, p.771. nukuu iliopo juu ambayo imetafsiriwa kutoka Kiarabu asili, haina neno lolote lililoengezwa na mfasiri, ambaye amefanya kazi kwenye vitabu vyetu vyote, maneno ya ziada yamewekwa katika mabano hapa ili kuepuka kuyachanganya na maandishi yaliotafsiriwa. Asili ya kifungu hapo juu kilichotolewa kwenye Hujjat-Allahi ala-l-alamin kilizalishwa na offset Istanbul mnamo mwaka 1394 [1974].

**“Hakika aliyetukuka zaidi miongoni mwenu kwa Mwenyezi Mungu ni yule anayemcha Mwenyezi Mungu zaidi”**. Imetajwa kwenye hadithi ilionukuliwa katika kitabu hicho ukurasa wa 365 **“Allahu taala na malaika na viumbe wote wanamuombea mtu anayefundisha watu wema kwenye siku ya malipo (kiama), kwanza mitume, halafu wanazuoni, halafu mashahidi watapewa fursa ya kufanya maombezi ‘ewe binaadamu‘, Juwa kwamba elimu inaweza kupatikana kwa njia ya kuwasikiliza maulamaa, jifunze elimu. Kujifunza elimu ni ibada. Mwalimu na mwanafunzi watapewa thawabu ya kufanya jitihada. Kufundisha elimu ni kama kutoa sadaka. Kujifunza elimu kutoka kwa ulamaa ni kama kusali usiku (tahajjud)”.** Tahir Buhari, muandishi wa kitabu cha fatwa kinachoitwa Khulasa, anasema; kusoma vitabu vya Fiqh unavuna thawabu nyingi kuliko kusali usiku. Kwa sababu ni fardhi kujifunza yalio fardhi na haram kutoka kwa waalim au vitabu vyao. Kusoma vitabu vya fiqh ili utekeleze kulingana na mafunzo au kufundisha unapata thawabu kuliko kusali salat tasbih. Hadithi sharif inasema: **(kujifunza elimu, unapata thawabu nyingi kuliko kufanya ibadat za sunna. Kwasababu anafaidika yeye pia, wanaosoma nao wanafaidika)** na **(yule anayesoma ili aweze kuwafundisha wengine atalipwa thawabu za ma siddik)**. Lakini mafunzo ya kiislam yanatolewa tu kwa ustadh au kwenye kitabu. Wanaosema kwamba hakuna haja juu ya vitabu vya kiislam na viongozi basi ni waongo, tena mazindiq. Wanadanganya Waislamu na kuwapeleka kwenye kuangamia. Mafunzo  yaliyomo katika vitabu vya dini yalitolewa kwenye Quran na hadithi sharif. Tafsir kutoka kwenye **Hadika** imeisha.

Allahu taala alimtuma mtume wake "alaihis-salaam" ili aweze kufundisha Quran karim. As-Sahabat al-kiram walijifunza elimu ya Quran tukufu kutoka kwa mtume. Wanazuoni wa kiislamu nao wakajifunza kutoka kwa masahaba na Waislamu wote walijifunza kutoka kwa wanazuoni wa kiislam na vitabu vyao. Inaelezwa katika hadithi sharif **“Elimu ni hazina. Funguo zake ni kuuliza na kujifunza”, “jifunze na fundisheni elimu!”, “kila kitu kina chimbuko. Chimbuko la taqwa ni moyo wa arif” kufundisha elimu kunafuta madhambi”.**

Al-Imam ar-Rabbani "rahmatullahi taala alaih" aliandika kwenye barua ya 193 ya mkusanyiko wake wa kwanza wa kitabu

chake **Maktubat** kwamba “Mukallaf yaani mtu ambaye amebaleghe ni lazima arekebishe Imani yake pamoja na itiqadi kwanza. Yaani kujifunza na kuamini mafunzo kuhusu akida yalioandikwa na wanazuoni wa Ahl as-Sunna. Allahu taala Awape thawabu nyingi watu wakubwa hao Amin. Siku ya kiama kuepuka adhabu za moto wa jahannam inategemea na kuamini mafunzo yalioelezwa na watu hao. Wale watakaookolewa kutokana na jahannam ni wale tu wanaofuata njia ya watu hawa. [Wanaofuata njia ya watu hawa wanaitwa **(Sunni)**] wafuasi wa mtume "swallallahu alaihi wa sallam" na masahaba zake ni hawa tu. Elimu yenye thamani na sahihi inayotolewa kwenye Kitabu yani Quran tukufu na sunna yani hadithi sharif ni ya watu hawa tu waliofundisha kutoka kwenye kitabu na sunna. Kwa sababu kila mwenye bid’a yani kila mwenye mageuzi na kila mjinga na wasio na madhehebu, kwa fikra zao potofu na akili zao fupi wanasema kwamba wanazitoa kutoka kwenye kitabu na sunna. Wanajaribu kuwadhalilisha maulamaa wa Ahl as-Sunna. Kwa kusema, kila maneno waliochukuwa kutoka kwenye kitabu na sunna isifikiriwe kwamba ni ukweli.

Kufafanua Itiqad ya ukweli iliofundishwa na maulamaa wa Ahl as-Sunna wal-jamaat, alim mkubwa Hadhrat Turpusti katika kitabu chake alichokiandika kwenye lugha ya kiajemi **(Al-Mu’tamad)** ni kitabu chenye thamani na kiliandikwa kwa uwazi. Kinafahamika kwa wepesi. **Hakikat Kitabevi** nao pia mwaka 1410 H. 1989 M. walikichapisha. Fadlullah ibn Hasan Turpusti ni mfuasi wa madhehebu ya Hanafi. Alifariki dunia mwaka wa 661 H. [1263 M.].

Baada ya Akaidi yaani baada ya kurekebisha yale yanayohusiana na kuabudu, kusoma na kufuata vitu vilivyo **Halali**, **Haram**, **Fardha**, **Sunna**, **Mandub** na **Makruh** kama vilivyoandikwa na maulamaa wa Ahl as-Sunna kwenye vitabu vyao ni lazima. Vitabu vilivyoandikwa na wajinga ambao hawajafahamu ukubwa wa maulamaa hawa havipaswi kusomwa. Allah atuepushe. Muislam ambaye itiqadi yake haamini yaliomo kwenye madhehebu ya Ahl as-Sunna, siku ya kiama hatookolewa dhidi ya moto wa Jahannam. Mwenye Imani sahihi akilegeza katika ibada, hata asipofanya toba anaweza kusamehewa. Hata asiposamehewa, baada ya kuadhibiwa ataokolewa dhidi ya Jahannam. Jambo muhimu ni kurekebisha itiqadi. Ubaydullahi Ahrar [qaddas-Allahu taala sirrahu-l-‘aziz

alifariki dunia mwaka 895 H. 1490 M. kwenye mji wa Samarkandi] alisema; ningekuwa nimepewa kashf zote na karamat zote lakini nikakosa itiqadi ya Ahl as-Sunna wal-jamaat basi ningejiona kuwa nimeangamia. Kama ningekosa kashf na karamat na dhambi zangu zikawa nyingi lakini nikapewa ihsan ya itiqadi ya Ahl as-Sunna wal-jamaat basi nisingehuzunika.

Leo, Waislamu wa India wamekuwa wakiwa. Maadui wa Uislam wameshambulia kwa kila upande. Shillingi moja inayolipwa kwa kusaidia Uislam leo ina thawabu nyingi kuliko maelfu ya shillingi zilizolipwa wakati mwengine. Huduma kubwa ya kufanywa kwa ajili ya Uislam ni kupata vitabu vya Ahl as-Sunna vinavyofundisha Iman na Uislam na kuvisambaza vijijini na kwa vijana. Mtu ambaye amepewa neema hii anafaa kuifurahia na kumshukuru Allahu taala kwa sababu ana bahati. Daima kuhudumia Uislam ni kitendo kizuri. Lakini kwenye mda kama huu ambapo Uislam umedhoofishwa, nguvu nyingi zimefanywa kuangamiza Uislam kwa njia ya uongo na kusingizia, kusambaza itiqadi ya Ahl as-Sunna ni bora zaidi na ina thawabu nyingi. Mtume "swallallahu alaihi wa sallam" aliwambia masahaba zake kwamba **‘mnaishi kwenye wakati ambapo mkitekeleza tisa kati ya kumi katika maamrisho yake Allahu taala na makatazo yake na mkiasi moja kati ya kumi basi mtaangamia. Mtaadhibiwa. Baada yenu utakuja wakati ambapo atakaetekeleza moja kati ya kumi katika maamrisho na makatazo ataokolewa.’** [Ukweli huu umeandikwa kwenye **Mishkat-ul masabih**, vol. 1, ukurasa wa 179 na kwenye **Tirmizi, Kitab-al Fitan,** ukurasa wa 79]. Huu ndio wakati ulivyoelezwa kwenye hadithi hii. Ni muhimu kupambana dhidi ya makafiri, ili kuwajua wale wanaoshambulia Uislam na kuwachukia[1].

Ili kusambaza vitabu na maneno ya wanazuoni wa Ahl as-Sunna, sio lazima mtu awe mwanazuoni au karama. Kila Muislam anafaa kupambana kufanya kazi hiyo. Fursa hii isipotezwe. Kwenye siku ya kiama kila Muislam ataulizwa kuhusu hili na wataulizwa kwa nini

---

[1] Jihad kwa njia ya jeshi (jihad qatli) inafanywa na serikali, kwa jeshi lake. Waislamu kufanya jihad katika hali hii ni kupelekwa kama maaskari kutekeleza jukumu walilopewa na serikali. Jihad qawli, inayofanywa kwa njia ya hotuba na maandishi ni bora kuliko jihad qatli na imeandikwa pia kwenye barua ya 65.

hawaja uhudumia Uislam. Wale wasiojitahidi kusambaza vitabu vinavyofundisha Uislam na wale wasiosaidia watu na taasisi kueneza elimu ya kiislam wataadhibiwa vibaya. Katika siku hiyo udhuru hautokubaliwa. Ingawa mitume "alaihimus-salaam" walikuwa watu wa juu na bora zaidi, hawakuzingatia starehe zao. Wakati wakusambaza dini ya Allahu taala, kuelekea furaha ya kudumu, walijitahidi mchana na usiku. Kwa wale walioomba miujiza walijibiwa kwamba **(Allahu taala anaumba miujiza na kazi yangu ni kufundisha dini ya Allah).** Wakati wanatekeleza kazi hii Allahu taala naye aliwasaidia na kuumba miujiza. Na sisi pia tunafaa kusambaza vitabu na maneno ya wanazuoni wa Ahl as-Sunna "rahmatullahi alaih" na kuwaambia vijana na marafiki zetu ubaya wa makafiri na kufichua uongo wa maadui na wale wanaowakashifu na kuwatesa Waislamu. [Kwa kusema haya sio gibat (umbeya) bali ni Amru bil-ma'ruf]. Watu ambao hawapiganii njia hii kwa kutumia mali zao, nguvu zao na vyeo vyao hawataokolewa dhidi ya adhabu. Wakati wa kupigania njia hii, mateso na kunyanyaswa ni lazima vichukuliwe kama ni ushindi mkubwa kwake. Mitume "alaihimus-salaam", wakati wanafundisha maamrisho ya Allahu taala walikumbana na hujuma za watu wajinga. Waliteswa sana. Muhammad "alaihis-salaam" ambae ni kipenzi chake Allahu taala na aliechaguliwa kuwa juu ya mitume wote alisema: **'Hakuna mtume alieteswa zaidi kuliko mimi'** tafsiri kutoka **(Maktubat)** imeisha.

[Kila Muislam anawajibika kujifunza itiqadi ya Ahl as-Sunna na kuwafundisha watu wake ambao anauwezo wa kuwashawishi. Vitabu, majarida na magazeti yanayoelezea maneno ya wanazuoni wa Ahl as-Sunna yanafaa kutafutwa na kununuliwa na kutumwa kwa vijana ili waweze kuyasoma. Pia vitabu vinavyofichua malengo ya maadui wa Uislam vinafaa kusambazwa].

Wanazuoni wa Ahl as-Sunna walioonesha Waislamu wote njia sahihi duniani na kutuongoza kujielimisha dini ya Muhammad "alaihis-salaam" bila mabadiliko yoyote au kuongeza kitu, ni wanazuoni wa madhehebu manne ambao walifikia daraja la ijtihadi. Watu hawa wanne ni **Abu Hanifa Nu'man ibn Thabit "**rahmatullahi alaih": Alikuwa mmoja kati ya wanazuoni wa kiislam wakubwa. Alikuwa kiongozi wa Ahl as-Sunna. Wasifu wake umeandikwa kwa urefu kwenye vitabu kama **Se'adet-i Ebediyye**

na **Faideli Bilgiler**. Alizaliwa mwaka wa 80 H. (699 M.) na mnamo mwaka wa 150 H. (767) aliuliwa kwenye mji wa Baghdad.

Wa pili ni **Imam Malik ibn Enes** "rahmahu-Allahu taala", ni alim mkubwa. Alizaliwa mwaka 90 H. kwenye mji wa Madina na mwaka 179 H. (795 M.) alifariki dunia huko Madina. Imeandikwa katika Ibn Abidin kwamba aliishi miaka 89. Malik ibn Abi Amir ni babu yake.

Wa tatu ni **Imam Muhammad ibn Idris al-Shafi'i** " rahmatullahi alaih" ambae alipendwa na wanazuoni wa kiislam wote. Alizaliwa mwaka 150 M. (767 M.) nchi ya Palestine mji wa Ghaza na alikufa mwaka 204 H. (820 M.).

Wa nne ni **Imam Ahmad ibn Hanbal** "rahmah-Allahu taala". Alizaliwa mwaka wa 164 H. (780 M.) kwenye mji wa Baghdad na kwenye mji huo huo mwaka 241H. (855M.) alikufa. Ndio nguzo za jengo la Uislam "rahmahumllah ajma'in".

Leo mtu asiefuata mmoja kati ya maimamu wanne hao yupo kwenye hatari kubwa. Ametoka kwenye njia sahihi. Zaidi ya hawa, maulamaa wa Ahl as-Sunna wengine wapo wengi. Nao pia madhehebu yao ya kweli yalikuwepo. Lakini baada ya mda madhehebu yao yalisahauliwa. Hayajaandikwa kwenye vitabu. Kwa mfano **(Fukaha-u sab'a)** walimu Saba wakubwa wa mji wa Madina na **Umar bin Abdul'aziz, Sufyan bun Uyaina**[1]**, Is'haq bun Rahawa, Dawud atTa'i, Amir bun Sharahil ash-Sha'bi, Layth ibn Sa'd, A'mash, Muhammad bun Jarir at-Tabari, Sufyan ath-Thawri**[2] **na Abdurrahman Awza'i** "rahmatullahi alaih" ni miongoni mwao.

Masahaba wote "radiyallahu anhuma" walikuwa nyota za kuongoza kuelekea uongofu. Mmoja kati yao anatosha kuongoza ulimwengu wote kwenda njia sahihi. Walikuwa mujtahid. Kila mmoja alikuwa kwenye madhehebu yake. Madhehebu mengi yalikuwa yanafanana. Lakini kwa kuwa madhehebu yao hayakukusanywa na kuandikwa kwenye kitabu, haiwezekani kwetu kuwafuata. Madhehebu manne ya maimamu wanne, yale waliofundisha kuhusu vitu vinavyofaa kuamini na vitu vinavyofaa

---

[1] Sufiyan bIn Uyaina mwaka 198 H. (813 M.) alikufa kwenye mji wa Makka.
[2] Sufiyan ath-Thawri alifariki dunia mwaka 161 H. (778 M.) kwenye mji wa Basra.

kufanywa, yalikusanywa pamoja na kufafanuliwa na wanafunzi wao. Walifungamana na vitabu. Leo kila Muislam ni lazima kuwa chini ya moja ya madhehebu yaliotajwa hapo juu na kuishi na kutekeleza ibada kulingana na madhehebu hayo. [Yule asietaka kufuata moja kati ya madhehebu haya basi hayupo katika kundi la Ahl as-Sunna].

Wawili kati ya wanafunzi wa maimamu wanne hawa , wamefikia daraja la juu kuhusu kusambaza masuala ya Iman. Kwa hivyo ikawa katika Itiqad au Iman madhehebu mawili. Itiqad sahihi kulingana na Quran na hadithi, ni itiqadi tu ilionyeshwa na maimamu wawili hawa, ambao walieneza itiqadi ya Ahl as-Sunna duniani kote, itiqad ambayo ni yenye uokovu. Mmoja kati yao alikuwa **Abu al-Hasan al-Ash'ari** "rahmatullahi alaih", aliezaliwa Basra mwaka 226 H. (879 M.) na kufariki dunia mwaka 330 H. (941 M.) kwenye mji wa Baghdad. Mwengine alikuwa Abu Mansur Maturidi "rahmatullahi alaih" aliekufa mwaka 333 H. (944 M.) kwenye mji wa Samarkand. Katika masuala ya Imani, kila Muislamu anafaa kufuata mmoja kati ya maimamu wakubwa hawa. Njia (turuq) za maauliya ni sahihi. Hawajatofautiana hata kidogo kutoka kwenye Uislam.[1] Maauliya wana karamat. Karamat yao ni sahihi na ukweli. Al-Imam Abdullah al-Yafi'i (alikufa mwaka 768 H. (1367 M.) kwenye mji wa Makka) alisema; "Ghawth ath-Thaqalain Mawlana Abd al-Qadir al-Gaylani "qaddasa-Allahu sirruhu-l-aziz"[2] karamat zake zimetambulika sana

---

[1] Katika kila karne kumekuwa na waongo na wazushi ambao wametumia dini kuendesha maisha yao ya kidunia na wanakua mbele kwa kujificha kwenye majina ya mawalii, murshid au watu wa dini. Leo kuna watu wabaya katika kila taaluma, katika kila tawi la ufundi na katika kila ofisi rasmi. Kuona watu wanaotafuta maslahi yao na furaha kwa kuwajeruhi wengine, ingekuwa udhalimu au ujinga kuwalaumu watu wote na ufundi ambapo watu hao wanajichanganya nao. Ingesaidia watenganishaji. Kwa sababu hii, upatikanaji wa watu wazushi wa dini na ujinga, watu wa uongo wa turuq (mitazamo, njia) hawatufanyi sisi kusema vibaya juu ya wanazuoni wa kiislam au watu wa kubwa wa njia ya Tasawwuf ambao huduma zao zenye kuheshimika zimejaza historia. Tunafaa kujua kwamba watu wanaowakashifu ni madhaalimu.

[2] Abdulqadir Gaylani alikuf mwaka 561 H. (1161 M.) kwenye mji wa Baghdad.

kiasi kwamba mtu hawezi kuwa na shaka au kuzikanusha kwa sababu zimeenea kwa njia ya **Tawatur** na sanadi yake inaaminika.

Hairuhusiwi kumwita kwa kuiga wengine, mtu anaesali kwamba ni kafiri isipokuwa ukafiri wake utaeleweka kutokana na yeye kutangaza wazi na bila kulazimishwa kusema neno au kutumia kitu kinachomfanya kuwa kafiri. Hatuwezi kuweka laana juu ya mtu huyu isipokuwa ieleweke kwamba alikufa katika hali ya ukafiri. Hairuhusiwi pia kuwalaani makafiri. Kwa mujibu huo, ni vizuri kutomlaani Yazidi.

5. **Nguzo ya Tano ya Iman ni "Kuamini siku ya mwisho (al-Yawm al-akhir)".** Hii inaanzia pale mtu anapoondoka duniani na kuendelea hadi siku ya kiama. Sababu inayofanya siku hiyo kuitwa siku ya mwisho ni kwamba usiku hautokuja tena baadae, au kwa sababu inakuja baada ya dunia. Siku iliotajwa katika hadithi hii sio kama mchana na usiku tunavyojua sisi. Siku hiimaana yake ni muda, ni wakati. Kiama kitakuja lini haikutajwa. Wakati gani kitakuja hakuna anayefahamu. Hata hivyo, mtume wetu "swallallahu alaihi wa sallam" alitaja baadhi ya alama zitakazojitokeza. Kwanza Hadhrat Mahdi atakuja, Issa "alaihis-salaam" atashuka kutoka mbiguni kwenye mji wa Damascus (Sham), Dajjal atatokea. Ya'juj na Ma'juj (Gog and Magog) kama wanavoitwa wataenea kila sehemu. Jua litachomoza magharibi, yatakuwepo matetemeko makubwa. Mafunzo ya dini yatasahauliwa. Ufisadi na mabaya yatakithiri. Watu Wapagani, wanaokwenda kinyume na maadili, wadanganyifu watakuwa viongozi. Amri zake Allahu taala hazitaamrishwa kutekelezwa. Mambo ya Haramu yatafanywa kila sehemu. Moto utatoka yemen. Mbingu na milima vitapasuka vipande vipande. Jua na mwezi vitazimwa na kuwa giza. Bahari zitajichanganya na kuchemka halafu zitakauka.

Waislamu wanaotenda maovu wanaitwa **(Fasik)**. Mafasik na makafiri wote wana adhabu kaburini. Haya bila shaka ni lazima kuaminiwa. Maiti anapotiwa kwenye kaburi, anafufuliwa kwa uhai ambao haujulikani, ataona raha au adhabu ndani ya kaburi. Malaika wawili wanoitwa **Munkar** na **Nakir** wanakuja kwa sura ya mtu asiejulikana mwenye kutisha na kuuliza maswala kama ilivyoeleza hadithi sharif kwa uwazi. Maswali ya kaburini, kulingana na baadhi ya maulamaa, baadhi yatatoka kwenye akida, baadhi ya maulamaa

wanasema maswala yote yatahusiana na akida. Kwa sababu hii, tunafaa kuwafundisha watoto wetu namna ya kujibu maswali haya. Mola wako ni nani? Dini yako ni ipi? Upo kwenye umma (wa mtume) gani? Kitabu chako ni kipi? Kibla chako ni wapi? Kuhusiana Iman na Itiqadi ya madhehebu yako ni ipi? Imeandikwa kwenye **Tadhkirat al-Qurtubi** [1] kwamba wale ambao sio Ahl as-Sunna hawatoweza kujibu maswali haya. Wale watakaojibu maswali hayo vizuri, kaburi zao zitapanuliwa, hapa dirisha la pepo litafunguliwa. Kila asubuhi na jioni atakuwa anaiona nafasi yake kwenye pepo. Malaika watakuwa wanamtendea wema na kumpa habari njema. Yule atakaeshindwa kujibu, atapigwa na nyundo ya chuma na atapiga kelele ambayo itasikika na kila kiumbe isipokuwa binadamu na majini. Kaburi lake litafanywa finyu (nyembamba) kiasi kwamba mifupa yake itaingiliana. Dirisha la Jahannam litafunguliwa. Kila asubuhi na jioni ataiona nafasi yake motoni. Ataadhibiwa katika kaburi hadi siku ya kufufuliwa.

Ni lazima kuamini kwamba kuna maisha baada ya kufa. Baada ya mwili na mifupa kuoza na kuwa mchanga na gas, vitarejeshwa tena kwenye hali ya mwili na nyoyo zitaingizwa kwenye miili iliokuwa inaishi, na kila mtu atafufuka kutoka kwenye kaburi lake. Ndio sababu siku hii inaitwa siku ya **Qiyama** (kufufuka).[2]

Viumbe hai wote watakusanywa kwenye eneo linaloitwa **Mahshar**. Kila mtu daftari lake kwa kupeperushwa litakwenda kwa Allahu taala, muumbaji wa ulimwengu, mbingu, nyota na chembe

---

[1] Mwandishi wa Tadhkira anaitwa Muhammad Kurtubi Maliki alikufa mwaka 671 H. (1272 M.). Muhtasar-I Tadhkira-I Kurtubi kilichapishwa upya na Hakikat Kitabevi mwaka 1421 H. (2000 M.)

[2] Mimea hunyonya carbon dioxide kutoka kwenye hewa, maji na chumvi yani dutu madini kutoka kwenye udongo na kuviunganisha pamoja na kuumba dutu za kikaboni, yaani viungo vyetu hai. Inafahamika leo kwamba mimenyuko kemikali inayochukuwa miaka inaweza kutokea chini ya sekunde endapo catalyst (kichocheo) kimetumika. Vile vile, Allahu taala atajumuisha maji, carbon dioxide na dutu madini ndani ya kaburi na kuumba dutu za kemikali na viungo hai ndani ya muda mchache. Mukhbir-i Sadiq (msemaji ukweli yaani mtume) alisema kwamba tutarejeshwa kwenye uhai mwengine namna hii. Na elimu ya science inaonyesha kwamba haya tayari yanafanyika duniani.

zote amaye atayafanya haya kutokea. Mtume wa Allahu taala "swallallahu alaihi wa sallam" alisema kwamba haya yatatokea. Anayoyasema bila shaka ni ukweli. Bila shaka yote yatatokea.

Watu wema na wazuri watapewa madaftari yao kwa mkono wa kulia, waovu na wabaya watepewa kwa nyuma au mkono wa kushoto. Matendo mema na mabaya, makubwa na madogo, yaliotendwa kwa siri na ya wazi yote yatakutwa yameandikwa kwenye daftari. Hata yale ambayo hayakujulikana na malaika wawili **(kiraman katibiin)** yatasemwa ima kwa njia ya viungo vya mwili au na Allahu taala, kila kitu kitaulizwa na kitahisabiwa. Kwenye mahshar mambo yote ya siri Allahu taala atakapotaka yatafichuka. Malaika wataulizwa mlifanya nini duniani na ulimwenguni? Mitume "alaihim salaam" wataulizwa walifundisha vipi amri za Allahu taala kwa waja wake? Pia kila mtu ataulizwa alimtii vipi mtume wake na yaliofundishwa na mitume mlitekeleza vipi?, haki zilizopo Kati yenu mlizitunza vipi wataulizwa?, Kwenye mahshar, watu wenye Imani na wenye matendo mema na tabia nzuri watazawadiwa na kutunzwa, na watu wabaya wenye matendo mabaya na tabia mbaya watapewa adhabu kali.

Allahu taala kwa uadilifu na ihsani yake miongoni mwa waumini waliotenda madhambi makubwa na madogo atawasamehe wale atakaotaka. Mbali na shirk na ukafiri, kila dhambi akitaka atasamehe, akitaka kwa uadilifu wake kwa madhambi madogo pia wataadhibiwa. Makafiri wenye kitabu na wasiona kitabu yani wale ambao hawa amini kwamba Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam" ni mtume wa watu wote na wanaokataa hata moja kati ya maamrisho na makatazo yake na wakafa katika hali hii bila shaka watatupwa kwenye Jahannam na wataadhibiwa milele.

Kwenye siku ya kiama, patakuepo na **Mizani** ambayo ni tofauti na zile tunazozijua. Mizani hii itatumika kupima vitendo na tabia. Itakuwa kubwa kiasi ambacho mmoja kati ya mikono yake ni sawa na mbingu na ardhi. Mizani ya matendo mema itakuwa inang´aa na itakuwa upande wa kulia wa Arsh ambapo inapatikana pepo, na mizani ya matendo maovu itakuwa nyeusi na itakuwa upande wa kushoto wa Arsh ambapo unapatikana moto. Vitendo, maneno, mawazo na mitazamo inayofanywa hapa duniani yatakua na sura huko, na matendo mema yatakuwa na sura yenye kung´aa na

maovu yatakuwa na sura nyeusi na pia yatapimwa kwenye mizani hii ambayo haifanani na mizani za duniani. Ilisemwa kwamba mkono wenye uzito zaidi utapanda juu na ule hafif utashuka chini. Kulingana na baadhi ya wanazuoni, zitakuepo mizani tofauti tofauti. Na wengine wengi walisema “Dini haijaonyesha wazi idadi ya mizani na zitakuaje, kwa hivyo ni vizuri kutofikiria kuhusu mizani”.

Patakuwepo na daraja linaloitwa **Sirat**, ambalo litajengwa juu ya moto kwa amri ya Allahu taala. Kila mtu ataambiwa kuvuka daraja hilo. Siku hiyo, mitume wote wataomba; “Ewe Allah! Toa salama! Watu wa pepo watavuka daraja hili kwa wepesi na kuingia peponi. Miongoni mwa hawa watavuka kwa mwendo kama radi, wengine kama upepo na wengine kama farasi anaekimbia. Sirat hii ni nyembamba kuliko nywele na kali kuliko kisu. Duniani kufuata Uislamu ni kama hivyo. Kufuata Uislam kwa ukweli ni kama kuvuka daraja (sirat). Hapa duniani wale wanaopambana na nafsi zao (matamanio) kwa nguvu basi huko watavuka sirat kwa wepesi na kwa raha. Wale wasiofuata Uislamu kwa sababu ya nafsi (matamanio) yao watavuka daraja (Sirat) kwa ugumu. Kwa sababu hii, njia sahihi inayoelezewa na Uislamu, Allahu taala aliipa jina la **“Sirat al Mustaqim”.** Mfano wa jina hili kwa wanaofuata Uislam ni kama kuvuka daraja la sirat. Watu wa motoni, badala ya kuvuka Sirat wataanguka kwenye moto.

Kutakuwa na chemchem (hodhi) inayoitwa **Hawd al-Kawthar** ambayo ni kwa ajili ya mtume wetu Muhammad "swallallahu alaihi wa sallam". Urefu wake ni mwendo wa mwezi mzima. Maji yake ni meupe kuliko maziwa, harufu yake ni nzuri kuliko misk. Glasi zilizoizunguka ni nyingi kuliko nyota. Mwenye kunywa kuonja maji yake hata mara moja hatopata kiu tena hata akiwa kwenye moto wa Jahannam.

Inafaa kuamini kwamba **Shafa’a** (maombezi) ni ukweli. Mitume, mawalii, waumini, malaika na wale watakaokubaliwa na Allah watawaombea wale waliotenda maovu madogo na makubwa na walikufa bila kutubu na maombi yao yatakubaliwa. Mtume wetu "alaihis-salaam" alisema **“nitawaombea wale waliotenda maovu makubwa ndani ya umma wangu”.** Kwenye Mahshar Shafa’a (maombezi) yatakua ya aina tano.

**Ya kwanza,** wenye dhambi baada ya kuchoka kutokana na msururu na kusubiri kwa muda mrefu kwenye sehemu ya mahshar, wataomba kwamba hisabu yao ifanywe haraka. Na kutakuwa na shafa'a kwa hili.

**Ya pili,** kutakuwa na shafa'a kwa ajili ya maswali kufanyika kwa wepesi na haraka.

**Ya tatu,** kutakuwa na shafa'a kwa Waislamu wenye dhambi ili wasianguke kutoka sirat na kuingia motoni na wataokolewa kutokana na moto.

**Ya nne,** kutakuwa na shafa'a kwa Waislamu wenye dhambi kutolewa motoni.

**Ya tano,** kutakuwa na shafa'a kwa ajili ya kuwapandisha Waislamu ngazi za juu ndani ya pepo. Ndani ya pepo kuna neema zisizohesabika na wataishi milele.

Pepo ina ngazi nane. Kila mtu ngazi yake itategemea kiwango cha vitendo vyake. Pepo na moto vipo sasa hivi. Pepo ipo juu ya mbingu ya saba. Jahannam ipo chini ya kila kitu. Kuna pepo nane na Jahannam saba. Pepo ni kubwa kuliko dunia, jua na mbingu. Jahannam ni kubwa kuliko jua.

6. **Nguzo ya mwisho kati ya nguzo sita za Iman ni "ni kuamini kadar, kwamba kheri na shari yanatokana na Allahu taala".** Mema na mabaya, faida na hatari, mapato na hasara vinayomwandama binaadamu vyote ni makadirio yake Allahu taala. 'Qadar' maana yake kilugha ni 'kupima wingi, uamuzi na amri. wingi na ukubwa pia inatumika. Makadirio ya Allahu taala ya tangu azali juu ya kuwepo kitu inaitwa **qadar**. Kutokea kwa qadar kunaitwa **qadha**. Qadha na qadar vinatumika kwa maana moja. Kulingana na hili qadha maana yake ni makadirio ya Allahu taala ya tangu azali juu ya vitu vitakavyoumbwa kuanzia mwanzo hadi mwisho wa dunia. Na kadari maana yake ni vitu vyote kuumbwa bila kuzidi au kupungua kwa mujibu wa qadha. Allahu taala alijua mwanzo kila kitu kitakachotokea. Elimu yake hii inaitwa **Qadha na Qadar**. Wanafalsafa wa kigiriki walisema hii ni inayet-I ezeliyye (neema ya milele). Viumbe wote walitoka kwenye qadha hiyo. Pia kuumbwa kwa vitu kutokana na elimu yake ya zamani inaitwa qadha na qadar. Ili kuamin kadar tunafaa kujua na kuamini kwamba Allahu taala

ikiwa alitaka kuumba kitu huku nyuma, basi bila shaka kitatokea kama alivyotaka, kwa kiwango kidogo au kwa wingi, haiwezekani kutotokea kitu alichotaka kuumba wala kutokea ambacho hakutaka kuumba.

Wanyama wote, mimea, viumbe visivyo na uhai [vigumu, kioevu, gas, nyota, molekuli, atomi, elektroni, mawimbi ya sumaku na umeme, kwa ufupi kila mwendo wa kila kiumbe, matukio ya kimwili, athari za kemikali na nyuklia, nishati, matukio ya fizioloji kwenye viumbe hai] kuepo au kutokuepo kwa kila kitu, matendo mema na mabaya ya binaadamu, kuadhibiwa kwao hapa duniani, na baadae na kila kitu kilikuwepo kwenye elimu ya Allah ya daima. Alijua kila kitu zamani. Vitu vinavyotokea kutoka kwenye umilele mda uliopita hadi milele ya baadae, upekee wake, matembezi yake na kila tukio yanaumbwa na yeye kulingana na yale aliyoyajua mwanzo. Matendo yote mema na mabaya ya binadam, Imani zao au ukafiri wao, matendo yao yote, yanayofanywa kwa hiyari au bila hiyari, yanaumbwa na Allahu taala. Ndio yeye pekee anayeumba na kufanya kila kitu kutokea kwa njia ya as'bab. Anaumba kila kitu kupitia baadhi ya njia (as'bab).

Kwa mfano, moto unavyowaka, kwa uhakika Allah ndiye anayeufanya uchome. Moto hauna athari yoyote kuhusiana na kuchoma. Lakini desturi ni kwamba moto usipoungana na kitu, basi hautengenezi kuchoma. [1] Anayechoma ni Allahu taala pekee.

---

[1] Moto haufanyi kitu zaidi ya kutoa joto. Sio moto unaounganisha kabon na haidrojeni na oksijeni ndani ya dutu za kikaboni au kusambaza harakati za elektroni. Wale ambao hawawezi kuona ukweli wanadhani moto unafanya hivi. Anayechoma, anayefanya kitendo cha kuchoma, sio moto. Wala sio oksijeni. Wala sio joto. Wala sio harakat za elektroni. Anayechoma ni Allahu taala pekee. Haya yote, ameumba ili yaweze kuwa sababu za kuchoma. Mtu asiokua na elimu, anadhani moto unachoma. Mtu aliemaliza skuli ya msingi, hasemi 'moto unachoma' bali anasema 'hewa inachoma'. Na mtu anayemaliza sekondari pia hakubaliani na hili, anasema hewa ilipo kwenye oksijeni ndio inachoma. Tena mtu aliemaliza high school, anasema kwamba kuchoma hakuhusiani na oksijeni tuu lakini kila kipengele kinachovutia elektroni kinachoma. Lakini aliyemaliza chuo kikuu anazingatia nishati na dutu pamoja. Inaonekana kwamba mtu anaposoma na kujua Zaidi anapata kufahamu kwa kina kwamba sababu

Anaweza kuchoma bila moto pia, lakini ni desturi yake kuchoma kwa moto. Asipotaka kuchoma, anazuia kuchoma hata ndani ya moto. Hakumchoma Ibrahim "alaihis-salaam" kwenye moto kwa sababu alimpenda sana, aliachilia mbali desturi yake. [Bila shaka, anaumba dutu kusababisha moto usichome. Wakemia wamevumbua dutu hizi.]

Allahu taala angependa angeumba kila kitu bila sababu, kuchoma bila moto, tungeshiba bila kula. Kuruka bila ndege. Kusikia habari kutoka masafa marefu bila radio. Lakini kwa neema zake juu ya waja wake ameumba kila kitu na kukiwezesha kutokea kwa sababu. Alitaka kutengeneza vitu maalum kupitia sababu maalum. Alificha kazi zake chini ya sababu zake. Uwezo wake aliuweka chini ya sababu zake. Yule anayemtaka kumtengenezea kitu basi ni lazima atafute sababu za kitu hicho na atafanikiwa. [Anayetaka kuwasha taa anatumia kibiriti. Anayetaka kutoa mafuta kwenye zaituni anatumia machine ya kusaga. Anayeumwa kichwa anatumia aspirin. Anayetaka kuingia peponi na kupata neema zisizo na kikomo anajiunganisha na Uislam. Anayejipiga risasi na bastola anakufa. Anayekunywa sumu anakufa. Anayekunywa maji wakati anajasho anahatarisha afya yake. Anayetenda maovu na kupoteza imani yake anakwenda Jahannam. Kila sababu inayofuatwa, basi sababu hiyo itakuwezesha kupata kile ilichoumbiwa. Anayesoma vitabu vya kiislam, anajifunza Uislam, na anaupenda kisha anakuwa Muislam. Anayeishi pamoja na wasio na dini na wasio na madhehebu na kusikiliza maneno yao anakuwa mjinga wa dini. Wengi ya hao wasiojuwa dini wanakuwa kafiri. Mtu akipanda chombo chochote basi anakwenda huko kinakoelekea].

Ingekuwa Allahu taala hajafanya kazi zake kwa kuziwekea sababu, basi watu wasingehitajiana. Kila mtu angeomba kila kitu moja kwa moja kutoka kwa Allah bila kupitia kitu chochote. Hali ikiwa hivi, watu kati yao kiongozi, raia, mfanya kazi, fundi,

---

moja haifanyi kitu kutokea. Mitume "alaihimus-salaam" ambao walikuwa kwa daraja la juu la elimu na sayansi na ambao walikuwa na uwezo wa kuona kila kitu kwa ukweli wake, na wanazuoni wa kiislam, waliofuata nyayo zao, walipata matone kutoka kwenye bahari ya elimu yao, walisema kwamba leo vitu vinavyodhaniwa kuchoma, vina sababu na muumbaji ambaye ni Allahu taala.

mwanafunzi, mwalimu na kadhalika uhusiano usingekuepo, sheria za duniani na akhira nazo zingeharibiwa. Isingekuepo tofauti kati ya mrembo na mwenye sura mbaya, kizuri na kibaya, mtiifu na muasi kati yao isingeonekana tofauti.

Allahu taala angelipenda, angefanya desturi zake kwa mfumo mwengine. Kila kitu alikiumba kulingana na desturi hiyo. Kwa mfano, angelikuwa amependa, angewatia peponi makafiri, wale wanaofuata matamanio yao duniani wale wanaoumiza wengine na wanaodanganya wengine, na angewatia waumini, wanaoabudu na wema kwenye Jahannam. Lakini aya na hadithi zinaonesha kwamba hakutaka hivyo.

Allah ndie anayeumba vitendo vya binadamu wote. Mja ili aweze kufanya harakati anazotaka, ndani mwake ameumbiwa **ihtiyar na irada**, na anatenda kulingana na matakwa yake kwa sababu ana irada. Mtu anapochagua na kutaka kufanya jambo, Allah naye anaumba jambo hilo akitaka. Mtu asipotaka na asipotamani, Allahu taala pia asipopenda, basi haumbi kitu hicho. Kitu hicho hakiumbwi tuu kwa sababu ya matumaini ya mtu. Kuumbwa kwa kitu anachokitaka mtu ni kama moto unaposhukia kitu anaumba hali ya kuchoma na kuwaka. Kisu kikigusa kitu anaumba kitendo cha kukata. Sio kisu lakini mkataji ndio yeye. Amefanya kisu kuwa sababu ya kukata. Kwa maneno mengine, anaumba vitendo vya mtu vya hiyari kwa sababu ambayo anataka, anapendelea kwa vitendo hivi. Hata hivyo, harakati kwenye maumbile haitegemei hiyari ya mtu. Haya Allahu taala pekee akitaka, inaumbwa kwa kutumia sababu nyengine. Hakuna muumbaji zaidi yake. Yeye pekee anaumba mwenendo wa kila kitu, wa jua, chembe chembe, matone, seli, wadudu na atomi, dutu zao na tabia. Hata hivyo kuna tofauti kati ya harakati za dutu zisizo hai na vitendo hiyari vya mtu na wanyama: mtu au mnyama anapotaka kufanya, kupendelea na kutamani kitu naye Mungu akipenda pia, anamfanya mtu au myama kutenda na Allah anaumba kitendo chake.

Vitendo vya mtu haviko juu ya nguvu zake. Kwa uhakika hajui hata namna vinavyofanyika. [Kila harakati za mtu zinatokana na sababu za kimwili na kikemikali.] Hakuna hiyari katika harakati za visivyo hai. Allah ameumba kuchoma kwa moto unapogusa kitu, na

sio kwa njia ya moto kutaka kuchoma ndio unachoma.[1] Vitendo vya mtu vya hiyari vinatokana na hali aina mbili. Ya kwanza chaguo la moyo wake, matakwa na nguvu inahusishwa. Ndio sababu vitendo vya mtu huitwa **kasb** (kujipatia) ambayo ni sifa ya mtu. Ya pili, uumbaji wa Allah unatokea. Amri yake Allahu taala, makatazo, thawab na adhab vyote vinatokana na kasb aliopewa binaadamu. Kwenye aya 96 ya sura as-Saaffat, Allah anasema; **"Allah Alikuumbeni na aliumba vitendo vyenu".** Aya hii inaonyesha upatikanaji wa hiyari ya moyo na **iradat juz'iyya** katika kasb ya watu. Inathibitisha wazi kutopatikana kwa ulazima. Ndio kwanini inasemwa kuwa "vitendo vya mtu" kwa mfano, inasemwa Ali kapiga, kavunja. Lakini ni hakika kwamba kila kitu kimeumbwa kwa qadha na qadar.

Ili kitendo cha mtu kifanywe na kuumbwa, hiyari ya moyo na makadirio yake lazima yawepo kwanza. Mtu anakadiria vitu vilivyomo ndani ya uwezo wake. Kadirio hili au tamanio hili linaitwa **kasb** (kujipatia). Marehemu Amidi alielezea kwamba kasb inahusika na kuumbwa kwa vitendo. Hata hivyo, kusema kwamba kasb haina uhusiano na vitendo hiyari haina ubaya kwa sababu vitendo vinavyokadiriwa na mtu na vile vinavyoumbwa havitofautiani. Hivyo mtu hawezi kufanya chochote anachotaka, vitu asivyotaka navyo vinaweza kutokea pia. Endapo mtu angekuwa na uwezo wa kufanya kila anachotaka na kile asichotamani kikakosa kutokea basi asingekuwa mtu bali angedai uungu. Allahu taala aliwahurumia na

---

[1] Allahu taala pia anataka na anaumba mazuri, yenye faida kwa waja wake anaowapenda na kuwahurumia. Hapendi au kuumba mabaya na hatari kwao. Matendo mazuri na yenye faida daima yanatendwa na waja wanaopendwa. Kuna vitu vingi wanavyojutia kwa kushindwa kuvifanya lakini wangejua na kufikiria kwamba vitendo hivyo havijaumbwa kwa sababu vingekuwa hatari kwao, basi wasingeyajutia hata kidogo. Badala yake wangefurahi na kumshukuru Allah, ambaye alikadiria zamani kwamba ataumba vitendo vya binaadamu vya hiyari baada ya nyoyo zao kutamani na kuwa na nia ya kuwifanya; Alikadiria vile. Asingekuwa amekadiria hivyo zamani, angekuwa daima anaumba hata hiyari zetu kwa nguvu, bila hiyari, bila sisi kuzitamani. Kuumba kwake hiyari zetu baada ya kuzitamani ni kwamba alishakadiria zamani. Sasa sababu kubwa kwa kila kitu kutokea ni (Irada) makadirio yake.

kuwaneemesha waja wake na akawapa nguvu na uwezo kiasi wanachotaka ili kutekeleza amri zake na makatazo yake. Kwa mfano, mtu tajiri na mwenye afya nzuri anaweza kuhiji mara moja maishani mwake, anaweza kufunga mwezi mmoja anapouona mwezi wa Ramadhani mbinguni, anaweza kusali sala tano kila siku, anayemiliki pesa nyingi au mali kama nisab baada ya mwaka kupita anatoa robo ya dhahabu au fedha kwa Waislamu kama zakat.

Hivyo mtu anafanya vitendo kwa hiyari yake anapotaka na hafanyi asipotaka. Allahu taala ukubwa wake unatambulika hapa pia. Kwa sababu wajinga na wapumbavu hawawezi kufahamu elimu ya qadha na qadar, hawaamini kile walichosema wanazuoni wa Ahl as-Sunna na kuwa na shaka kuhusu uwezo na hiyari ya mtu. Wanafikiri kwamba mtu hana hiyari katika kufanya kitu bali analazimishwa. Baada ya kuona kwamba mtu hana hiyari kwenye mambo mengine wanawarushia maneno wanazuoni wa Ahl as-Sunna. Maneno yao mabaya haya yanaonesha upatikanaji wa irada na hiyari kwao.

Uwezo wa kufanya au kutofanya kitu unahusiana na **qudra** (nguvu). Kupendekeza, kuchagua kufanya au kutofanya kitu kunaitwa **ikhtiyar** (chaguo). Kutamani kufanya ulichochagua ni irada. Kukubali kufanya kitu au kutokanusha kunaitwa **ridhaa** (kuridhia). Nguvu na irada vikiungana pamoja na irada kufanya kitu kwa ufanisi inaitwa **Khalq** (kuumba) kunatokea. Vikiungana bila ufanisi inaitwa **kasb** (kujipatia). Kila mwenye hiyari sio lazima awe muumbaji. Vilevile kila kilicho kadiriwa sio lazima kikubalike. Allahu taala anaitwa Khaliq (muumbaji) na Mukhtar (mwenye hiyari), na mtu anaitwa kasib na mukhtar.

Allahu taala anakadiria na kuumba ibada (vitendo vya kuabudu) na maovu ya waja wake. Haliyakua anapenda ibada na anachukia maovu. Kila kitu kinatokea kwa irada yake na kuumba kwake. Kwenye aya ya 102 ya sura al-An'am anasema; **"hakuna Mungu isipokua yeye. Yeye pekee ni muumbaji wa kila kitu".**

Kundi la **Mu'tazila**, kwa kushindwa kuona tofauti kati ya irada na ridhaa, walichanganyikiwa na kusema: "mtu mwenyewe anaumba vitendo atakavyo". Walikanusha qadha na qadar. Kundi la jabariyya nao walichanganyikiwa, hawakujua kwamba hiyari inaweza kuwepo bila uumbaji. Kwa kufikiria kwamba mtu hana

hiyari walimfananisha na jiwe na kuni. Walisema kwamba watu kamwe hawana makosa. Walisema Allahu taala ndiye anayesababisha maovu kufanywa. Isingekuepo irada na hiyari kwa watu na Allahu taala angekuwa anafanya maovu na mabaya kwa nguvu kama wanavyodai kundi la jabariyya, isingekuwepo tofauti yoyote kati ya mwendo wa mtu anayetupwa chini kutoka juu ya mlima wakati amefungwa mikono na miguu yake na mwendo wa yule mtu anaeshuka kwa kutembea wakati anaangalia hapa na pale. Ukweli ni kwamba mtu wa kwanza anakwenda kwa nguvu (analazimishwa hana chaguo) lakini wa pili anakwenda kwa hiyari yake. Watu wasioona tofauti kati yake hawaoni mbali. Na wanakuwa hawaja amini aya tukufu pia. Wanayachukulia maamrisho na makatazo ya Allahu taala kutofaa na kutokuwa chochote. Kudhania kama walivyosema Mu'tazila au Kadariyya kwamba mtu anaumba vitendo vyake mwenyewe basi ni kutoamini aya tukufu, inayosema **"Allahu taala pekee ndio muumbaji wa kila kitu,"** na kusema kwamba mtu ni msaidizi wa Allahu taala.

Mashi'a nao wanasema kama Mu'tazila kwamba mtu anaumba vitendo vyake anavyotaka. Kujenga hoja yao wanatoa mfano wa punda kwamba hata akipigwa viboko havuki maji. Hawa hawafikirii kwamba mtu akitaka kufanya kitu, Allahu taala naye asipotaka kitu hicho kifanyike, basi alichotaka Allahu taala ndio kitakuwa. Hapo inafahamika kwamba maneno ya Mu'tazila yanakuwa sio sahihi. Yaani binadamu, kila anachotaka hakifanyi wala hakiumbi. Ingekuwa kama walivyosema wao kwamba binadam kila anachotaka kinatokea basi Allahu taala angekuwa ameshindwa. Allahu taala yuko mbali na kushindwa yaani Hashindwi. Hata hivyo irada yake inakuwa. Ndiye pekee anaeumba kila kitu. Na hivyo alivyo Allahu taala. Kwa watu kusema kama "mtu aliumba hiki," "tumeumba hiki," au "waliumba hiki" ni maneno mabaya. Inakuwa tabia mbaya dhidi ya Allahu taala. Na inasababisha ukafiri.[1]

---

[1] Kama ilivyoelezwa juu, harakati za binadamu za hiyari, vitu vinavyotokea bila hiyari yake, hata vile ambavyo hajapata kusikia, vinatokana na matukio ya kimwili, kikemikali na fiziolojia. Mwanasayansi aliyesoma na kufahamu vizuri anaona haya mbele ya Mungu kusema "nimefanya hiki" au "nimeumba hiki" kuhusu vitendo vyake vya hiyari. Lakini mtu mwenye elimu ndogo, uelewaji na tabia, haoni haya kusema chochote katika

Tafsiri ya kitabu **Itiqad-nama** inafikia hapa. Haji Fayzullah Efendi, mwenye kufanya tafsiri hii, alikuwa anatoka Kamah, mji wa Erzincan, Alifundisha kama professor kwenye mji wa Soke (Uturuki) kwa miaka mingi, na alifariki dunia mwaka 1323 H. (1905 M.). Mawlana Khalidi Baghdadi Uthmani 'quddisa sirruh', mtunzi wa kitabu alizaliwa 1192 H. kwenye mji wa Shahrazur, kaskazini mwa mji wa Baghdadi, na alifariki dunia kwenye mji wa Damascus mnamo mwaka 1242 H. (1826 M.). Anaitwa 'Uthmani kwa sababu anatoka kwenye kizazi cha Hadhrat Uthman Zannurayn "radiyallahu anhu". Alipokuwa anamfundisha kaka yake Mawlana Mahmud Sahib kuhusu hadithi ya pili kwenye kitabu cha Imam Nawawi **Hadith-I Arbain**, hadithi maarufu kama **Hadithi Jibril**, Mawlana Mahmud Sahib alimuomba kaka yake kuandika ufafanuzi wa hadithi hii. Mawlana Khalid "rahmatullahi alaih" alikubali ombi hili ili kufurahisha moyo wa kaka yake na akafafanuwa hadithi hii kwenye lugha ya kiajemi.

## BARUA YA SHARFUDDIN MANERI "rahmatullahi alaih"

Sharfuddin Ahmed bin Yahya Maneri alikufa mwaka (782 H./ 1380 M.), ni mmoja wa wanazuoni wa kiislam waliopata elimu India, aliandika kwenye barua ya 18 kwenye kitabu chake cha kiajemi **Maktubat:**

---

sehemu yoyote. Allahu taala anahuruma juu ya watu wote duniani. Anaumba kila wanachotaka na kuvituma kwa kila mtu. Anawaeleza mambo mengi yanayofaa kufanya ili waweze kuishi kwa Amani na furaha hapa duniani, na kupata furaha ya milele baadae kwenye maisha yajayo. Anaongoza kwenye njia sahihi kila anayemtaka miongoni mwa wale walioacha njia sahihi na kufuata njia ya ukafiri na ya uzushi baada ya kudanganywa na nafsi zao wenyewe (matamanio), marafiki wabaya, vitabu hatari na mitandao. Anawavuta kuwaelekeza njia sahihi. Lakini neema hii hawapi wale waliopindukia na kupita kikomo, Anawaacha ndani ya bwawa la ukafiri ambapo walianguka na wakapendelea na kutoamini.

“Watu wengi wanakosea kwa kutegemea kwenye dhana na njozi. Baadhi ya watu wenye dhana mbovu wanasema ‘Allahu taala hana haja na ibada zetu. Ibada zetu hazimsaidii. Watu kumuabudu au kumuasi havibadilishi kitu dhidi ya ukubwa wake. Wanasema watu wanaofanya ibada wanajisumbua na kujichosha bure. Kufikiria namna hii sio sahihi. Kutofahamu kwao Uislamu wanasema hivyo. Wanadhani ibada zimeamrishwa kwa sababu zina faida kwake Allah. Dhana hii ni mbaya sana. Ni kama kufikiria kisichowezekana kuwezekana. Ibada yoyote inayofanywa na mtu anafaidika yeye tu. Allah anaeleza wazi wazi kwenye aya ya 18 ya sura Fatir kwamba ndivyo ilivyo. Mtu mwenye fikra mbovu kama hizi ni kama mgonjwa anayepewa utaratibu wa mlo na daktari lakini hafuati utaratibu huo na kusema, ‘nisipofuata utaratibu hautomuathiri daktari.’ Ni kweli kusema kwamba daktari hatoathirika, ila muathirika ndio yeye binafsi. Daktari anampa utaratibu wa mlo sio kwamba daktari anafaidika lakini ni kutibu ugonjwa wa mgonjwa. Anapofuata nasaha ya daktari basi atapona. Na asipofuata, atakufa na kwenda zake, na hili halitomuathiri daktari kabisa.

Baadhi ya makundi yenye fikira mbovu nao, hawajafanya ibada hata kidogo na hawajikingi dhidi ya maovu, yaani hawaufuati Uislam. Wanasema ‘Allah ni mkarim, mwenye rehma. Anawahurumia waja wake sana. Msamaha wake hauna kikomo. Hatomuadhibu mtu yoyote.’ Kweli maneno yao ya kwanza ni sahihi lakini wamekosea kwenye maneno ya mwisho. Hapa shetani anawadanganya na kuwavutia maasi. Mwenye akili hadanganywi na shetani. Allahu taala kama alivyo mkarimu, msamehevu, adhabu zake pia ni kali mno. Anawachoma watu. Tunaona hapa duniani anavyowafanya wengi kuishi kwenye umasikini na matatizo, anawafanya waja wake wengi kuishi kwenye adhabu bila kusita, Ingawa ni mkarimu sana na ni Razzaq (mgawaji wa riziki), hatotoa hata mkate mmoja hadi pale mazao na kilimo vitakaposhugulikiwa. Ingawa ndiye anayewafanya watu wote kuwa hai, hatomkubalia mtu kuishi bila kula na kunywa. Hatompa shifaa mgonjwa ambae hatumii dawa. Anaumba sababu kwa neema za ulimwengu wote kama kuishi, kutopata maradhi, kumiliki mali, na hasiti kuwanyima neema hizi wale ambao hawatafuti sababu za kuwawezesha kupata neema hizo. Kuna aina mbili za dawa: dawa za kimali na dawa za kiroho. Dawa ya kiroho inayotibu kila ugonjwa, ni kutoa zaka na

kuomba dua. Hadithi mbili mashuhuri zinazohimiza hili, **“tibuni ugonjwa wenu kwa kutoa zaka”** na **“kusoma sana istighfar, ni dawa ya magonjwa yote.”** Dawa za kimali ni nyingi sana, inahitaji uzoefu kuzijua. Kwa kutumia dawa za kiroho kunasaidia kutafuta dawa za kimali pia. Kupata neema za akhira ni kama hivyo. Alifanya ukafiri, uwe sumu inayoua roho namoyo, na uzembe unafanya moyo kuumwa. Dawa isipotumika moyo utaumwa na kufa. Dawa pekee ya ujinga na ukafiri ni elimu na maarifa. Na dawa ya uzembe ni kusali sala na kufanya ibada za kila aina. Hapa duniani, mtu anapokunywa sumu na halafu akasema, ‘Allah ni mwenye rehma, na atanikinga dhidi ya hatari ya sumu,’ atakuwa mgonjwa na atakufa. Mtu mwenye kuharisha akinywa mafuta ya kupikia au (mwenye kisukari akila vitamu au vyakula vya wanga), ugonjwa utazidi. Kwakuwa mwili wa binadamu ni nyeti, vitu vilivyo lazima ni vingi [kama chakula, mavazi na makazi]. Hivi kuvipata na kuvitumia kama inavyostahiki kulingana na Uislam, ni vigumu kujiandaa. Vitu hivyo ili vitumike kirahisi na kwa raha, uwezo unaoitwa **Nafs** umeumbwa ndani ya mtu. Hakuna sababu ya kuumba uwezo huu kwenye wanyama. Nafs inataka vitu vilivyo lazima kwa mwili vifanywe. Nafs inafurahia kufanya vitu hivyo kwa kupita kiasi. Matakwa ya Nafs inaitwa **Shahwa**. Shahwa isiposhauriana na akili, na ikafanya kupita kiasi kinachotakikana, inahatarisha moyo na mwili na wengine na linakuwa kosa. Angalia kwenye **Endless Bliss** (Furaha bila kikomo) ukurasa wa 32.

Kundi lengine lenye fikira mbovu nalo wanafanya **riyada** kwa kujiumiza njaa. Hivyo wanataka kuondoa chanzo cha shahwa, hasira na burudani zao ambazo haziendani na Uislamu. Wanadhani Uislam unaamrisha kuziondoa. Baada ya kukaa mda mrefu na njaa wanajikuta matamanio yao mabaya hayajaondoka, na mwisho wanasema Uislam uliamrisha kitu ambacho hakiwezekani. Wanasema: **‘Amri ya Uislam hii haifanyiki. Mtu hawezi kujiokoa kwa kitu alichoumbwa nacho. Kujaribu kujiokoa kwa haya ni kama kujaribu kumfanya mtu mweusi kuwa mweupe. Kufanya kitu kisichowezekana ni kupoteza umri wa mtu bure.’** Wanafikiria vibaya na wanafanya kazi mbaya. Hata hivyo, kusema kwao kwamba Uislam unaamrisha hivi ni ujinga mkubwa na upumbavu. Kwasababu Uislam hauamrishi kuondoa sifa za kitu kama hasira, shahwa. Kusema hivyo basi ni kuusingizia Uislam. Ingekuwa Uislam umeamrisha hivi basi Muhammad "alaihis-salaam" mwenye dini ya

Uislam asingekuwa na sifa hizi. Kwa kweli, alisema: **‘mimi ni binadamu pia kama wengine, nami nakasirika.’** Mara kwa mara alionekana amekasirika. Kukasirika kwake mara zote kulikua kwa ajili ya Allahu taala. Allah anawasifu watu **‘wanaoshinda hasira zao’** kwenye Quran tukufu sura aali-Imran aya ya 134. Hawasifu wasiokasirika. Mtu mwenye fikira mbaya, kusema kwake kwamba mtu anafaa kuondoa shahwa yake ni uongo mkubwa. Kitendo cha mtume "swallallahu alaihi wa sallam" kuoa wake tisa, kinaonesha wazi kwamba maneno ya mtu huyu ni uongo. Mtu akipoteza shahwa yake anairejesha kwa kumeza dawa. Hasira nazo ziko hivyo. Mtu anatumia sifa ya hasira kulinda mkewe na watoto wake. Dhidi ya maadui wa Uislam kwa msaada wa sifa hii jihad inafanyika. Kupitia shahwa, mtu mwenye watoto anasifiwa na kuheshimiwa baada ya kifo chake. Hivi ni vitu vilivyopendwa na kusifiwa na Uislam.

Uislam hauamrishi kutokomeza shahwa na hasira lakini unaamrisha vyote viwili kuviendesha na kuvitumia kama ulivyosema Uislam. Ni sawa na mpanda farasi au mbwa wa kuwinda. Sio lazima kuacha farasi au mbwa lakini kuwafuga kuweza kunufaika na faida zao. Yaani shahwa na hasira ni kama mbwa wa muindaji na farasi na mpanda farasi. Bila ya hivi viwili neema za akhera hazishindwi. Lakini ili kunufaika kutoka kwa hivi, ni lazima kuchukuwa mafunzo yanayofaa kama ya Uislam. Yasipochukuliwa mafunzo, yakapindukia kiasi na kuvuka mipaka, yanampeleka mtu kwenye hasara. Kufanya riyadha, sio kutokomeza sifa mbili hizi, lakini kuzipa mafunzo na kuzifanya kufuata Uislam. Na hili linawezekana kwa kila mtu. Ustaraabu sio kutumia nguvu za atomic na kufanya vitu kama ndege za kivita. Ustaarabu ni kutumia hivi kuwahudumia watu. Na haya yanatumika kwa kufuata Uislam.

Tukija kwenye kundi lenye fikira mbaya la nne, hawa wanajidanganya wenyewe wanasema: **(kila kitu kishakadiriwa zamani. Mtoto kabla hajazaliwa, ni wazi kwamba atakuwa Sa’id (mwema) au Shaqi (sio mwema). Hii haitabadilika baadae. Kwa hivyo hakuna haja ya kufanya ibada)**. Mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alipokuwa anaelezea qadha na kadar kutobadilika na kwamba kila kitu kishakadiriwa zamani, masahaba nao walisema hivi (yaliokadiriwa zamani tunayaamini. Tusifanye ibada). Lakini mtume "swallallahu alaihi wa sallam" aliwajibu kwamba, **‘Fanyeni ibada! Ni rahisi kwa kila mtu kufanya kile alichokadiriwa zamani’**.

Yaani mtu aliekadiriwa kuwa sa'id zamani duniani anafanya vitendo vya sa'id. Kutokana na haya inafahamika kwamba, watu waliokadiriwa kuwa sa'id zamani walitekeleza ibada na wale waliojaaliwa kuwa shaqi walimuasi Allahu taala ni sawa na ukweli kwamba watu waliojaaliwa kuishi na afya nzuri wanakula chakula na wanameza dawa na wale waliojaaliwa kuwa wagonjwa na kufa hawali na hawamezi dawa. Watu ambao hatima yao ni kufa kwa njaa au ugonjwa hawawezi kufaidika na chakula au dawa. Njia za kupata mali ziko wazi kwa mtu aliejaaliwa kuwa tajiri. Mtu aliejaaliwa kifo chake mashariki basi njia zinazompeleka magharibi zinafungwa. Kulingana na tunayosikia, Izrail "alaihis-salaam" alipomtembelea nabii Sulaiman "alaihis-salaam" alimuangalia kwa umakini mmoja kati ya waliokuwepo naye. Huyu mtu alipata hofu kutokana na macho ya Malaika Izrail. Alipokwenda huyu mtu akamuomba nabii Sulaiman "alaihis-salaam" kuamrisha upepo kumpeleka kwenye moja kati ya miji ya magharibi ili aweze kumkimbia Izrail "alaihis-salaam". Izrail "alaihis-salaam" aliporudi, Sulaiman "alaihis-salaam" alimuuliza kwanini alikuwa anamuangalia mtu yule kwa uchungu. Izrail "alaihis-salaam" alisema, 'nimeamrishwa kuchukuwa roho yake huko magharibi baada ya saa. Lakini nilipomuona kwenye kundi lako, sikukatisha kumwangalia kwa kushangaa. Baadae nilikwenda zangu magharibi kutekeleza amri na nikamuona huko nikachukua uhai wake. [Kisa hiki Jalal ad-Din Rumi amekieleza kwa urefu katika kitabu chake Mathnawi, alikufa mnamo mwaka 672 H. (1273 M.) Konya/Uturuki.] Inaonekana kwamba makadirio ya zamani sio amri lakini ni Elimu. Angalia ukurasa wa hamsini na saba! Mtu huyu alimuogopa Izrail "alaihis-salaam" ili kutimiza makadirio ya zamani. Sulaiman "alaihis-salaam" naye alitii amri hiyo. Makadirio ya zamani yalitekelezwa kwa njia ya mtiririko wa sababu. Vile vile mtu aliejaaliwa kuwa sa'id (mwema) zamani atapata neema ya kuwa na iman na kurekebisha vitendo vyake vibaya kupitia riyadha. Aya ya 125 sura al-An'am inasema: **'Basi yule ambaye Allahu taala anataka kumuongoza anauweka Uislam kwenye kifua chake.'** Mtu aliekadiriwa kuwa shaqi zamani, tuseme aliejaliwa kwenda motoni, anapata wazo kwamba, 'hakuna haja ya kufanya ibada. Ilishajaaliwa zamani kwamba mtu atakuwa sa'id au shaqi.' Hatekelezi ibada kwa sababu ya wazo hili. Kutotekeleza kwake ibada kwa sababu ya wazo hili inaonyesha kwamba alijaaliwa kuwa shaqi zamani. Vile vile mtu

aliejaliwa ujinga anapata wazo kwamba ‘kila kitu kishajaaliwa zamani. Kusoma au kujifunza hakutokuwa na faida kwa mtu kama alijaaliwa kuwa mjinga. Kwa hivyo hasomi wala hajifunzi kitu chochote. Anabaki mjinga. Kama mtu alijaaliwa kupanda na kuvuna mazao mengi, anapata nguvu za kupanda mbegu kwenye shamba lake. Kwa hali hii ni sawa na wale waliojaaliwa kuwa sa’id zamani wanapata imani na kuabudu na wale waliojaaliwa kama shaqi wanakanusha na kuasi. Wapumbavu, kwa kushindwa kuelewa haya, wanasema, ‘imani na ibada vina uhusiano gani na kuwa sa’id zamani, au ukafiri na uasi na kuwa shaqi?’ Kwa hoja zao fupi, wanajaribu kufahamu hili kwa kulinganisha na kutatua kila kitu kwa kutumia akili zao. Lakini hoja ya binadamu ni ndogo, na ni ujinga au upumbavu kujaribu kuelewa vitu vilivyo zaidi ya hoja. Wale wanaofikiria hivyo wanafaa kuhukumiwa kuwa wapumbavu. Issa "alaihis-salaam" anasema kwamba, kuwaponyesha waliozaliwa wakiwa vipofu, hata kufufua waliokufa uwezo haukuwa wangu, lakini sikuweza kumueleza mjinga ukweli wa maneno haya. Allahu taala kwa elimu yake isiyo na kikomo na hikma yake anawapandisha daraja baadhi ya waja wake hadi daraja la malaika. Hata wanawapita malaika. Baadhi yao wanashushwa vyeo vyao pia na kuwa kama mbwa na nguruwe. Tafsiri ya barua ya kumi na nane inaishia hapa. Kitabu cha hazrat Sharfuddin Ahmed bin Yahya Maneri cha **Maktubat** kuna barua mia moja. Zilikusanywa mwaka 741 H. [1339 M.] na kuchapishwa mwaka 1329 H. [1911 M.] India.

Istanbul nako kwenye maktaba ya Sulaymaniyye nakala ilioandikwa kwa mkono ipo. Barua ya sabini na sita inasema kwamba: **‘Sa’ada’** maana yake ni ‘kustahiki pepo.’ Na **‘Shaqawa’** maana yake ni ‘kustahiki moto.’ Sa’ada na shaqawa ni kama hazina mbili za Allahu taala. Funguo za hazina ya kwanza ni utiifu na ibada. Funguo za hazina ya pili ni maasi yaani madhambi. Allahu taala alijua zamani nani atakuwa sai’d au shaqi. Elimu hii inaitwa **Kadar**. Mtu aliejulikana kwamba atakuwa sa’id (mwema) zamani basi anamtıı Allahu taala. Na yule aliyejulikana kwamba atakuwa shakii, mara kwa mara anatenda maovu. Duniani sai’d (mwema) au shaqi (muovu) anatambulika kutokana na vitendo vyake. Wanazuoni wanaofikiria kwenye akhera, hivi ndivyo wanavyofahamu sai’d na shaqi. Lakini watu wa dini waliozama na dunia hawaelewi hili. Kila heshima na Baraka vinapatikana kwa sababu ya kumuabudu Allahu taala. Kila mabaya na matatizo ni natija ya kutenda maovu. Shida

na balaa juu ya kila mtu yanatokana na kutenda maovu. Furaha na utulivu navyo vinapatikana kwa njia ya kumtii Allah.[1] Jerusalem kwenye msikiti wa Aqsa palikuwepo na mtu mmoja alieabudu kwa muda mrefu umri wake wote lakini kwa kutojifunza masharti ya ibada na ihlasi, alipoacha sujudi moja tu aliharibu na kuangamia. Hata hivyo mbwa wa As'habul kahfi hali ya kuwa mchafu lakini kwa sababu alitembea pamoja na watu wema (siddik) alipandishwa cheo ambacho hakikadiriki. Hali hii inawashangaza watu. Kwa karne nyingi wataalamu wameshindwa kutatuwa siri hii. Akili ya mtu haiwezi kufahamu hekima iliyomo. Adam "alaihis-salaam" alikatazwa kula ngano lakini alimuacha akala kwa sababu alijua mwanzoni kwamba ataila. Alimuamrisha shetani kumsujudia Adamu "alaihis-salaam" na alipendekeza kutomsujudia kwake. Alituamrisha tumtafute ila hakujaalia wale wasio na ikhlasi kumpata. Baada ya kusema njia ya Allah hatujaifahamu hawajasema kitu kingine. Inakuwaje sisi tuseme hana haja na Imani za watu na kufanya ibada kwao! Watu kuwa makafiri na utendaji maovu wao haumpi hasara. Hana haja na viumbe wake. Alifanya Elimu kuwa sababu ya kusafisha dhuluma, na ujinga kuwa sababu ya kutenda maovu. Elimu ni chanzo cha imani na twaat vile vile ujinga nao ni chanzo cha ukafiri na maovu. Twaat hata ikiwa ndogo basi isipotezwe! Na ovu hata likionekana dogo sana basi lisikaribiwe. Wanazuoni wa kiislam wanasema kwamba mambo matatu yanasababisha mambo matatu, Twaat ni sababu ya kupata radhi za Allahu taala. Kutenda maovu ni sababu ya ghadhabu za Allah. Kuwa na imani ni sababu ya kupata heshima na sifa njema. Kwa sababu hii tunafaa kuepuka sana kutenda maovu madogo pia. Hasira za Allah zinaweza zikatokea kwa sababu ya maovu. Kila muumini anafaa kuheshimiwa.

Muumini huyu anaweza akawa mja anayependwa na Allah. Makadirio ya kila mtu yaliofanywa mwanzoni kamwe hayabadilishwi. Muislam alietenda maovu tu na hakumtii Allah hata kidogo, Allahu taala akipenda atamsamehe. Sura al-Baqarah aya ya

---

[1] Hizi ndizo sheria za Allah tukufu. Hakuna anayeweza kubadilisha hili. Tusichukulie vitu vinavyoonekana vyepesi na vitamu kwa nafsi zetu kama sa'ada. Na wala tusifikirie vitu vinavyoonekana vigumu na vichungu kwa nafsi zetu kama shaqawa.

thelathini Malaika waliposema **(Ewe Mola! Kwanini unamuumba mtu ambaye atafanya ufisadi kwenye dunia na kumwaga damu)** Allahu taala hakusema kwamba hawatofanya ufisadi lakini Alisema **(najua msiojuwa nyinyi)**. Alimaanisha kwamba nafanya yanayostahiki kutoka kwenye yasiostahiki. Nasogeza yalioko mbali. Nawafanya kuwa wenye heshima wale wenye udhalilifu. Nyie mnaangalia kwenye matendo yao, Lakini mimi naangalia yaliomo kwenye nyoyo zao. Ninyi mnajiangalia kuwa hamtendi maovu, lakini wao wana imani na rehma zangu na wanaomba msamaha. Kama anavyotaka kutotenda maovu kwenu ndivyo anavyotaka kusamehe Waislamu madhambi yao. Hamjui ninavyovijua. Nawafanya waumini wapate neema zangu za milele. Tafsiri ya barua ya sabini na sita inaishia hapa.

Sharfuddin Ahmed bin Yahya Maneri "rahmatullahi alaih" alifariki mnamo mwaka 732 H (1380 M). Aliishi kwenye mji wa Bihar, India. Kaburi lake lipo huko pia. Maner ni moja ya jina la vijiji vilivyopo kwenye mji wa Bihar. Hali yake imeelezwa kwa urefu kwenye kitabu **Akhbarul akhyar** kilichoandikwa na Shah Abdulhaq Dahlawi "rahmatullahi taala". Kitabu hiki kipo kwenye lugha ya kiajemi, na kilichapishwa kwenye mji wa Diobend, India mwaka 1332 H. (1914 M), na baadae kwenye mji wa Lahore, Pakistan. Vitabu hivi; **Irshad-us-salikin**, **Ma'din-ul-ma'ani** na **Maktubat** ni vitabu muhimu sana.

Imam Rabbani "rahmatullahi alaih" kwenye vitabu vyake tofauti anasema kwamba, maamrisho ya Allahu taala yanaitwa **Farz**. Makatazo yake yanaitwa **Haram**. Yalioachwa wazi bila kubainishwa kwamba ni Farz au Haramu yanaitwa **Mubah**. Kitendo cha kufanya yalio farz na kuepuka yalio haramu na kufanya yalio mubaha kwa kumridhisha Allah kinaitwa **Ibada**. Ibada ili iweze kuwa sahihi na kukubaliwa, yani ikubaliwe na Allah, ni lazima upate **İlm** (elimu) yani kusoma masharti yake, halafu **Amel** (utekelezaji) yani kutekeleza ipasavyo pamoja na **Ikhlas** (ihlas) yani nia njema. Ikhlas, ni kufanya kitu bila kufikiria manufaa ya kidunia kama pesa, cheo, kupata umaarufu, lakini kwa kuwa ni maamrisho ya Allah, na kupata ridhaa yake na upendo wake. Elimu inapatikana kwa kusoma vitabu vya fiqh pamoja na ustadh, Ihlas nayo inapatikana kwa kusoma vitabu vya tasawwufu na kusikiliza maneno ya mawalii na hali zao na kufuata nyendo zao. Elimu katika Uislam ni ya aina mbili; elimu ya dini na elimu ya sayansi. Ni lazima kujifunza kutokana na mahitaji.

Kwa mfano; kujua matumizi na kipimo cha dawa na anayetaka kutumia umeme ni lazima kujifunza kabla. Asipojifunza inaweza kuwa sababu ya kifo.

Muislam asiefanya ibada kwa sababu ya uvivu au kwa kuwafuata marafiki wabaya akifa bila kutubu, hata akiwa anaamini farz na haram, atachomwa kwenye Jahannam kadir ya madhambi yake. Mtu asipojifunza farz, au akazijua lakini akakosa kuzipa thamani na kuzipa umuhimu, bila ya kusikitika na kumuogopa Allah, basi mtu huyu anatoka kwenye Uislam na anakuwa kafiri. Atachomwa kwenye Jahannam milele. Na yule anayefanya haramu hali ni hiyo hiyo. Ibada inapofanywa bila kupata elimu kuhusu ibada hiyo haiwi sahihi hata mtendaji akiwa ametenda na ikhlas. Anakuwa kama hajafanya na atachomwa kwenye Jahannam. Ibada ikifanywa kwa kujua na kuzingatia sharti zake basi inakuwa sahihi. Mtendaji anaokolewa dhidi ya Jahannam. Lakini asipofanya na ihlas, ibada hii haitokubaliwa pamoja na matendo mengine. Na hawezi kupata thawabu. Inafundishwa kwamba ibada yake na wema wake na hasanati zake hazitokubaliwa na Allah. Ibada zinazofanywa bila elimu na ikhlas hazina faida. Ibada hizo haziwezi kumuokoa mtu dhidi ya ukafiri, dhambi na adhabu. Wanafiki wengi wanaofanya ibada hivi na kufa kama kafiri wameonekana maisha yote. Ibada zinazofanywa na elimu na ihlas, zinamuokoa mtu kutokana na ukafiri, madhambi na kumfanya mwenye heshima duniani. Pia kwenye siku ya kiama Allah aliahidi kumuokoa dhidi ya adhabu za Jahannam katika sura al-Maidah aya ya tisa na katika sura al-Asr. Ahadi ya Allah ni ya kweli. Ahadi anayotoa bila shaka anaitekeleza.

***Allahu taala naye analipiza kisasi kwa njia ya waja wake.***
***Kwa wale wasiokuwa na 'ilm-i-ladunni hudhania haya yametendwa na mja.***
***Kila kitu ndio muumbaji, lakini inatekelezwa na mikono ya waja.***
***Usidhani kitu hata kidogo kupiga hatua bila nguvu za Allah.***

# ALLAH YUPO NA NI MMOJA, ZAIDI YAKE VIUMBE VYOTE HAVIKUWEPO NA TENA VITATOWEKA.

Tunatambua vitu vilivyotuzunguka kwa kutumia viungo vya hisia. Vitu vinavyo athiri viungo vyetu vya hisia vinaitwa **matukio** au **viumbe**. Viumbe vinavyo athiri hisia zetu tano vinaitwa **tabia** au **sifa** na vinatofautishwa kwa njia hiyo hiyo. Mwangaza, sauti, maji, hewa na nyenzo za kioo vyote ni viumbe, vyote vipo. Viumbe vilivyo na kipimo, uzito, ujazo au kwa namna nyengine vinavyochukuwa nafasi kwenye uwazi vinaitwa **Dutu** au **maada**. Maada zinatofuautishwa moja na nyengine kulingana na tabia zao. Hewa, maji, jiwe na glass (kioo) ni maada tofauti. Mwangaza na sauti sio maada kwa sababu havichukuwi nafasi uwazini wala havina uzito. Kila kiumbe kina **nishati** yani **(uwezo)**, tuseme vina uwezo wa kufanya kazi. Kila maada ipo katika hali tatu: yabisi, kioevu na gesi. maada zilizopo kwenye hali ya yabisi zina umbo. Kioevu na gesi zinachukua umbo la chombo ambacho zimewekwa, na havina umbo rasmi. Maada yenye umbo inaitwa **dutu**. Maada daima zinakuwa kwenye hali ya dutu. Kwa mfano, funguo, sindano, makoleo na msumari ni vitu tofuauti vyenye umbo tofauti. Lakini vyote vinatoka kwenye maada moja, yaani chuma. Kuna aina mbili za dutu. Elementi na Mimumunyo.

Mabadiliko daima yanatokea kwenye kila kitu. Kwa mfano, kinaweza kutembea na kubadilisha mahali pake au kinakuwa kikubwa au kidogo. Kinabadilika rangi. Kama ni kiumbe hai kinapata ugonjwa na kufa. Mabadiliko haya yanaitwa **matukio**. Hakuna mabadiliko yanayotokea kwenye maada bila athari kutoka nje yake. Tukio linapotokea na kutofanya mabadiliko yoyote kwenye kiini cha maada linaitwa tukio la kiumbo. Kuchana karatasi ni **tukio** la **kiumbo**. Tukio la kiumbo kuweza kutokea kwenye dutu fulani lazima ipatikane nguvu inayoathiri dutu. Matukio yanayobadilisha muundo au kiini cha dutu huitwa **tukio** la **kikemikali**. Kuchomeka kwa karatasi na kuwa jivu, ni tukio la kikemikali. Ili tukio la kikemikali liweze kutokea kwenye dutu lazima dutu iathiriwe na dutu nyengine. Dutu mbili au Zaidi zinapoungana pamoja na tukio la kikemikali likatokea kwenye kila moja, basi hii inaitwa **Utendanaji wa Kikemikali.**

Utendanaji wa kikemikali kati ya dutu, tuseme, moja kuathiri nyengine unatokea kati ya kipande kidogo zaidi. Kipande hiki kiduchu cha dutu kinaitwa atomi. Kila kitu kimeumbwa kutokana na atomi. Yaani masi ya atomi. Hata hivyo muundo wa atomi unafanana lakini ukubwa na uzito wake ni tofauti. Kwa sababu hiyo, leo tunafahamu aina mia moja na tano za atomi. Hata atomi kubwa zaidi ni ndogo sana kiasi ambacho haiwezi kuonwa kwa kutumia maikroskop. Atomi zenye jinsia moja zikija pamoja zinatengeneza **elementi**. Kwa kuwa kuna atomi mia moja na tano, kuna elementi mia moja na tano pia. Kila chuma, salfa, zebaki, oksijen, na kaboni ni elementi. Atomi tofauti tofauti zikija pamoja zinaunda mmumunyo. Kuna mamia ya maelfu ya mimumunyo. Maji, pombe, chumvi na chokaa (lime) ni mimumunyo. Mimumunyo inatokana na kuungana kwa elementi mbili au zaidi. Inatokea pia kwa kuungana kwa atomi na elementi.

Kila dutu, kwa mfano; milima, bahari, aina zote za mimea na wanyama vyote vinatoka kwenye elementi mia moja na tano. Mawe yanayotengeneza dutu hai na zisizo hai ni kutokana na elementi mia moja na tano hizi. Dutu zote zinaundwa kutokana na mchanganyiko wa atomi moja au zaidi kati ya elementi mia moja na tano hizi. Hewa, udongo, maji, joto, mwangaza, umeme na vijidudu vinatenganisha mimumunyo au vinasababisha dutu kuungana pamoja. **Hakuna mabadiliko yanayotokea bila sababu**. Katika mabadiliko haya, elementi yani vijiwe vilivyotengeneza viumbe hivi vinahama kutoka kwenye dutu moja na kwenda nyengine au kuacha dutu na kuwa huru. Na tunaona dutu kutoweka. Lakini kwa kuwa tunatoa hukumu kulingana na tunavyoona tunakosea kwa sababu, kutoweka na kuwepo kama tunavyosema sio kitu zaidi ya mgeuzo wa maada. Kwa mfano maiti iliopo kaburini kutoweka kwake ni kugeuka kuwa dutu mpya kama maji, gesi na udongo. Mabadiliko yanapotokea kwenye maada bila kuathiri hisia zetu hatuwezi kufahamu kwamba mabadiliko yametokea. Ndio maana tunasema maada ya kwanza ilitoweka.

Tunaona kwamba umbo kutoka kwenye elementi mia moja na tano linabadilika na katika kila elementi hutokea tukio la kiumbo na la kikemikali. Elementi moja ikiungana na mmumunyo inaingia kwenye hali ya ion (ayoni). Yani atomi zake hupoteza au huongeza

elektroni. Hivyo tabia tofauti za kiumbo na za kikemikali za elementi hii hubadilika. Kila atomi ya elementi imeumbwa kutokana na kiini pamoja na vipande vidogo viitwavyo **Elektroni**. Kiini kipo kati kati ya atomi. Mbali na haidrojen, viini vya atom vimeumbwa kutokana na **protoni na nutroni**. Protoni inachukuwa umeme na nutroni haichukuwi umeme. Elektroni ni chembe chembe zisizochukuwa umeme ambazo zinazunguka kiini.

Katika kiini cha atomi pia kunatokea mabadiliko na mipasuko inayojulikana kuwa **Radioactive** kutoka kwenye elementi. Katika mipasuko hii ya kiini, mgeuko wa elementi moja kwenda nyengine na maada kutoweka na kugeuka kuwa nishati, na mabadiliko haya pia yamefanyiwa mahesabu na myahudi Einstein (alikufa mwaka 1375 A.H 1955 M). Hivyo, kama ilivyo kwenye mimumunyo, pia kwenye elementi mabadiliko yanatokea kutoka hali moja kwenda nyengine.

Kila maada iwe ilio hai au isio hai inabadilika, tuseme kongwe hupotea na mpya kutokea. Leo kile kilicho hai, wanyama au mimea havikuwepo mwanzo. Kulikuwepo viumbe wengine. Na baada ya muda pia, viumbe hai vilivyopo sasa vitatoweka na hakuna kitakachobaki, viumbe hai vingine vitatokea. Hivyo ilivyo kwenye viumbe visivyo hai. Kila kiumbe hai na kisio hai kwa mfano elementi chuma, mmumunyo wa jiwe, mfupa, maada zote na chembe chembe zote hubadilika. Yani kongwe kutoweka na mpya kutokea. Sifa za maada iliopo na ile iliotoweka zikifanana basi mtu hawezi kuelewa mabadiliko haya na anaendelea kudhania kwamba maada hiyo bado ipo. Swala hili mfano wake ni kama kwenye sinema, kwenye mkanda wa filamu inayoendelea kunakuwa na harakati kila wakati picha nyengine inakuja na inapokwenda, basi watazamaji tukio hili hawalielewi na kudhania kwamba ni picha moja hiyo inayoendelea. Karatasi inapochomeka na kuwa jivu, kwa kuwa tumefahamu mabadiliko haya tunasema karatasi imetoweka na kuwa jivu. Barafu inapoyayuka tunasema barafu imetoweka na kuwa maji. Maelezo zaidi kuhusiana na maada ya kisasa imeelezwa kwenye kitabu **(Se'adet-i Ebediyya)** ukurasa wa 546, 971 na 1041.

Kwenye mwanzo wa kitabu **Sharh al-'Aqa'id**: kinasema kwamba, kwa sababu ya kuwa viumbe wote ni alama ya upatikanaji wa Allahu taala, na kuonesha upatikanaji wake, viumbe wote

wanaitwa alam. Pia kila tabaka kutoka kwenye viumbe wenye umbo moja linaitwa alam. Kwa mfano: aalam ya watu, aalam ya malaika, aalam ya wanyama, aalam ya visio hai n.k. au kila dutu inaitwa aalam.

Katika ukurasa wa 441 wa kitabu Sharh al-Mawaqif[1] kinasema kwamba, aalam ni **hadithi** yaani kila kitu kimeumbwa. Yaani vilitokea baada ya kutokuwepo. (Pia tumeelezea juu kwamba kila wakati viumbe vinatokea kutokana na kwa vyengine). Maada na tabia za dutu pia ni hadithi. Kuhusu swala hili kuna kauli nne.

1- Kulingana na Waislamu, Mayahudi, Wakristu na Majusi (wanao abudu moto/magician) wanasema maada na tabia za dutu zote mbili ni hadithi.

2- Kulingana na Aristotle na wafuasi wake wanafalsafa, wanasema maada na tabia za dutu zote ni kadim (zamani). Maelezo ya kisasa ya kimiya yanaeleza kuwa maneno ya Aristotle na wenzake ni ya uwongo. Wale wanaoamini na kusema hivyo wanatoka kwenye Uislam na kuwa kafiri. Hata Ibn Sina [2] na Muhammad Farabi[3] walisema hivyo.

3- Kulingana na wanafalsafa waliomtangulia Aristotle wanasema maada ni ya zamani lakini tabia zake (sifa) ni hadithi. Leo wanasayansi wengi wana itiqadi potofu hii.

4- Hakuna aliyesema kwamba maada ni hadithi na sifa zake ni kadim (zamani). Calinos yeye katika kauli nne hizi hakusema kitu.

Waislamu kwa njia mbali mbali wanathibitisha kwamba maada na sifa zake ni hadith ya kwanza, ni kwamba maada na chembe chembe zake zote zinabadilika mara kwa mara.

---

[1] Mwandishi wa sharh-I mawaqif Sayyid Sharif Ali Jurjani alikufa mwaka 816 H. 1413 M. kwenye mji wa Shiraz.

[2] Ibn Sina Huseyn alikufa mwaka 428 H. 1037 M.

[3] Muhammad Farabi alikufa mwaka 339 H. 950 M.

# SALAFIYYA

Mwanzo wa yote tutasema kwamba vitabu vilivyoandikwa na wanazuoni wa Ahl as-Sunna "rahmatullahi alaihim" havitaji chochote kinachohusiana na jina “Salafiyya” au “madhehebu ya salafiyya”. Majina haya yaliyozushwa baadae na watu wasiokuwa na madhehebu (La madhhab) yameenea miongoni mwa waturuki kupitia vitabu vya La madhhab vilivyotafsiriwa kwa kituruki kutoka lugha ya kiarabu na watu wasio na elimu kuhusu dini. Kulingana nao: “Salafiyya ni jina la madhehebu ambayo yamekuwa yanafatwa na Sunni wote kabla madhehebu ya Ash’ariyya na Maturidiyya hayajaanzishwa. Walikuwa ni wafuasi wa Masahaba na Tabi’in. Madhehebu ya salafiyya ni madhehebu ya Masahaba, Tabi’in na Taba at-Tabi’in. Kitabu cha kwanza kutetea madhehebu ya Salafiyya kilikuwa **Fiqh al-akbar** kilichoandikwa na al-Imam al-A’zam. Al-Imam al-Ghazali aliandika kwenye kitabu chake **Iljam al-awam ‘ani-l-kalam** kwamba madhehebu ya Salafiyya yalikuwa na nguzo saba. ‘Ilm al-kalam ya mutaakhirin (waliokuja baadae) ilianza na al-Imam al-Ghazali. Baada ya kusoma madhehebu ya ‘maulamaa’ wa kalam wa mwanzo na fikra za wanafalsafa wa kiislam, al-Imam al-Ghazali alifanya mabadiliko katika njia za ufundishaji wa ‘ilm al-kalam. Aliingiza masomo ya falsafa kwenye ‘ilm al-kalam kwa wazo la kuzikanusha. Ar-Radi na al-Amidi waliunganisha pamoja kalam na falsafa na kuvifanya kuwa tawi la Elimu. Na Baydhawi alivifanya kalam na falsafa kuwa havitenganishwi. ‘Ilm al-kalam ya mutaakhirin ilizuia kuenea kwa madhehebu ya Salafiyya. Ibn Taimiyya na wafuasi wake kina Ibn al-Qayyim al-Jawziyya walijaribu kuimarisha madhehebu ya Salafiyya na baadae yaligawika makundi mawili. Salaf wa mwanzo hawakuelezea kwa undani kuhusiana na sifa za Allahu taala au nass (aya) za mutashabih. Salafi waliofuata walikuwa na hamu ya kueleza kwa undani. Hali hii ilionekana wazi na Salafi waliokuja baadae kama Ibn Taymiyya na Ibn al-Qayyim al-Jawziyya. Salafi wa mwanzo na wa mwisho kwa pamoja wanaitwa **Ahl as-Sunna al-khassa**. Watu wa kalam miongoni mwa Ahl as-Sunna walitafsiri baadhi ya nass lakini Salafiyya walizikanusha. Walisema kwamba uso wake Allah na kuja kwake ni tofauti na nyuso za watu na kuja kwao, Salafiyya wao wanatofautiana na Mushabbih.”

Sio sahihi kusema kwamba madhehebu ya **al-Ash’ari** na **al-Maturidi** yalianzishwa baadae. Maimamu wawili wakubwa hawa

walifafanua elimu ya itiqad na imani iliofundishwa na Salaf as-salihin, wakaiandaa kwenye darasa na kuichapisha, kuifanya ieleweke kwa vijana. Al-Imam al-Ash'ari alikuwa kwenye mstari wa wafuasi wa al-Imam ash-Shafi'i. Na al-Imam al-Maturidi alikuwa kwenye mstari wa wafuasi wa al-Imam al-A'zam Abu Hanifa. Al-Ash'ari na al-Maturidi hawakwenda nje ya madhehebu ya waalimu wao, hawakuanzisha madhehebu mapya. Hawa wawili pamoja na waalimu wao na maimamu wa madhehebu manne walikuwa na madhehebu ya aina moja. Madhehebu yanayojulikana wazi kwa jina **Ahl as-Sunna wal-jamaat**. Malengo ya msingi yalioshikwa na kundi la watu hawa ni sawa na malego ya msingi yalioshikiliwa na Sahabat al-kiram, Tabi'in na Tabi' at-Tabi'in. Kitabu kinachoitwa **Fiqh al-akbar** kilichoandikwa na al-Imam al-A'zam Abu Hanifa kinatetea madhehebu ya Ahl as-Sunna. Neno 'Salafiyya' halipatikani katika kitabu hicho au katika kitabu cha al-Imam al-Ghazali **Iljam Al-awam 'ani-l-kalam**. Vitabu hivi viwili na **Qawl al-fasl**, moja ya fafanuzi za kitabu Fiqh al-akbar, kinafundisha madhehebu ya Ahl as-Sunna na kujibu makundi ya wazushi na wana falsafa. Al-Imam al-Ghazali anaandika katika kitabu chake **Iljam al-awam**: "ndani ya kitabu hiki nitaelezea kwamba madhehebu ya salafi ni sahihi na kweli. Nitaelezea kwamba wale wanaoachana na madhehebu haya ni wenye bid'a (uzushi). Madhehebu ya salafi maana yake ni madhehebu yalioshikiliwa na Sahabat al-kiram na Tabi'in. Misingi muhimu ya madhehebu haya ni saba." Kama inavyoonekana, kitabu **Iljam** kinaandika misingi saba ya madhehebu ya salafi. Kusema kwamba ni misingi ya madhehebu ya "salafiyya" ni kupotosha maandishi ya kitabu na kumkashifu al-Imam al-Ghazali. Kama ilivyo kwenye vitabu vya Ahl as-Sunna vyote, imeandikwa chini ya viingilio 'Salaf' na 'Khalaf' kwenye mlango unaohusiana na "Kutoa Ushahidi" katika kitabu **Durr ul-Mukhtar**, kitabu cha Fiqh chenye thamani: "Salaf ni sifa ya Sahab na Tabi'in. Pia wanaitwa **Salaf as-salihin**. Na 'ulamaa' (wanazuoni) wa Ahl as-Sunna wanaofuata Salaf as-salihin wanaitwa **'Khalaf.'"** Al-Imam al-Ghazali, al-Imam ar-Razi na al-Imam al-Baydhawi, ambao walipendwa na kuheshimiwa zaidi ya wote na 'ulamaa' (wanazuoni) wa Tafsiri, wote walikuwa ndani ya madhehebu ya Salaf as-salihin. Makundi yenye bid'a (uzushi) waliojitokeza katika enzi zao walichanganya 'ilm al-kalam na falsafa. Kwakweli walianzisha imani yao kutegemea falsafa. Kitabu **al-Milal wa-n-**

**nihal** kinatoa maelezo kwa undani kuhusu itiqad zinazofuatwa na makundi ya wazushi hao. Hakuna nadharia za kifalsafa au njia ya kifalsafa katika maandishi (kazi) ya al-Baydhawi, kwenye tafsiri ya **Shaikh-Zada**, hoja zenye thamani kubwa zaidi, ni tuhuma mbaya sana kusema kwamba imamu watukufu hawa walifuata falsafa. Hisia ya kukanusha hii iliambatanishwa kwa maulamaa wa Ahl as-Sunna na Ibn Taymiyya kwenye kitabu chake **al-Wasita**. Zaidi ya hayo, kuelezea kwamba Ibn Taymiyya na mfuasi wake Ibn al-Qayyim al-Jawziyya walijaribu kurekebisha madhehebu ya salafiyya ni kutoa ushahidi muhimu unaoonyesha namna watu waliopo kwenye njia sahihi wanavyotofautiana na wale walioangukia kwenye makosa. Kabla ya watu hawa wawili dhehebu linaloitwa “Salafiyya” halikuwepo, wala neno “Salafiyya” inakuaje wakasema kwamba walirekebisha madhehebu ya Salafiyya? Kabla ya hawa wawili, palikuepo dhehebu moja sahihi, dhehebu la “Salaf as-Salihin", ambalo liliitwa **Ahl as-Sunna wal-jamaat**. Ibn Taymiyya alijaribu kubadilisha dhehebu sahihi hili na kuvumbuwa uzushi mwingi. Chanzo cha vitabu, maneno na uzushi, mawazo yenye uzushi ya watu wale wasio na madhehebu (La-madhhabi) na wageuzi wa dini uzushi uliorithishwa na Ibn Taymiyya ili kudanganya Waislamu kwamba njia yao ya uzushi ndio njia sahihi, wazushi hawa walianzisha hila/plan yenye utata. Waligundua jina “Salafiyya” kutoka kwenye neno “Salaf as-Salihin” ili wathibitishe bid’a na mawazo ya uzushi ya Ibn Taymiyya na kuelekeza njama kwenye msimamo huu, waliambatanisha dhana za kifalsafa na bid’a kwa maulamaa wa kiislam, ambao ni warithi wa Salaf as-Salihin, na kuwalaumu kuacha jina walilovumbua la Salafiyya. Walimueka mbele Ibn Taymiyya kama mujtahid kama shujaa alierudisha Salafiyya kwenye hali nzuri. Kwa ukweli, wanazuoni wa Ahl as-Sunna "rahmatullahi alaihim", ambao ni warithi wa wanazuoni wanaoitwa Salaf as-Salihin, wanalinda mafundisho ya İtiqad ya Ahl as-Sunna ambayo yalikuwa madhehebu ya Salaf as-Salihin, na katika vitabu ambavyo wameandika hadi enzi zetu na vile wanavyoendelea kuandika hadi leo, wanaeleza kwamba Ibn Taymiyya, ash-Shawkani na wengineo waligeuka kutoka kwenye njia sahihi ya Salaf as-Salihin na wamekuwa wanaelekeza Waislamu kwenye adhabu kali na moto.

Watu wanaosoma vitabu **at-Tawassuli bi-n-Nabi wa bi-s-Salihin, Ulema al-muslimin wal- mukhalifun, Shifa’ as-siqam** na

dibaji zake, **Ta’thir alfu’ad min danasi-l-itiqad**, atagundua kwamba waanzishaji wa itiqadi potofu inayoitwa “New Salafiyya” Salafiyya mpya wanaongoza Waislamu kuelekea adhabu kali na kuteketeza Uislam kwa ndani.

Siku hizi, baadhi ya midomo mara nyingi hutumia jina “Salafiyya”, kila Muislam anafaa kujua vizuri kwamba katika Uislam hakuna kitu kwa jina la madhehebu ya Salafiyya lakini kuna madhehebu ya Salaf as-Salihin pekee, ambao ni Waislamu wa karne za kiislam mbili za mwanzo ambazo zilisifiwa kwenye hadithi sharif. Wanazuoni wa kiislam walioishi kwenye karne ya tatu na ya nne wanaitwa khalaf as-Sadiqin. Itiqadi ya watu waheshimiwa hawa inaitwa madhehebu ya Ahl as-Sunna wal-jamaat. Haya ni madhehebu ya iman, nguzo za iman. Imani iliongoza masahaba watukufu na tabi’in ilikuwa moja. Hakukupatikana tofauti kati ya itiqadi zao. Leo Waislamu wengi ulimwenguni wapo kwenye madhehebu ya Ahl as-Sunna. Makundi sabini na mbili ya wazushi yote yalitokea baada ya karne ya pili ya Uislamu. Waanzilishi wa baadhi ya makundi haya waliishi mwanzo, lakini ilikuwa baada ya Tabi’in, vitabu vyao viliandikwa na kutokea kwenye makundi na kuharibu itqad ya Ahl as-Sunna.

Rasulullah "alaihis-salaam" alileta itiqad ya Ahl as-Sunna, Masahaba watukufu walichukuwa mafunzo haya ya imani kutoka kwenye chimbuko. Na Tabiin idhaam, nao walijifunza mafunzo haya kutoka kwa maswahaba watukufu. Na kutoka kwao walijifunza urithi wao. Kwa njia hiyo mafunzo ya Ahl as-Sunna yalitufikia kwa Tawatur. Akili haiwezi kubadilisha wala hazisaidii kufahamu. Kwa kusema, akili ni lazima kuzifahamu, kujua kwamba ni sahihi na kujua umuhimu wake. Wanazuoni wote wa hadithi walikuwa kwenye itiqad ya Ahl as-Sunna. Maimamu wa madhehebu manne nao pia walikuwa kwenye madhehebu haya. Pia al Maturidi na al-Ash’ari, maimamu wawili wa madhehebu yetu ya itiqadi, walikuwa kwenye madhehebu ya Ahl as-Sunna. Wote maimamu wawili hawa walieneza madhehebu haya. Mara kwa mara walikuwa wanalinda madhehebu haya dhidi ya wazushi na dhidi ya materialist, ambao walikuwa wamedidimia kwenye falsafa za wagiriki wa zamani. Hata hivyo, walikuepo kwa wakati mmoja, waliishi katika sehemu tofauti na namna yao ya kufikiria na jinsi ya kutoa hukumu kwa watenda maovu ilikuwa tofauti, kwa hiyo mtindo wa ulinzi waliotumia, na majibu yaliyotolewa na wanazuoni wakubwa wa Ahl as-Sunna hawa

ilikuwa tofauti. Lakini haya hayamaanishi kwamba watu hawa walikuwa na madhehebu tofauti. Mamia ya maelfu ya wanazuoni na maauliyaa waliokuja baada ya maimamu wataalamu hawa walisoma vitabu vyao na kwa jumla walisema kwamba watu hawa walikuwa kwenye madhehebu ya Ahl as-Sunna. Wanazuoni wa Ahl as-Sunna walichukuwa nass pamoja na maana yake. Kwa kusema walitoa tafsiri za aya na hadithi zenye uhakika, na hawakufafanuwa nass (taawil) au kubadilisha/kugeuza maana hii isipokuwa palikuwepo dharura kufanya hivyo. Na kwa hiyo, hawakufanya mageuzi yoyote kutumia akili zao binafsi au mawazo. Lakini watu ambao walikuwa kwenye makundi ya uzushi na La-madhhabi (wasio na madhehebu) hawakusita kugeuza mafunzo ya imani na ibada kama walivyosoma kutoka kwa wanafalsafa wa kigiriki na kutoka kwa wanasayansi wa kisham ambao walikuwa wapinzani wa Uislam.

Dola la ki Ottoman, ambalo ni walinzi (guardian) na watumishi wa Ahl as-Sunna lilisambaratishwa na kushindwa kuendelea kwa karne kutokana na njama zilizofanywa na mafreemason, misionari na utawala mbaya ulioletwa na Waingereza, ambao walihimiza majeshi yao ya wasio na madhehebu (La-madhhabi) kutumia fursa hii. Pamoja na uongo mkubwa na njama, walianza kuwavamia Ahl as-Sunna na kuuvunja Uislamu kwa ndani, hasa katika nchi kama Saudi Arabia, nchi ambamo wanazuoni wa Ahl as-Sunna hawaruhusiwi kuongea. Kipimo cha dhahabu kisicho hesabika kilichomilikiwa na mawahabi kilisaidia dhuluma hii kuenea ulimwenguni kote. Kama inavyoeleweka kutoka kwenye ripoti kutoka Pakistan, India na nchi za Africa, baadhi ya watu wa dini wenye elimu ndogo ya dini na wasiomuogopa Allah walipewa nyadhifa/kazi na majumba makubwa kwa kuwasaidia madhalimu hawa. Hasa njama zao za kudanganya vijana na kuwapoteza kutoka kwenye madhehebu ya Ahl as-Sunna ziliwawezesha kupata faida mbaya hizi. Moja kati ya vitabu walivyoandika, ili kupoteza wanafunzi kwenye madrasa na watoto wa Waislamu, mwandishi anasema: “nimeandika kitabu hiki na wazo la kukomesha madhehebu na kusaidia kila mtu kuishi kwenye madhehebu yake kwa Amani”. Mtu huyu anamaanisha kwa ufumbuzi wa kutokomeza madhehebu ni kuvamia madhehebu ya Ahl as-Sunna na kudhalilisha wasomi wa Ahl as-Sunna. Anachoma kisu kwenye Uislam, halafu anasema anafanya hivi ili Waislamu waishi kwa

Amani. Katika sehemu nyingine kwenye kitabu hiki, anasema: “mtu mwenye akili akifikiria, atalipwa thawabu kumi, akikosa atalipwa thawabu moja”. Vile vile, kila mtu hata akiwa mkristu au mshirikina, atalipwa kila wazo lake na atapata thawabu kumi kutokana na mawazo yake sahihi! Angalia jinsi gani alibadilisha hadithi as-sharif ya mtume "alaihis-salaam" na jinsi anavyo cheza njama zake! Hadithi as-sharif inaeleza: **“mjitahid akifanikiwa kuchambua sheria kutoka kwenye aya tukufu au kutoka kwenye hadithi as-sharif atapata thawabu kumi, akikosea atapata thawabu moja.”** Hadithi as-sharif hii inaonyesha kwamba thawabu hizi hazitapewa kila mtu anayefikiria lakini zinapewa mwanazuoni Muislam ambae amefikia daraja la İjtihad, na kwamba zitalipwa sio kwa kila wazo lake lakini kwa kazi yake ya kuchambua sheria kutoka kwenye nass. Kwa kuwa kazi yake ni ibada, kama ibada zengine, atalipwa thawabu.

Katika enzi za Salaf as-Salihin na enzi za mujtahid ambao walikuwa warithi wao, mfano, hadi mwisho wa karne ya nne ya Uislam, kila jambo linalojitokeza kutokana na mabadiliko ya maisha na hali, mujtahid walifanya kazi usiku na mchana na kutafuta jinsi mambo yanayoweza kutatuliwa kulingana na chimbuko nne zinazoitwa **al-adillat ash-Shariyya**, na Waislamu wote walitekeleza hayo kwa kufuata mapendekezo ya maimamu wa madhehebu na wanazuoni wakubwa hao ambao walifanya hivyo walipewa thawabu kumi au moja. Baada ya karne ya nne, watu waliendelea kufuata mawazo ya mujtahid. Katika muda mrefu huu hakuna Muislam yoyote aliepotea au kupata matatizo kuhusu jinsi ya kutenda. Katika mda huo, hakuna mwanazuoni au mamufti waliokuwa na elimu ili kuwawezesha kupata daraja la saba la ijtihad, kwa hivyo, leo tunafaa kujifunza kutoka kwa Waislamu wanaoweza kusoma na kuelewa vitabu vya mwanazuoni mmoja kati ya madhehebu manne, na kutokana na tafsiri zake na kupata ibada zetu za kila siku. Allahu taala aliidhinisha sheria za kila kitu kwenye Quran tukufu. Mtume wake Muhammad "alaihis-salaam" alizifafanua zote. Na wanazuoni wa Ahl as-Sunna kujielimisha yote kutoka kwa sahabat al-kiram, waliandika sheria hizo kwenye vitabu vyao. Vitabu hivi vinapatikana ulimwenguni kote hivi sasa. Jambo jipya lolote ambalo litajitokeza kote ulimwenguni hadi siku ya kiama linaweza kutatuliwa kutokana na mafundisho yaliyomo kwenye vitabu hivi. Uwezekano huu ni miujiza ya Quran tukufu na

karama ya wanazuoni wa kiislamu. Lakini ni muhimu sana kujifunza kwa kumuuliza Muislamu wa Kisunni sahihi. Utakapomuuliza La-madhhabi (asio na madhehebu) atakupoteza kwa kukupa jibu ambalo haliendani na vitabu vya fiqh.

Nyuma tumefafanua jinsi gani vijana wamedanganywa na La-madhhabi hao wasiokuwa na elimu ambao wameishi katika nchi za kiarabu kwa miaka michache na kujifunza namna ya kuongea kiarab. Wamepoteza muda wao kwa kuishi maisha ya kifahari, burudani na kutenda maovu na halafu kupata vyeti kutoka kwa La-madhhabi ambao ni maadui wa Ahl as-Sunna, kisha walirudi nyumbani Pakistan au India. Vijana ambao waliviona vyeti vyao bandia na kuwasikia wakisema kiarabu walidhani kwamba watu hawa ni wataalamu wa dini, hali ya kua hawafahamu vitabu vya fiqh hata kidogo na hawajui chochote kuhusiana na mafundisho ya fiqh katika vitabu. Kwa kweli hawaamini mafunzo ya kidini haya, wanayaita uzushi. Zamani wanazuoni wa kiislam walitoa majibu ya maswali walioulizwa kwa kuangalia vitabu vya fiqh na kujibu waliowauliza majibu walipata lakini mtu La-madhhabi kwa kutoweza kusoma au kuelewa kitabu cha fiqh, atapoteza muulizaji kwa kusema chochote kinachotokea kwenye kichwa chake na akili zake duni na atamsababisha kwenda motoni, kuhusiana na hii mtume "swallallahu alaihi wa sallam" alisema **“mwanazuoni mzuri ndio mbora katika watu. Na mwanazuoni mbaya ndio mbaya zaidi wa binadamu”** hadithi hii inaonesha kwamba wanazuoni wa Ahl as-Sunna ndio bora zaidi katika jamii, na La-madhhabi ndio wabaya zaidi kati ya binadamu, kwa sababu wa mwanzo anaongoza watu kumfuata Rasulullah, mfano kwenda peponi na wale wengine wanaongoza watu kwa fikira za uzushi na hatimae kwenda motoni.

Ustadh Ibn Khalifa Aliwi, mtu muhimu kutoka chuo cha Uislamu (Islamic University of Jami’al-Azhar) anaandika kwenye kitabu chake **Aqidat as-Salafi wal-khalaf: "**kama Allama Abu zuhra anaandika kwenye kitabu chake **tarikh al-madhahibul-İslamiyya**, baadhi ya watu ambao walijitenga na madhehebu ya Hanbali kimawazo katika karne ya nne baada ya hijra walijiita **Salafiyyin**. Abu-l-Faraj Ibn al-Jawzi na wanazuoni wengine katika madhehebu ya Hanbali pia walitangaza kwamba Salafi hao hawakuwa wafuasi wa Salaf as-Salihin na kwamba walikuwa wenye kushikilia bid’a, kuwa kwenye kundi la Mujassima, walizuia fitna hii kuenea. Kwenye karne ya saba Ibn Taymiyya alianzisha tena fitna hii. La-madhhabi

walijiita jina “Salafiyya” na kumuita Ibn Taymiyya “imam mkuu wa salaf”. Neno hili linaweza kuwa sahihi kwa upande mmoja kwasababu neno “Salaf” halikuwepo kabla yake. Kulikuwepo Salaf as-Salihin ambao madhehebu yao ilikuwa ya Ahl as-Sunna. Itqad za uzushi za Ibn Taymiyya zimekuwa chanzo cha mawahabi na Lamadhhabi wengine. Ibn Taymiyya alifundishwa kulingana na madhehebu ya Hanbali yani alikuwa Sunni. Lakini, pale akili zake zilipozidi na kufikia daraja la kutoa fatwa, alianza kujiona mwenye akili zaidi kuliko wanazuoni wa Ahl as-Sunna. Kuongezeka kwa akili zake kulimfanya kuwa mzushi, hakuwa tena kwenye madhehebu ya Hanbali kwasababu, kuwa katika moja ya madhehebu manne, inalazimisha mtu kushikilia nguzo za Ahl as-Sunna. Mtu ambaye hashikilii nguzo za Ahl as-Sunna hawezi kusema kwamba yupo kwenye madhehebu ya Hanbali. La-madhhabi wanachukuwa kila fursa kudhalilisha watu wa dini ya kisunni wanapotimiza wajibu wao nchini mwao. Wanakataza watu kusoma vitabu vya ki sunni na kupata mafunzo ya Ahl as-Sunna. Kwa mfano, mtu La-madhhabi, lilipotajwa jina la mwanazuoni wa kweli alisema, “mwana fizikia au kimia ana biashara gani kwenye elimu ya dini? Anafaa kufanya kazi kwenye tawi lake na sio kuingilia mambo yetu.” Mawazo gani ya kijinga haya! Anafikiri mwanasayansi hawezi kuwa na elimu ya dini. Hajui ukweli kwamba mwanasayansi Muislam anajua na kufikiria uumbaji kila wakati, anazingatia ukamilifu wa sifa za muumbaji ambazo zimetajwa kwenye kitabu cha uumbaji, na kuona uwezo mdogo wa viumbe ukilinganisha na nguvu za Allahu taala za milele, na kujua kwamba Allahu taala sio kama kila kitu na yuko mbali na kasoro za aina yote. Mjerumani maarufu Max Planck, alieleza hili vizuri kwenye kazi yake **Der Strom**. Lakini La-madhhabi mwenye akili mbovu akitegemea maandishi aliopata kutoka kwa watu wazushi kama yeye na kupata adhabu kutoka nje, anafikiria kwamba elimu ya dini anayo peke yake. Tunamuomba Allahu taala atuongoze na mtu mpotofu huyu. Allah pia tunamuomba awalinde vijana dhidi ya njama za wezi wa dini hawa. Amiin.

Kwa kweli, mwanazuoni anayesemwa alihudumia nchi yake vizuri kwa zaidi ya miaka thelathini katika nyanja ya madawa (pharmacy) na chemical engineering. Kwa muda huo huo kuchukuwa mafunzo ya dini na kufanya kazi usiku na mchana kwa miaka saba, alipewa tuzo ya ijaz ilyotolewa na wanazuoni wakiislamu wakubwa. Mtaalamu huyu hakupata nguvu kuandika

mawazo yake kwenye vitabu vyake vyovyote. Kila mara alijaribu kumpa mdogo wake maandishi yenye thamani ya wanazuoni wa Ahl as-Sunna ambayo yalipendwa na watu wanayoyafahamu kwa kuyatafsiri kwa lugha ya Kiarab au Kifursi. Hofu yake kuwa kubwa, alikuwa bado hajafikiria kuandika vitabu kwa miaka mingi. Alipoona hadithi sharif kwenye ukurasa wa kwanza wa **Sawaiqul Muhriqa, "fitna inapokuwa mbaya, yule anayejua ukweli anafaa kuambia wengine. Endapo hatofanya hivyo, atalaaniwa na Allah na watu wote!"** alianza kufikiria. Kwa upande mmoja, alipojifunza ukubwa wa wanazuoni wa Ahl as-Sunna kafahamu na kuelewa elimu ya dini na elimu ya sayansi ya wakati huo na jitihada zao kuhusu ibada na taqwa, aliona upole wake kwa upande mwengine, aliona kwamba watu waaminifu wachache ndio wenye uwezo wa kusoma na kuelewa vitabu vilivyoandikwa na wanazuoni wa Ahl as-Sunna na kwamba wajinga wamejichanganya na watu wa dini na kazi za dini na walikuwa wameandika vitabu vya uzushi alisikitika sana.

Mwanazuoni mkubwa Ibn Hajar al-Makki "rahmatullahi alaih" aliandika kwenye kitabu chake **Fatawa al-hadithiyya**: "Allahu taala alimfanya Ibn Taimiyya kuangukia kwenye uzushi na kuangamia. Alimfanya kipofu na kiziwi. Wanazuoni wengi walieleza kwamba vitendo vyake vilikua vya upotofu na maneno yake yalikuwa ya uongo, na walithibitisha hili kwa maandishi. Watu ambao walisoma vitabu vya wanazuoni Waislamu wakubwa Abu Hasan as-Subki, mtoto wake Taj-ad-din as-Subki na Imam al-izz ibn Jama'a, na wale waliosoma maandishi walisema na kuandika kwa kumjibu kwa wanazuoni wa Shafii, Maliki, Hanafi walioishi katika enzi hizo, wataona vizuri kwamba tuko sahihi."

Ibn Taymiyya alisingizia wanazuoni wa kisufi. Zaidi ya hayo, hakusita kuwavamia Hadhrat Umar na Hadhrat Ali, ambao walikuwa watu wakubwa katika Uislam. Maneno yake yalipita kikomo na sheria za adabu. Aliwasingizia wanazuoni wakiislam walioko kwenye njia sahihi kwamba wanashikilia bid'a, na ujinga.

Alisema: "maneno ya wanafalsafa wagirik yasiokubaliana na Uislam yaliwekwa kwenye vitabu vya watu wakubwa wakisufi na kujaribu kuthibitisha kwa kutumia fikra za uzushi na uongo." Vijana ambao hawajui ukweli wanaweza kupotezwa na maneno yake ya uongo. Kwa mfano, alisema: "watu wakisufi wanasema kwamba wanaona Lawh al-mahfuz. Wanafalsafa wengine kama Ibn Sina, anaiita an-nafs al-falakiyya. Wanasema kwamba moyo wa mtu

ukifika daraja la ukamilifu, moyo unaungana na an-nafs al-falakiyya au al-'aql al-fa'al anapokuwa macho au amelala, na moyo wa mtu unapoungana na viwili hivi, ambavyo vinasababisha kila kitu kutokea katika dunia, anaambiwa vitu vinavyopatikana ndani yake. Haya hayakusemwa na wanafalsafa wa kigirik. Yalisemwa na Ibn Sina na wengineo waliokuja baadae. Pia Imam Abu Hamid al-Ghazali, Muhyiddin Ibn al-Arabi na wanafalsafa kutoka Andalusi Qutb ad-din Muhammad ibn Sa'bin walisema maneno kama hayo. Ni maneno ya wanafalsafa. Vitu kama hivyo havipo katika Uislam. Kwa maneno hayo walitoka kwenye Uislam na kuwa mulhid kama mulhid wa kishi'a, Ismailiyya, Qaramitwa na Batiniyya. Kwenye kitabu cha Ibn Sina **Akhir al- isharat'ala maqami-l-'arifin** kuna maneno kama haya mengi. Imam Ghazali pia alisema maneno yanayofanana haya kwenye vitabu vyake kama **al-Kitab al-madnun na Mishkat al-anwar**. Kwa kweli rafiki yake Abu Bakr Ibn al-Arabi alijaribu kumuokoa kwa kusema aliyachukuwa kwenye wanafalsafa lakini alishindwa. Kwa upande mwengine, al-Imam al-Ghazali alisema kwamba wanafalsafa walikuwa makafiri. Wengine wanasema kwamba maneno hayo yaliambatanishwa kwa imam al-Ghazali ili kumuaibisha."

Taj ad-din as-Subki aliorodhesha mambo ambayo Ibn Taymiyya anatofautiana na Salaf as-salihin kama ifuatavyo:

1. Alisema: Talaka ikitokea ni lazima kulipa kafara kwa kuapa. Hakuna mwanazuoni wakiislam aliekuepo kabla yake aliesema kwamba kafara inalipwa.
2. Alisema: Talaka anayopewa mwanamke mwenye hedhi haiwi.
3. Alisema: Sio lazima kulipa swala ikiwa imekupita kimakusudi.
4. Alisema: ni mubaha (inaruhusiwa) kwa mwanamke mwenye hedhi kuzunguka kaaba wakati wa tawaf.
5. Alisema: talaka moja inayotolewa kwa jina la talaka tatu, bado ni moja. Hata hivyo kabla ya kusema hayo, mara kwa mara alisema kwa mda mrefu kwamba ijma' al-Muslimin hawakusema hivyo.
6. Alisema: ushuru ambao haulingani na Uislamu ni halali kwa wale wanaouomba. Ushuru unapokusanywa kutoka kwa wafanya biashara, unatolewa kama zaka hata ikiwa haikukusudiwa vile.

7. Alisema: maji hayawi najsi endapo panya au kitu kingine kimefilia ndani yake.

8. Alisema: inaruhusiwa kwa mtu mwenye janaba kusali sala za suna bila kuoga janaba usiku.

9. Alisema: masharti yanayotolewa na waqif hayafuatwi.

10. Alisema: mtu anayetofautiana na ijma' al-umma hawi kafiri au mwenye dhambi.

11. Alisema: Allahu taala ni ma hall-I hawadith na ameumbwa nachembe chembe zilizoungana pamoja.

12. Alisema: Quran tukufu iliumbwa kutoka kwa Dhat ya Allahu taala.

13. Alisema: ulimwengu pamoja na vilivyomo ni vya milele.

14. Alisema: Allahu taala anaumba vitendo vizuri.

15. Alisema: Allahu taala ana mwili na anabadilisha sehemu.

16. Alisema: moto sio wa milele. Utatolewa mwisho wake.

17. Alikanusha ukweli kwamba mitume ni maasum (hawana dhambi).

18. Alisema: Rasulullah "swallallahu alaihi wa sallam" hana tofuauti na watu wengine. Hairuhusiwi kuomba kwa kutumia jina lake.

19. Alisema: ni dhambi kwenda Madina na nia ya kumtembelea Rasulullah.

20. Pia alisema: ni haram ni dhambi kwenda huko kuomba shafa'a msamaha.

21. Alisema: vitabu vya **Tawrat** na **al-Injil** havikutofautiana ki lugha. Vilitofautiana kwenye maana.

Baadhi ya wanazuoni walisema kwamba mengi ya maneno ambayo yamenukuliwa hapo juu sio ya Ibn Taymiyya, lakini hakuna yoyote aliekanusha maneno yake kwamba Allahu taala ana eneo na aliumbwa kutokana na chembe chembe kwa kujumuika pamoja.

Hivi sasa umekuwa mtindo kumuiga Ibn Taymiyya. Wanalinda maandishi yake ya uzushi na kuzalisha vitabu vyake, hasa kitabu chake **al-Wasita**. Kuanzia mwanzo hadi mwisho, kitabu hiki kimejaa mawazo yake yanayotofautiana na Quran tukufu, hadithi sharif na ijma' al-Muslimin. Inaleta fitna kubwa na mgawanyiko kati ya wasomi na inasababisha uadui kati ya ndugu. Mawahabi wa India na watu wajinga kuhusu dini ambao walianguka kwenye njama zao katika nchi za Waislamu wengine wamemfanya Ibn Taymiyya kuwa bango lao na wamempa majina kama Mjitahid mkubwa na Sheikh al-İslam.

# KAMUSI

Maingizo yanayohusiana na **Tasawwuf** yanaweza kusomwa vizuri kutoka kwenye kitabu cha Hadhrat Ahmad al-Faruqi as-Serhindi **Maktubat.**

**adillat ash-Shar'iyya:** asili nne za Uislam: **al-Quran al-karim, hadithi as-sharif, ijma' al-Umma na qiyas al-fuqaha.**

**ahl:** watu; **Ahl al-Bayt**, watu wa karibu wa mtume (kulingana na **wanazuoni Waislamu**) Ali, Fatima, Hasan na Huseyn; **Ahl as-Sunna wal-jamaat.**

**a'immat al-madhahib:** wingi wa **imam al-madhhab.**

**Allah: Allahu akbar, Allahu taala.**

**Amin:** kubali dua yangu.

**Amru bi-l-ma'ruf wa-n-nahyu ani 'l-munkar:** uwajibu wa kufundisha maamrisho ya **Allahu taala** na kukataza makatazo yake.

**Ansar:** wakazi wa Madina waliokubali Uislamu kabla fathi Makka. **'aqa'id:** iman

**'Arafat:** sehemu ya wazi ilioko kilometer 24 kaskazini mwa mji wa Makka.

**'arif: alim** ni mtu anayejua yale yanayowezekana kujua.

**'Arsh:** mwisho wa mbingu saba.

**As-hab al-kaf:** waumini saba waliopata cheo cha juu kutokana na kuhama kwao kwenda sehemu nyengine ili kuokoa Imani yao makafiri walipovamia makazi yao.

**Basmala:** katika kiarabu "Bismillah Rahman Rahim".
**Batini:** mfuasi wa kundi la wazushi wa batiniyya.

**Fadila, Wasila:** daraja la juu sana kwenye pepo.

**Faqih:** mwanazuoni mkubwa wa fiqh; fuqaha' as-sab'a.

**Fardh:** vitendo vilivyoamrishwa na **Allahu taala** kwenye **Quran tukufu.**